# Nipashe

Ijumaa Januari 31, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580142


www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

## Watuhumiwa watano ujambazi wauawa wakipambana na polisi

UKURASA 3



Ukurasa 20
Ndoa ya kuungana na bilionea, tajiri 'akichacha ndio mwisho'

Ukurasa 18
Unataka kutajirika kupitia pilipili hoho? Ingia darasa kitaalamu

BUFE

Ijumaa Januari 31, 2020 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 15
Shinikizo la mabinti 10, pedi yafutiwa kodi

KILIMO PILIPILI KICHAA...
Mradi utakaoajiri vijana mamia Unguja

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MIAKA 20 iliyopita, Zanzibar ilikua mzalishaji mzuri wa zao la pilipili kichaa, ikisafirishwa nje ya nchi. Lakini leo hii, uzalishaji wake umepungua.

Zao la pilipili kichaa, ni miongoni mwa viungo vya mboga na limekuwa likitumika katika chakula. Wizara ya Biashara na Viwanda ya Zanzibar, hivi sasa imedhamiria kurejesha hadhi ya uzalishaji wa zao hilo, baada ya kuona inahitajika sana katika soko la ndani na nje ya nchi.

Hivi sasa wizara, kwa kushirikiana na Shirika la Biashara Zanzibar (ZSTC), imeshaandaa shamba darasa la pilipili kichaa lenye matarajio kuvunwa tani 200, mkakati unaoshirikisha mabaraza ya vijana ya mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja, ili vijana hao wajikite katika kilimo biashara cha zao hilo na kuondokana na ukosefu wa ajira.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI
Habari katika picha
Ukurasa 17

Suala la pamba: Wadau walilia bei, serikali lao pembejeo na ubora wake Ukurasa 14

UKURASA 13

# Rugemalira 'alipua bomu' mahakamani

• **Adai** kumwandikia Kamishna TRA kufichua ukwepaji kodi wa benki maarufu... *Endelea ukurasa 2*






Wataalam wa Kitengo cha Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), wakiwakagua abiria kwa mashine maalum za kupima joto la mwili, ili kubaini virusi vya homa ya Corona, waliowasili kwa ndege ya Qatar Airways, kwenye Jengo la Tatu la abiria, jijini Dar es Salaam jana. **Picha ndogo:** Ofisa Afya Mkuu Mazingira, Onesmo Kitange (kushoto), akimpima raia wa India, Maitrick Dave, aliyewasili kwa ndege ya Kenya Airways. **PICHA: BAHATI MOLLEL**

## Corona wazuia wanafunzi kurudi China

UKURASA 3



## Kina Lugola kitimoto Takukuru leo

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


MICHEZO SIMBA, YANGA VITANI MACHI 8 UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Rugemalira 'alipua bomu' mahakamani

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA James Rugemalira, amedai mahakamani kwamba ameandika barua kwenda kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kumwelezea namna benki ya Standard Chartered Hong Kong ilivyokuwa ikikwepa kodi na ushuru wa forodha.

Mshtakiwa huyo na wenzake wawili wanakabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha fedha.

Rugemalira alitoa hoja hiyo jana Mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, wakati kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa.

Alitoa madai hayo baada ya Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Maghela Ndimbo, kudai kuwa kesi ilipangwa kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wake bado haujakamilika.

Rugemalira aliomba ruhusa ya kuzungumza na aliporuhusiwa alidai kuwa Januari 24, mwaka huu, alizungumza na mwakilishi wa Takukuru alipotembelea mahabusu na akamkabidhi nakala ya barua hiyo aliyoandika kwenda kwa Kamishna Mkuu wa TRA lakini mpaka sasa hajapata majibu yake.

"Mheshimiwa Hakimu, naomba mahakama yako itakapopanga tarehe nyingine ya kutajwa, upande wa Jamhuri walete majibu kwa sababu wanaostahili kushtakiwa katika kesi hii ni benki hiyo lakini nashangaa kuona wengine wanaunganishwa kwa madai upelelezi haujakamilika.

"Mheshimiwa Hakimu upelelezi wa kesi hii hautakamilika. Kama kweli wanataka ukamilike, wafuatilie hiyo barua aliyowapelekea TRA," alidai Rugemalira.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itatajwa Februari 13, mwaka huu, na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali na Rugemalira, washtakiwa wengine ni Harbinder Sethi na Joseph Makandege.

Katika kesi ya msingi ya uhujumu uchumi namba 27/2017, Makandege anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kusababishia serikali hasara ya dola za Marekani 980,000 pamoja na utakatishaji wa Fedha.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka hayo Desemba 20, mwaka jana, baada ya kuunganishwa na washtakiwa Sethi na Rugemalira katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi.

INAENDELEA UK. 8



Mshauri wa chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, akionyesha fomu ya kugombea uwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, baada ya kukabidhiwa na Kaimu Katibu Mkuu wa chama hicho, Dorothy Temu (katikati), katika ofisi za chama hicho, Vuga mjini Zanzibar jana. Habari uk. 23. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kina Lugola kuwekwa kiti moto Takukuru leo

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), leo inatarajia kumuhoji aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, Kangi Lugola na wenzake wanaotuhumiwa katika utiaji saini makubaliano ya zabuni ya ununuzi wa vifaa vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Sakata hilo liliibuliwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Rais John Magufuli wakati akizindua nyumba za maofisa wa Jeshi la Magereza na askari Ukonga jijini Dar es Salaam, ambapo alisema mkataba huo ulisainiwa bila baraka za serikali na Bunge kwa Euro milioni 408 (zaidi trilioni moja).

Msemaji wa Takukuru, Doreen Kapwani, aliliambia Nipashe jana kuwa, taasisi hiyo itaanza kuwahoji watuhumiwa hao kuanzia leo yakiwa ni maagizo ya Rais John Magufuli kuhusiana na sakata hilo.

"Ni kweli wataanza kuhojiwa kesho (leo), hata jana (juzi) Mkurugenzi Mkuu Takukuru alisema hivyo, wataanza kuhojiwa kwa tuhuma zinazowakabili," alisema.

Ingawa Kapwani hakuwataja watu wengine watakaohojiwa mbali na Lugola, ambaye ni Mbunge wa Mwibara, mkoani Mara, lakini baadhi ya vyombo vya habari jana vilriwataja kuwa ni Thobias Andengenye, aliyekuwa Kamishna wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji; Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni na Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ramadhan Kailima.

Januari 27, wakati akimwapisha Waziri mpya wa Wizara hiyo, George Simbachawene Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Magufuli aliiagiza Takukuru kuchunguza suala hilo bila kuogopa mtu, na kwamba watakaobainika wachukuliwe hatua za kisheria. Pia alimkabidhi Waziri Simbachawene nyaraka zinazohusu mkataba huo aliouita mbovu uliosainiwa nje ya Tanzania.

Akifungua nyumba hizo, Rais Magufuli alisema ipo miradi ya ovyo iliyokuwa ikifanyika na kwamba alitegemea watu wangekuwa wanajifunza.

Rais Magufuli alisema: "Kitu kikubwa ni nini, watu kukosa uadilifu, hivi karibuni kulikuwa na mkataba mmoja wa ajabu unatengenezwa Wizara ya Mambo ya Ndani wenye thamani ya Uero milioni 408 (zaidi trilioni 1). "Mradi umetayarishwa na kusainiwa na Kamishna wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Andengenye haujapangwa kwenye bajeti haujapitishwa na Bunge."

"Wakati wa vikao na kampuni moja nafikiri kutoka Romania wahusika wote wa Tanzania walipokuwa wanakwenda kwenye majadiliano wanalipwa posho ya kikao dola 800 (sawa na Sh. milioni 1.8) bado kulipiwa tiketi ya ndege, mradi wa ovyo," alisema. "Wamesaini makubaliano ya pamoja, lakini ukitaka kuyavunja makubaliano hayo ya ndani yale ambayo yameanza kutekelezwa, lazima yaendelee kutekelezwa.

"Lugola nampenda sana, ni mwanafunzi wangu nimemfundisha Sengerema, pamoja na mwili wake ni mwanafunzi wangu, lakini kwenye hili hapana, nilitegemea hata hapa nisingemkuta, nasema kwa dhati," alisema.

Rais Magufuli alisema, "Kamishna Jenerali Andengenye nampenda sana ni mchapakazi, lakini kwenye hili hapana, nilitegemea hapa awe hayupo, hatuwezi kuendesha nchi kwa misingi ya ajabu namna hii."

Rais Magufuli alisisitiza kuwa yanayokwenda kununuliwa kwenye mkataba huo ni ya ovyo na ajabu. "Ndiyo maana ninasema ninampongeza sana Meja Jenerali Jacob Kingu ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kuwajibika... na hii imempa heshima kwamba angalau ametambua kwamba inawezekana haya hakuyafanya, lakini yeye ni Katibu Mkuu, amewajibika kwenye hilo, ninampongeza sana na nitaendelea kumheshimu, kama Meja Jenerali," alisema.

# Bunge laelezwa hali mbaya Stamico kifedha

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

BUNGE limetaarifiwa kuwa, Shirika la Madini la Taifa (Stamico) liko hoi kutokana na ukuaji wa gharama za uendeshaji kutoendana na ukuaji wa mapato ya shirika hilo.

Katika kipindi cha miaka mitatu kiwango cha gharama kwa mapato kimekuwa kikubwa, ambapo ni kati ya asilimia 101 na asilimia 206 ikiwa ni wastani wa asilimia 134.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), Dk. Raphael Chegeni, alitoa siri hiyo jana wakati akiwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na kamati yake kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

"Hali hii inadhihirisha kuwa utendaji wa Shirika hauzalishi mapato ya kutosheleza ambapo Shirika limekuwa likitumia wastani wa asilimia 134 ya mapato yake ghafi kwa ajili ya gharama za uendeshaji," alisema Chegeni.

Kutokana na kupungua kwa mtaji mwaka hadi mwaka, kamati hiyo imeliambia Bunge kwamba kumekuwa na ongezeko la matumizi ya shirika yasiyoendana na mapato.

Alisema matumizi ya shirika yamekuwa yakiongezeka kutoka Sh. bilioni 9.05 kwa mwaka 2016/17 hadi kufikia Sh. bilioni 10.16 kwa mwaka 2017/18 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 12.

Katika taarifa ya kamati hiyo, ukuaji wa gharama za uendeshaji hauendani na ukuaji wa mapato ya shirika, ambapo mapato ya shirika hilo yalishuka kutoka Sh. bilioni 6.33 kwa mwaka 2016/17 hadi kufikia Sh. bilioni 2.01 mwaka 2017/18 sawa na pungufu wa asilimia 48. Uchambuzi wa kamati hiyo ya uwekezaji wa mitaji ya umma, imeeleza zaidi kuwa athari nyingine ya kukosekana kwa mtaji katika Shirika la Madini la Taifa ni shirika kushindwa kulipa madeni yake.

Katika uchambuzi wake, kamati pia imelieleza Bunge kuwa imepima uwezo wa shirika hilo kwa kuangalia kigezo cha ukwasi na endapo Shirika lina uwezo wa kulipa madeni yake na limebainika kuwa wakati mali za muda mfupi za shirika zikiendelea kupungua, kiwango cha madeni ya muda mfupi kimekuwa kikiongezeka.

Kutokana na hali hiyo, Bunge limeishauri serikali kulifufua shirika hilo kwa kuondoa changamoto zote zilizopo kwa kuliongezea mtaji, kukamilisha uhamisho wa umiliki ili kulipa shirika uhalali wa kumiliki na kuisimamia miradi iliyokabidhiwa na kuliondolea shirika madeni makubwa yaliyorithiwa.

Serikali imefanya uwekezaji wa ndani katika jumla ya taasisi na mashirika 229, ambapo ina umiliki wa hisa asilimia 100.

HABARI KITAIFA

# Corona yazuia wanafunzi kurejea masomoni China

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SERIKALI imewazuia kwa muda wanafunzi wanaosoma nchini China ambao walirejea nyumbani kwa ajili ya likizo, kutorudi nchini humo mpaka hapo itakapopata taarifa za kidiplomasia kuhusiana na mwenendo wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na kirusi aina ya Corona.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni jijini hapa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akijibu swali la Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi, katika kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu.

Katika swali hilo, Chumi alitaka kujua serikali imejipangaje kukabiliana na ugonjwa huo.

"Tunatambua kuna wazazi wana watoto wanasoma nchini China na wengine wamesharudi likizo. Tunawasihi watoto hao wasiende kwanza China mpaka hapo tutakapopata taarifa za kidiplomasia," alisema Majaliwa na kuongeza:

"Wizara ya Mambo ya Nje (na Ushirikiano wa Afrika Mashariki) inaendelea kufanya mawasiliano na balozi zote mbili, China nchini Tanzania na Tanzania nchini China kuona mwenendo wa ugonjwa huo. Serikali itakaporidhika kwamba kule hali imepungua, tutatoa tamko kwa Watanzania walioko likizo hapa kurudi China kuendelea na masomo. Vinginevyo ikiendelea sana, serikali itatafuta utaratibu mwingine," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu alitoa wito kwa Watanzania kama ambavyo Wizara imetoa tahadhari, kila Mtanzania awe makini na wageni wanaoingia mpakani hususani ambao wamewekwa kuhakiki wanaongia nchini.

Aliwataka wataaamu hao kusisitiza wageni wanaongia nchini kutumia vifaa ambavyo vinaweza kutambua magonjwa mbalimbali ili kubaini ambao wana dalili za ugonjwa huo.

Alisema vifaa hivyo ni maalum kwa ajii ya kudhibiti kuingia kwa ugonjwa huo wa Corona hapa nchini.

Alisema serikali imeimarisha mawasiliano na ubalozi wa Tanzania nchini China kujua hali inaendeleaje na kwamba Balozi Mbelwa Kairuki

INAENDELEA UK. 8

# Polisi waua washukiwa ujambazi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JESHI LA Polisi mkoani Arusha, limesema limewaua watu watano wanaodaiwa kuwa majambazi sugu, wakati wakijiandaa kwenda kufanya uhalifu Simanjiro mkoani Manyara.

Aidha, katika tukio hilo jeshi hilo limesema limekamata pikipiki tatu, bastola moja bandia, bastola aina ya Chinese iliyofutwa namba na bunduki aina ya Shotgun Pump Action yenye namba 32265-02.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shanna, alisema jana kuwa watu hao waliuawa juzi majira ya saa 3.45 usiku katika eneo la njia panda ya Mateves, Kata ya Olmot, jijini Arusha.

Alisema tukio hilo lilitokea baada ya polisi kupata taarifa za siri kuwa watu hao walikuwa wamepanga kwenda wilayani Simanjiro kufanya uhalifu kwa kutumia pikipiki kupita barabara ya Afrika Mashariki (Baypass) kupitia Olasiti hadi mzunguko wa Kwa Mrombo na kuweka mtego.

"Tulipopata taarifa hizi tuliweka mtego kwa kutumia kikosi kazi cha askari jasiri, wakakamavu na wenye weledi wa hali ya juu katika eneo la njia panda ya Mateves," alisema Shanna.

Alisema katika eneo la mtego, ilipofika saa 3:45 usiku, askari hao waliona pikipiki tatu zikitoka upande wa Mateves kuelekea barabara mpya ya Afrika Mashariki ndipo walipozisimamisha. Badala ya kutii amri ya kusimama, watu hao walianza kuwafyatulia risasi polisi.

"Baada ya hali hiyo, polisi walianza kujibu mashambulizi kwa muda wa dakika 35. Majambazi wanne walifariki hapo hapo na mmoja aliyekuwa nyuma ya wenzake aligeuza pikipiki yake na kukimbia umbali wa mita 500 lakini naye alipigwa risasi na kudondoka," alisema.

Kamanda Shanna alisema baada ya kuwaua, polisi walikamata pikipiki tatu zenye namba za usajili MC 871 BWR aina ya Skygo, MC 555 CGE aina ya Kinglion na MC 478 AYV aina ya Toyo.

Alitaja vingine walivyowakuta navyo ni kuwa ni magazini mbili za Chinese Pistol ikiwa na risasi nane na nyingine risasi moja, maganda saba ya risasi ya Chinese Pistol, risasi mbili za bunduki ya Shotgun, maganda matano ya risasi ya Shotgun na simu mbili aina ya Tekno na moja aina ya Oking.

Alisema uchunguzi wa awali ulibaini bunduki hiyo aina ya Shotgun Pump Action iliibwa Januari 26, mwaka huu, majira ya saa 9:00 usiku nyumbani kwa Jackson Msangi baada ya majambazi hao kuvunja nyumba yake eneo la Burka, Kata ya Olasiti.

"Pia waliiba simu ya mkewe, Nikira Msangi, na baada ya tukio hilo waliitwa kutambua vitu vilivyokamatwa walitambua simu na silaha hiyo kuwa ni vyao," alisema.

Shanna alisema miili ya marehemu imehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru na kuomba wananchi kujitokeza kutambua miili hiyo ili wachukue ndugu zao kwenda kuahifadhi.

Kwa upande wao, Msangi na mkewe Nikira, walishukuru jeshi hilo kwa kuwakamata watu hao ndani ya kipindi kifupi tangu watoe taarifa ya kuvamiwa na kuporwa.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alipongeza jeshi hilo kwa kazi nzuri ya kukabiliana na ujambazi mkoani hapa na kuahidi kuzungumza na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali Simon Sirro, na viongozi wengine ili wawape zawadi askari waliopambana na majambazi hayo.


brac

**'TAARIFA YA KUHAMA'**

Tunapenda kuwataarifu wateja na wadau wetu kuwa ofisi za Makao makuu za

**BRAC TANZANIA FINANCE LTD**

na

**BRAC MAENDELEO TANZANIA**

zinahama kutoka Mbezi Beach, Makonde kuanzia tarehe **31/01/2020**

**Anuani mpya ni**

NATAI Plaza
Plot No. 17 - Coca Cola Road
Mikocheni Light Industrial Area

215610802



**TATHIMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII**

**TAARIFA KUHUSU MRADI TARAJIWA WA DHAHABU WA NYAMULILIMA, KWA AJILI YA KAMPUNI YA GEITA GOLD MINING LIMITED, WILAYA YA GEITA, MKOA WA GEITA**

Mradi tarajiwa wa uchimbaji wa dhahabu katika eneo la Nyamulilima upo ndani ya ukanda wa madini wa ziwa Victoria takribani kilometa 20 hadi 25 kwa njia ya barabara kutokea mji wa Geita. Mradi pendekezwa unamilikiwa na kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) ambayo ni kampuni tanzu ya AngloGold Ashanti. Mradi huu upo ndani ya leseni mahsusi ya uchimbaji madini yenye yaani ***Special Mining Licence (SML)*** namba 45/99 iliyotolewa Juni 1999. Sehemu ya leseni ulipo mradi ipo ndani ya kata Nyamwilolelwa, wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita.

Mgodi wa Geita umekuwa ukifanya uchimbaji wa madini kwa kutumia njia ya mashimo ya wazi na uchimbaji wa chini ya ardhi an uchenjuaji kwa kutumia sayanadi. Hata hivyo, rasilimali ya dhahabu iliyobaki kwa mgodi wa Geita inaonekana kuisha mwishoni mwa mwaka 2020. Hivyo, kwa mgodi wa Geita kuendelea kutoa mchango muhimu katika uchumi wa Tanzania, utafiti ulisaidia kugundua maeneo mengine mbadala ndani ya leseni yenye madini. Maeneo ya Nyamlilima yamethibitishwa kuwa na ukanda wenye hifadhi ya dhahabu ambao utaweza kupatikana na kuingizwa katika uzalishaji kwa kupitia njia ya uchimbaji wa mashimo ya wazi na pengine uchimbaji wa chini ya ardhi hapo baadae.

Hifadhi ya madini ya dhahabu iliyopopo na inayopendekezwa kuchimbwa kutoka eneo la Nyamlilima ni miongoni miradi ya uchimbaji ambayo itasaidia kuendelea kuwepo kwa shughuli za uchimbaji zinazofanywa kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML)hata baada ya mwaka 2020. Ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu, tathmini ya athari za kimazingira na kijamii inahitajika kama ilivyoainishwa katika Sheria ya usimamizi wa mazingira, 2004 na Sheria ya Madini, 2010.

Pia ili kukidhi mahitaji ya sheria ya mazingira ya taifa na kuhakikisha shughuli zinaendana na viwango vinavyokubalika kimataifa kwa ajili ya usimamizi wa mazingira na mahitaji ya kijamii; kampuni ya GGML imeiteua kampuni ya ushauri iitwayo MTL kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii zinazoweza kutokana na mradii. Utafiti huo utachunguza faida pamoja na athari na kuelezea hatua zote mbadala zitakazotumika ili kuongeza faida na kupunguza athari.

Ili kufikia mahitaji ya kisheria ya ndani ya nchi na yale ya kimataifa katika kufanya utafiti huu wa athari za kimazingira na kijamii, majadiliano na wadau wanaohusika na mradi ni muhimu. Na hivyo tangazo hili linawakaribisha wadau wote wenye maslahi, ushauri au taarifa muhimu kuhusu athari zozote ama za kimazingira au kijamii kuhusiana na mradi huu kuwasiliana kwa simu au kwa kutoa mawazo kwa Msahuri Mwelekezi kupitia anuani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mtendaji**
**MTL Consulting Company Limited,**
**Masaki, Nyumba namba 2,Kitalu 689,**
**S.L.P 77894, Barabara ya Sandvik**
**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel./Fax: +255 22 2600594**
**Cellular: +255 (0) 767 360 225**
**Email: emasasila@mtlconsulting-tz.com**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**
**S.L.P 63154, Regent Estate Plot No. 29/30,**
**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255 22 2774889**
**Email: dg@nemc.or.tz**

215596502

# Mke adaiwa kuua mume madai kunywea pombe fedha za shamba

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi Mkoani Rukwa linamshikilia mwanamke mmoja kwa tuhuma za kumuua mumewe kwa madai ya kuiba pesa walizoweka kwa ajili ya palizi shambani.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Justine Masejo, alisema tukio hilo lilitokea Januari 22, mwaka huu wilayani Sumbawanga na kumtaja mwanaume aliyeuawa ni Satiruni Sapi. Kamanda Masejo alisema mwanamke huyo ambaye hakumtaja jina, anadaiwa kumpiga mumewe na kipande cha mti kichwani na kumsababishia mauti.

Alisema kuwa chanzo cha tukio hilo ni ugomvi wa kifamilia kati ya Sabi na mkewe ambaye inadaiwa alichukizwa na kitendo cha mumewe kuchukua fedha walizokuwa wameziweka kwa ajili ya palizi la shambani na kwenda kununilia pombe.

"Baada ya kitendo hicho ndipo mkewe alipoanza kumpiga na alitumia kipande cha mti kumjeruhi, kisha alikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Sumbawanga kwa ajili ya kupatiwa matibabu, lakini alifariki dunia wakati anaendelea kupata matibabu siku hiyo," alisema Kamanda Masejo.

Kamanda Masejo alisema mtuhumiwa ameshakamatwa na baada ya kuhojiwa alikiri kutenda kosa hilo na atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi wa awali kukamilika.

Wakati huohuo, Kamanda Masejo alisema Polisi kwa kushirikiana na askari wa Shirika la Hifadhi ya Taifa (Tanapa) limekamata vipande 24 vya meno ya tembo baada ya kufanya upekuzi katika nyumba ya Philemon Ntibasiga (31). Masejo alisema meno hayo ya tembo yalikuwa yamehifadhiwa kwenye mabegi mawili ya mgongoni na nyingine kufungwa kwenye mifuko aina ya viroba na kuchanganywa na pumba za mahindi.



Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro (kushoto), akisalimiana na Mwenyekiti wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi wa nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SARPCCO), Kamishna Jenerali wa Jeshi la Polisi Zimbabwe, Tandabantu Godwin Matanga kabla ya mazungumzo yao katika makao makuu ya jeshi hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JESHI LA POLISI**

## Lori la mafuta laua watatu

**Na Gideon Mwakanosya,** TUNDURU

WATU watatu wamefariki dunia katika tukio la ajali ya lori la mafuta iliyotokea katika Kijiji cha Huria Wilayani Tunduru mkoani Ruvuma.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Saimon Maigwa, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kueleza kuwa lori hilo lenye namba za usajiri T 956 DJL lililokuwa limebeba petroli, lilidondoka na kusababisha vifo vya watu watatu akiwamo dereva wa gari hilo.

Alisema gari hilo lilikuwa likitokea Dar es Salaam kwenda mjini songea, lilikuwa likiendeshwa na Joseph Kilowe Mtitu (39).

Alisema watu wengine wawili waliofariki katika ajali hiyo majina yao hayajafahamika.

Kamanda Maigwa alisema chanzo cha ajali hiyo kinachunguzwa, na alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kutambua miili ya watu hao ambayo imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru.

Nipashe lilizungumza na mashuhuda wa tukio hilo akiwamo Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Huria, Shaibu Ngolonje ambaye alisema kuwa chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa gari hilo kushindwa kulimudu kwenye mteremko katika barabara ya kutoka Tunduru, Huria kuelekea Songea.

# Kanda ya Ziwa kutibiwa kifafa, degedege Bugando

**Na Mary Geofrey,** MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Bugando, imewataka wananchi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa kujitokeza kupata huduma ya matibabu ya kifafa na degedege.

Huduma hiyo imeanza kutolewa mwaka jana baada ya hospitali hiyo kununua mashine maalumu ijulikanayo kama EEG yenye uwezo wa kubaini ugonjwa huo.

Wito huo ulitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Bahati Wajanga, wakati akizungumzia mafanikio ya hospitali hiyo katika kipindi cha miaka minne ya Serikali wakati wa ziara maofisa Mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Maofisa hao wapo kwenye kampeni ijulikanayo kama 'Tumeboresha Sekta ya Afya' inalenga kuangazia mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya nchini.

Alisema tangu kuanzishwa huduma hiyo imefanikiwa kutibu wagonjwa 600 wa ugonjwa huo.

Naye Daktari Bingwa wa Watoto, Mishipa ya Fahamu na Ubongo, Dk. Yusuph Jamnagerwalla, alisema mashine hiyo inachukua vipimo vya mgonjwa kwa muda wa saa mbili na kutoa majibu ndani ya saa 25 hadi 48.

"Mashine hii ina uwezo wa kupima na kubaini ugonjwa huu ndani ya saa mbili na mgonjwa ataanzishiwa matibabu na kuna uwezekano wa kupona kuanzia wiki 14 hadi mwezi mmoja atakuwa amepona kabisa," alisema Dk. Jamnagerwalla.

Kuhusu sababu za kuwapo kwa ugonjwa huo, alisema walifanya utafiti mdogo na kubaini kuwa kati ya watu 100 wenye utindio wa ubongo asilimia 60 wanaugua kifafa.

Alisema watoto waliozaliwa na tatizo la ubongo wapo kwenye hatari ya kupata ugojwa wa degedege.

Alisema ugonjwa huo unawapata waliopooza na wanaokula nyama ya Nguruwe ambao wana virusi vinavyosababisha kifafa.

Dk. Jamnagerwalla alisema sababu nyingine ni ajali ambazo husababisha ugonjwa wa kifafa baada ya kupata majeraha kwenye ubongo.

Alisema wanatoa elimu kwa vituo vya afya na Zahanati mkoani humo kuwasihi watu wenye ugonjwa huo kujitokeza kupima na kuanza matibabu kwa sababu unatibika.

Alisema awali wagonjwa walikuwa wanakwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) hivyo kuwapo kwa huduma hiyo kutupunguza gharama kwa wagonjwa.

**TANGAZO**

VisionFund TANZANIA

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka ya sasa Tarehe 31/12/2019 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/09/2019 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 133 | 144 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 8,489 | 9,364 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushungulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima ya Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | | - | - |
| | Mikopo Halisi Iliyopo | 19,545 | 18,877 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,996 | 3,052 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika ,Mitambo na Vifaa | 1,813 | 1,888 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **32,975** | **33,325** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 1,794 | 2,310 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 4,190 | 4,171 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 327 | 326 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 214 | 214 |
| 27 | Zitakazolipwa Baadae | 838 | 780 |
| 28 | Dhima Nyingine | - | - |
| **29** | **Madeni** | **7,363** | **7,801** |
| | **JUMLA YA DHIMA** | | |
| **30** | **MALI/(DHIMA)HALISI (16 kutoka 29)** | **25,613** | **25,524** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,200 | 21,200 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 12 | 12 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 1,307 | 1,307 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 529 | 378 |
| 35 | Akauti Nyingine za Mtaji | 2,566 | 2,627 |
| 36 | **Stahiki ya Wenyehisa Chache** | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISANI** | **25,613** | **25,524** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | **1,640** | **1,640** |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | **1,725** | **1,820** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | **-** | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | **78%** | **77%** |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | **8.5%** | **9.1%** |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **359%** | **324%** |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **65%** | **63%** |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **79%** | **69%** |
| (vi) | Ongezeko la Amana | **-7.7%** | **-18.9%** |
| (vii) | Ongezeko la Mali | **-1.0%** | **-7.2%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 31/12/2019 | Robo ya Mwaka Linganishi 31/12/2018 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31/12/2019 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31.12.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 | Mapato ya Riba | 2,760 | 2,698 | 11,699 | 11,787 |
| 2 | Gharama za Riba | 4 | 109 | 244 | 497 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **2,756** | **2,589** | **11,455** | **11,290** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (186) | **(201)** | (428) | **(1,655)** |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **643** | **737** | **2,251** | **2,531** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (2) | 0 | (3) | (6) |
| | 6.2 Ada za Kamisheni | 443 | 468 | 1,651 | 1,599 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 203 | 269 | 603 | 938 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba :** | **3,062** | **3,362** | **12,749** | **12,883** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 1,582 | 1,719 | 6,534 | 6,950 |
| | 7.2 Gharama Nyingine | 1,481 | 1,643 | 6,215 | 5,933 |
| | 7.3 Ada na Kamisheni | | | | |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **150** | **(237)** | **529** | **(717)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10** | **Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **150** | **(237)** | **529** | **(717)** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | **326** | **364** | **334** | **364** |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 7,084 | (11,169) | 25,909 | (35,144) |
| 13 | Kipato kwa Hisa | 7,084 | (11,169) | 25,909 | (35,144) |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 | Vituo Vya Biashara | 54 | 54 | 54 | 54 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | 0.5% | -0.7% | 1.5% | -2.0% |
| (ii) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.6% | -0.9% | 2.1% | -2.9% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 90% | 101% | 93% | 93% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalisha | **24%** | **20%** | **77%** | **83%** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 DECEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2019)** | **21,200** | **1,513** | **204** | **2,123** | **25,040** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | **-** | **529** | **-** | **-** | **529** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | **(385)** | **(14)** | **443** | **45** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **21,200** | **1,657** | **190** | **2,566** | **25,613** |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2018)** | **21,200** | **2,329** | **215** | **2,345** | **26,089** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **(816)** | **(11)** | **(222)** | **(1,050)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **1,513** | **204** | **2,123** | **25,040** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 31/12/2019 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 31/12/2018 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2019 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31.12.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| **I:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| | Mapato/(Hasara)Hakisi | **150** | **48** | **529** | **(717)** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | | | | |
| | Hasara Katika Mali | 177 | 169 | 647 | 1,192 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (667) | 2,045 | 2,015 | 282 |
| | Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (497) | (1,506) | (672) | 785 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 56 | (199) | (327) | (241) |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo | 59 | (27) | (202) | 458 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| | **kwa shughuli za uendeshaji** | **(723)** | **529** | **1,990** | **1,760** |
| **II:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | | | | |
| | Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (102) | (168) | (860) | (726) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za uekezaji** | **(102)** | (168) | (860) | (726) |
| | | - | - | - | - |
| **III:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | (1,115) | (1,672) | (593) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (62) | - | 45 | (990) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za Kifedha** | **(62)** | **(1,115)** | **(1,627)** | **(1,583)** |
| **IV:** | **FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | | | | |
| | Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tastimu | (886) | (753) | (498) | (550) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 9,508 | 10,261 | 9,120 | 9,670 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu / Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **8,622** | **9,508** | **8,622** | **9,120** |

Katika kuaandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Yohane Ibrahim Kaduma ( Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 28 Januari 2020 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha ) | | 28 Januari 2020 |
| Emmanuel Shee (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 28 Januari 2020 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1 **Mwijage B Bishota (Mwenyekiti ya Bodi)** | | 28 Januari 2020 |
| 2 **Loyce Isanzu (Mwendeshaji)** | | 28 Januari 2020 |

## ADA NA GHARAMA

**Group Loans Product**

| | Product | Interest p.m. | VAT Inclusive Processing Fees |
|---|---|---|---|
| 1 | Group Biashara | 3% flat | 3% |
| 2 | Group Savings Group Loan | 3% flat | 2.5% |
| 3 | Group Jiendeleze | 2.5%flat | 3.5% |

**Individual Loans Product**

| | Product | Interest | Proc. Fee |
|---|---|---|---|
| 4 | Kitita | 2.5% flat | 2.5% |
| 5 | Premium | 2% flat | 2.5% |
| 6 | Uzalishaji | Btn 14% to 30% Declining balance and | 1.5% - 2.5% |
| 7 | Elimisha | 2.5% flat | 3.5% |

**Agriculture (Balloon) Loans Product**

| | Product | Interest | Proc. Fee |
|---|---|---|---|
| 9 | Jikomboe | 4% flat | 5% |
| 10 | Jitume | 5% flat | 5% |
| 11 | Mkombozi | 5% flat | 5% |

**Partnership Products**

| | Product | Interest | VAT Inclusive Processing Fees |
|---|---|---|---|
| 12 | Partnership | Negotiable | Negotiable |

**Banking Services**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Balance Enquiry | n/a | Free |
| 2 | Dormancy Fees | n/a | 5000 pm |
| 3 | Payments | n/a | Free |
| 4 | Withdrawal | n/a | 300 |

**Mobile Banking**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | Balance Enquiry | n/a | Free |
| 5 | Payments | n/a | Free |
| 6 | Withdrawal | n/a | Free |

**Saving Products**

| | Product | Interest P.A | VAT Inclusive Processing Fees |
|---|---|---|---|
| 1 | Savings Group Accounts | 4% | n/a |
| 2 | Joint Accounts | 4% | n/a |
| 3 | Akiba Accounts | 4% | n/a |
| 4 | Watoto Accounts | 4% | n/a |
| 5 | Bussiness Accounts | 4% | n/a |
| 6 | Fixed Deposit Accounts | Tied to the Amount | n/a |
| 7 | Conditional Savings | Tied to the Amount | n/a |

| Name and Title | Signature | Date |
|---|---|---|
| Yohane Ibrahim Kaduma ( Ofisa Mtendaji Mkuu) | Signed | 28 Januari 2020 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha ) | Signed | 28 Januari 2020 |
| Emmanuel Shee (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | Signed | 28 Januari 2020 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwaka 2020 uhimize kampeni ya lishe bora

**UPUNGUFU** wa vitamini A na ukosefu wa lishe bora miongoni mwa watoto unatishia afya na uhai wa watoto wa chini ya miaka mitano na hata kinamama wajawazito.

Ukosefu wa vitamin hizo na lishe bora husababisha watoto na kinamama kudhoofika kutokana na upungufu wa kinga ya mwili na kuongeza hatari ya kupata magonjwa hasa malaria, upungufu wa damu, kuhara, kutapika na magonjwa ya ngozi.

Mikakati mbalimbali ya kukabiliana na upungufu wa vitamini A imebuniwa na hata ile ya kuongeza ubora wa chakula kwa kukiongezea virutubisho yakiwamo madini zinafanyika.

Hata hivyo, si watu wengi wenye taarifa za kutumia vyakula vyenye lishe bora na vilivyoongezewa virutubisho ili kuhakikisha kuwa watoto hasa wenye umri wa chini ya miaka mitano wanakuwa na afya njema, licha ya kwamba kwa vitamin A wengi wanawapeleka watoto wao kliniki.

Licha ya Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), kueleza mikakati mingi ya kutumia vyakula vilivyoongezwa virutubisho ni ukweli kuwa shule nyingi za sekondari na msingi hazitumii unga wenye virutubisho hasa sembe na dona.

Tunaona kuwa pamoja na kutoa vitamin A, ni vyema pia TFNC ikashirikiana na shule pamoja na wafanyabiashara wanaosaga unga wa sembe na dona vijijini na mijini ili kuwahimiza kuongeza virutubisho na kuhakikisha kuwa wanaziuzia shule ili kuandaa vyakula hivyo vilivyoongezewa nguvu ili vitumike kuwapikia watoto uji na ugali. Tunapongeza baadhi ya waandaaji ambao husaga unga ambao umeongezewa virutubisho lakini wakati mwingine taarifa zake hazijaandikwa kwa uwazi hivyo kutowafikia wananchi kwa wepesi.

Taarifa zake zimeandikwa kwa Kiingereza kama 'fortified mill' lugha ambayo si rahisi watu wasiofahamu Kizungu kaisoma. Kwa hiyo tunashauri kuwaelemisha wateja kwa kuwaandikia kwa lugha ya Kiswahili ambayo wanaielewa na pia kuwahamasisha kutumia unga huo. Ni vyema kuwashirikisha wanaosaga nafaka mijini na vijijini kwa kuwapatia virutubisho vilivyoandaliwa ili kuvifikisha kwenye viwanda au mashine zao na kuvichanganya na unga ili wananchi wanapopeleka nafaka kwa ajili ya kusaga unga uwe wa mahindi, mtama au ulezi wawaongezee.

Tatizo la utapiamlo na udumavu halitakwisha kama hakutakuwa na mkakati kabambe wa kuandaa lishe bora yenye virutubisho muhimu kwa ajili ya watoto wanaoanza kutumia chakula lakini bila kuwasahau mama wajawazito.


Licha ya jitihada za TFNC kufikiria uwezekano wa kutengeneza mafuta yaliyoongezewa virutubisho ikumbukwe kuwa mafuta ni bidhaa ambayo ni muhimu lakini si wote wanaoitumia.

Tunashauri kuwa pamoja na kutoa vitamin A, kuhimiza ulaji wa vyakula vyenye virutubisho ni vyema pia kuwaandaa watoto katika ngazi za chini hasa vijijini ili waweze kufahamu namna ya kuandaa chakula bora katika mazingira wanayoishi na kuzifundisha familia zao.

Tunaishauri TFNC kushirikiana na wataalamu wa lishe wilayani kuziwezesha shule kufundisha wanafunzi shuleni kuandaa vyakula bora vyenye lishe bora kwa ajili ya familia za vijijini ili kuzihamasisha jamii kuhusu uzalishaji, uhifadhi na ulaji wa vyakula vyenye vitamin A kwa wingi na vyenye lishe bora vinavopatikana maeneo hayo.

Ikumbukwe kuwa watu wengi wanaamini katika kula chakula lakini hawajahamasika kula vyakula bora vyenye mchanganyiko wa vitu vyote kama wanga, mboga, matunda, protini na mafuta ili kupata lishe bora. Ili kuwa na kizazi chenye afya ni vyema kutumia chakula cha wanga hasa ugali au mchele na protini kama nyama, maharage na jamii nyingine za kunde pamoja na mboga za majani na matunda ili kupata virutubisho vyote muhimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Asasi zisaidie kuwaonyesha vijana uchumi ulioko kijijini

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya tatizo kubwa hivi sasa kwa vijana nchini, ni ukosefu wa ajira, inaosababisha baadhi yao kushinda vijiweni au kuzunguka katika ofisi kusaka ajira ya kukimu maisha yao.

Pamoja na kuwapo tatizo la ukosefu wa ajira, bado wanaweza kutumia mlango mwingine kujiajiri katika biashara, hata wakayaona mafanikiwa kimaisha, badala ya kutegemea kuajiriwa tu.

Kuna fursa zilozopo mikononi mwao, watazitambua na kuziendea katika ufahamu wa jinsi ya kuzitumia, kuliko kusubiri kuajiriwa, ihali nafasi inajulikana kuwa finyu sana. Pia, tukubali, wote wenye vigezo vya kuajiriwa. Ni bahati mbaya, wote wamedumbukizwa katika kapu moja la kutafuta ajira na kujikuta wanakwama. Wapo wanaofikia hatua ya kukata tamaa, wakidhani hakuna njia nyingine iliyobaki ya kuendesha maisha.

Inawezekana, ni mtazamo unaotokana na baadhi yao kutopewa elimu ya kutambua fursa zilizopo za kuwawezesha kiuchumi. Hivyo, nionavyo kuna haja ya wadau mbalimbali nchini, zikiwamo asasi za kiraia ziwaonyeshea vijana fursa hizo wasizoziona . Matokeo ya Utafiti wa Afya za Watu ya Mwaka 2015, yanaonyesha mmoja kati ya Watanzania wanne, ni kijana wa umri wa chini ya miaka 19, ambao kimsingi wana uwezo kuchangia maendeleo ya taifa lao.

Uwezekano wa kupata maendeleo, unategemea ni kwa kiasi gani vijana wametayarishwa, kuendelezwa kushiriki katika ujenzi wa taifa, hivyo watazamwe kwa jicho la ziada.

Kimsingi, ni kundi lenye changamoto nyingi, zikiwamo hata za kiafya. Hapo nitalitaja janga kuu, maradhi ya ikimwi ambayo matokeo yake ni kukatisha masomo na hatua zingine za maendeleo kwa vijana.

Vijana wasipoondolewa changamoto hizo, hata uwezo kuchangia maendeleo ya taifa unakuwa ni mdogo. Hivyo, wasaidiwe kuonyeshwa fursa za maendeleo na waepushwe na matatizo mengine ya kiafya.

Asasi za kiraia nazo zina nafasi kubwa katika jambo hilo, kwa ajili ya kuwasaidia vijana kuwapa elimu ya kutumia fursa zilizopo kuinuka kiuchumi, ili dhana 'Vijana ni Taifa la Kesho' iwe na maana nzuri.

Asasi ya Foundation for Civil Society (FCS), imetoa Sh. bilioni 11 kwa asasui za kiraia au azaki 154, ili zitekeleze miradi inayolenga kuboresha maisha ya Watanzania katika ngazi ya taifa hadi chini, pia kutekeleza miradi ya utawala bora.

Asasi hizo zinajikita katika ujenzi wa amani na utatuzi wa migogoro, uboreshaji maisha na kukuza uchumi. Hivyo, ni wajibu wa asasi hizo ambazo hadi sasa zinaendelea na miradi hiyo kutambua kundi hilo.

Vijana wanatakiwa kupata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara, ili waweze kutambua fursa zilizopo na kuziendeza, kuliko kubaki wakilalamika tu kwamba hakuna ajira kumbe kuna mlango mwingine wa kutokea. Kimazingira, Tanzania ni nchi iliyotambuliwa kuwa na fursa nyingi ambazo vijana wakizitumia, zitawanufaisha na waondokane na mihangiko ya kusaka ajira, badala ya kujiajiri kwa kuanzisha biashara ndogo mbalimbali.

Miongoni mwake ni kilimo cha mazao mbalimbali ya biashara, yakiwamo alizeti, mpunga, mahindi, karanga, choroko, kunde, pamba na mengine mengi yanayolimwa nchini.

Baadhi yao, wanajamii wanakwepa kilimo wakiwa na sababu mbalimbali, wakitaja zana zinazotumika zimepitwa na wakati, pia mtindo wa kutegemea mvua badala ya kilimo cha umwagiliaji, vyote vikifanya kilimo kuwa kigumu. Kilimo cha kutumia trekta au teknolojia nyingine ya kisasa ikiambatana na umwagiliaji, kinaweza kutatua tatizo la ajira kwa vijana, iwapo kitapanuliwa na vijana wenyewe wakiwa tayari kurudi shambani.

Hakuna haja ya vijana kulundikana mijini, wakati vijijini kunapokuwapo fursa, kwani ambao wamezitambua wanaendelea nazo, ikiwamo kuendesha bodaboda badala ya kilimo, sekta wanayoikimbia.

Asasi zisaidie vijana kuondokana na fikra mbovu za duni kwamba maisha mazuri yako mjini pekee. Watambue hata vijijini, wanaweza kufanikiwa, hivyo waelekezwe cha kufanya, ili wafanikiwe.

Vijana wanapaswa kutambua kuwa fursa za mafanikio, haziko mijini tu, bali hata vijijini, hivyo waelimishwe wasikimbilie mijini na kujikuta wakiishia kufanya biashara ndogo zisizo na matumaini kwa maisha yao ya baadaye.

# Polisi yawahoji viongozi ACT-Wazalendo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, limesema limeshawahoji viongozi wawili wa Chama cha ACT -Wazalendo, baada ya kudaiwa kutoa lugha zinazoashiria uchochezi miongoni mwa wananchi.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Ahmed Khamis Makarani, alisema lengo la kuwahoji ni kuhusiana na vitendo vyao vya uchochezi walivyodaiwa kuvifanya kwa nyakati tofauti.

Alisema viongozi hao kupitia televisheni za mitandaoni, walitoa lugha zenye kuashiria uchochezi, na ndio maana walilazimika kupata maelezo yao ya kina.

Alisema, Jeshi la Polisi kama walinzi wa amani halikuridhika na kauli hizo, ndio maana wamewahoji na kupima, iwapo kuna kesi ya msingi, ambayo wanaweza kuifikisha mbele ya vyombo vya sheria kujibu.

"Ni kweli viongozi wawili wa ACT-Wazalendo, Omar Ali Shehe na Saleh Nassor Juma tumewaita hapa makao makuu ya Jeshi la Polisi na tumeshwahoji, kwa tuhuma za kutoa lugha zenye kuashiria uchochezi," alifafanua.

Katika hatua nyingine, alieleza iwapo viongozi hao hawataonekana na kosa, mahojiano hayo yatatosheleza kwao.

Alisema Jeshi la Polisi, linaendelea na upelelezi wa kina wa tukio hilo na kama kuna kesi ya kujibu, jalada lao litapelekewa kwa mwanasheria.

Katibu wa mipango, wanachama na mafunzo wa chama hicho, Omar Ali Shehe, alikiri kuhojiwa na Jeshi la Polisi.

Alisema, walipokea taarifa ya wito kutoka Jeshi la Polisi, yeye na kiongozi mwenzake, maalim Saleh Nassor Juma na walihojiwa kwa tuhuma za kutoa lugha zenye kuashiria uchochezi kwa wananchi.

Alisema, kabla ya kuitwa na Jeshi hilo, Januari 10 mwaka huu majira ya mchana, baada ya wananchi wa kijiji cha Kwale wilaya ya Chake Chake, kukusanyika juu ya hatma ya kupatiwa vitambulisho na aliwaita ili kuzungumza nao.

"Kwa shehia ile ya Kwale, siku hiyo ilikua ni ya mwisho ya kutolewa vitambulisho vya ukaazi na wananchi 1,200 walikuwa hawajapatiwa, hivyo nilikwenda kuzungumza nao, ndio sababu ya kuitwa Polisi,' 'alifafanua.

Alisema kauli iliowashitua Jeshi la Polisi wakati anazungumza na wananchi hao, ni ile kuwa wataendelea kuwasimamia wananchi na wanachama wote, hadi watakapopatiwa vitambulisho vyao.

Kiongozi huyo alisema jambo lingine alilowaahidi wananchi hao na wanachama wao ambalo lilisababisha kuhojiwa na Jeshi la Polisi, ni kuwahakikisha iwapo hawatopatiwa vitambulisho, daftari la kudumu la wapiga kura wataomba lisimamishwe kwanza.




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, wakiwa amesimamisha mabasi ya daladala na kuhoji madereva wake katikati ya barabara, eneo la Sinza Mapambano, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, bila ya kujali foleni kubwa ya magari. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rugemalira 'alipua bomu' mahakamani

**INATOKA UK. 2**

Aidha, Makandege anadaiwa kuwa kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 19, 2014 katika maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam, Kenya, Afrika Kusini na India, akiwa na wenzake, walikula njama ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Pia anadaiwa kuongoza genge la uhalifu katika nchi hizo, akiwa si mtumishi wa serikali akishirikiana na watumishi wa umma kwa kuratibu na kufadhili mpango wa uhalifu.

Katika shtaka la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, Makandege anadaiwa kuwa kati ya Januari 23, 2014 na Februari, 2014 alijipatia dola 380,000 katika benki ya Stanbic iliyopo Kinondoni na dola 600,000 katika benki ya UBL Bank (T) Ltd iliyoko wilaya ya Ilala, zilizotoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa nyakati tofauti.

Kwa upande wa Sethi na Rugemalira, walifikishwa mahakamani hapo zaidi ya miaka miwili na wamekaa rumande, kutokana na upelelezi wa kesi yao kutokukamilika.

Washitakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashitaka 12 yakiwamo ya utakatishaji fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh 309,461,300,158.27, kwa mara ya kwanza walifikishwa mahakamani hapo Juni 19, 2017.

Washitakiwa hao wanadaiwa kuwa Oktoba 18, 2011 na Machi 19 , 2014 jijini Dar es Salaam walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ili kutenda kosa.

Aidha, inadaiwa katika mashitaka ya kujipatia fedha kwamba kati ya Novemba 28 na 29, 2011 na Januari 23,2014 katika Makao makuu ya Benki ya Stanbic Kinondoni na Benki ya Mkombozi tawi la Mtakatifu Joseph, kwa ulaghai washitakiwa hao walijipatia kutoka BOT Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh 309, 461,300,158.27.

Pia washitakiwa wote wanadaiwa kuisababishia serikali hasara ambapo inadaiwa walitenda makosa hayo Novemba 29, 2013 katika Benki ya Stanbic tawi la kati kinondoni, kwa vitendo vyao walisababishia serikali hasara ya Dola 22, 198, 544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Kati ya Novemba 29,2013 na Januari 23, 2014 maeneo tofauti Dar es Salaam kwa pamoja wanadaiwa kutenda kosa la kutakatisha fedha kwa kuchukua fedha kutoka BoT ambazo ni dola za Marekani milioni 22.1 na Sh bilioni 309.4 wakati wakijua fedha hizo ni zao la kujihusisha na genge la uhalifu.

# Corona yazuia wanafunzi kurejea masomoni China

**INATOKA UK. 3**

anafanya kazi ya kutoa mrejesho wa kila siku wa hali ilivyo nchini humo.

Majaliwa alisema Balozi Kairuki anafanya kazi nzuri ya kutoa elimu kwa Watanzania, ikiwamo kutafuta madaktari wa Kitanzania ambao wamejifunza ugonjwa huo na wanaendeea kuwaelimisha Watanzania waliopo China namna ya kujikinga.

"Na Balozi kule (Kairuki) amewakanya Watanzania wasiwe na mizunguko mingi sana, kwa sababu ugonjwa huo maambukizi yake ni pale ambako watu wanakutana," alisema Majaliwa na kuongeza:

"Tumewataka Watanzania wale wanapohitaji labda kurudi Tanzania, na kwa sababu watatakiwa kusafiri kwenye treni, mabasi, wawasiliane na balozi namna nzuri ya kusafiri, wasisafiri kwenda ubalozini, Beijing ilipo watumie mawasiliano ya kimtandao kupata ridhaa hiyo na kuambiwa hali ikoje na wapate vibali vya kurudi.

MTEGO UCHAGUZI MITAA

Wakati huohuo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema kuwa uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika mwaka jana hautarudiwa na kwamba hakuna sababu ya kutengua uchaguzi wote.

Amesema endapo kuna mgombea mwenye malalamiko anayo fursa ya kwenda mahakamani.

Waziri Mkuu Majaliwa alitoa ufafanuzi huo baada ya kuulizwa swali na Mbunge wa Mbozi (Chadema), Paschal Haonga.

"Kulichukua hili kwa ujumla ujumla, si sahihi sana kwa sababu kila mmoja alipo alikuwa na mamlaka yake inayoratibu na anayo fursa ya kwenda kwenye mamlaka ya kukatia rufaa pale ambapo hajaridhika na utekelezaji wa jambo hilo," alisema Majaliwa na kuongeza

"Na vyama vyote vilishiriki kwenye hili katika kanuni ya kukata rufaa, kwa hiyo ni wajibu wa huyo mgombea kwenye eneo hilo kwenda kukata rufaa, na kama kulikuwa na dosari kama ambavyo nimeeleza, bado zilikuwa zinaweza kuelezwa huko huko kwenye ngazi hiyo" alisema Majaliwa.

Alisema moja kati ya kanuni inayotoa fursa kwa yeyote ambaye hajaridhika ana haki ya kukata rufaa eneo aligombea na endapo hajaridhika aende mahakamani.

Aidha, Waziri Mkuu Majaliwa alitetea uamuzi wake wa kuzuia utoaji wa vibali vya kuingiza sukari kutoka nje hadi sukari inayozalishwa na Kiwanda cha Sukari cha Mahonda-Zanzibar iishe.

Majaliwa alisema anaamini, Watanzania walimuelewa na hasa Wazanzibar na kwamba alichokisema ni sahihi na hao wanaotamka kuwa amewachefua Wazanzibar, ni wanunuzi na sio Wazanzibar.

## HABARI KITAIFA

# Kamati maafa mikoa 8 zatakiwa kuweka mradi bomba mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa, imezishauri kamati za usimamizi wa maafa katika mikoa 8 na vijiji 184 katika wilaya 24 zilizopo katika mikoa ya hiyo ambapo mradi wa bomba la mafuta utatekelezwa, kuuweka mradi huo katika mipango yao ya kujiandaa na kukabiliana na maafa.

Mikoa hiyo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, huku lengo likiwa ni kuhakikisha mradi huo hauthiriwi na majanga yanayoweza kutokea.

Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 7 ya mwaka 2015, inaainisha majukumu ya kamati za usimamizi wa maafa kuanzia ngazi ya kijiji hadi mkoa, ambapo kwa mujibu wa sheria hiyo, jukumu la msingi ni kutoa taarifa za tahadhari ndani ya eneo husika, kuratibu na kusimamia shughuli za usimamizi wa maafa na operesheni za dharura ndani ya kijiji wilaya au mkoa pamoja na kutafuta rasilimali kwa ajili ya usimamizi wa maafa ngazi husika.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo la kwenye rasi ya Chongoleani karibu na Bandari ya Tanga ambapo mradi huo utatekelezwa, Mkurugenzi Idara ya Menejimenti ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kanali Jimmy Matamwe, alifafanua kuwa kamati za maafa zinalo jukumu la kuchukua tahadhari ya namna ya kuhakikisha majanga yanayoweza kuuathiri mradi huo yanakuwa katika mipango yao ya menejimenti ya maafa ili faida zitakazotokana na utekelezaji wa mradi huo zinakuwa endelevu.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Noel Kazimoto, alieleza kuwa utekelezaji wa mradi huo utafungua fursa za kiuchumi kwa Watanzania, hivyo ni dhahiri kuwa eneo la Chongoleani litakuwa na mwingiliano mkubwa wa watu na shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zitakuwa zikiendeshwa, kwa kuwa wananchi ni wadau wa menejimeti ya maafa kupitia kamati za menejimenti za maafa kuanzia ngazi ya vijiji.

Kazimoto alisema wataendelea kuelimishwa juu ya majanga yanayoweza kuuathiri mradi huo ili kuhakikisha unakuwa endelevu. Mradi wa bomba la mafuta ghafi unatekelezwa kwa ubia wa ujenzi na uendeshaji kwa kushirikisha kampuni za Total ya Ufaransa, CNOOC ya China, Tullow ya Uingereza na Serikali za Tanzania na Uganda. Mafuta ghafi yatasafirishwa kutoka Kabaale katika Wilaya ya Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga nchini Tanzania. Mradi wa bomba hilo una umbali wa kilometa 1,445, ambapo kilometa 298 zitakuwa nchini Uganda, na kilometa 1,147 zitakuwa Tanzania.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Unilever Tanzania, David Minja (wa nne kushoto), akikata utepe kuzindua kampeni ya kitaifa ya usafi wa familia iliyopewa jina la Omo Ng'arisha familia katika Uwanja wa Mbagala Zakhem, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

# Sumu kuvu kwenye karanga, mahindi chanzo cha saratani

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imesema mojawapo ya madhara anayoweza kupata mtu aliyekula mahindi na karanga zilizochanganyika na sumu kuvu ni kuugua saratani ya Ini.

Kadhalika, imesema endapo watoto wakila nafaka hizo nao wako katika hatari ya kupata ugonjwa wa udumavu.

Mratibu wa mradi wa kudhibiti sumu kuvu (TANIPAC) unaorabitiwa na serikali, Clepin Josephat, aliyasema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusiana na mikakati waliojiwekea dhidi ya kupambana na Sumukuvu.

Josephat alisema sumukuvu ni hatari katika mwili wa binadamu na hii inasababishwa na wakulima kutofuata taratibu na kanuni za Kilimo katika maeneo au mikoa ambayo imeathiriwa.

"Kuna uhusiano wa saratani ya Ini na chakula kilichoathiriwa na sumukuvu ndiyo maana unaona serikali iko mstari wa mbele kuhakikisha inamaliza tatizo hilo nchini," alisema Josephat.

Alisema kwa sasa kuna uhusiano kati ya ugonjwa wa saratani na uwapo wa sumukuvu katika mazao hususani mahindi na karanga.

Alisema pia kuna udumavu kwa watoto, na kwamba mtoto akiathirika siyo rahisi kumrejesha katika ukuaji wake wa kawaida.

"Ninaomba wakulima, wasindikaji tuwe na taratibu za kufuata kanuni itasaidia kupunguza tatizo la sumu kuvu. Tunakwenda kuboresha miundombinu bara na visiwani ikiwamo kutoa elimu lengo ni kutokomeza kabisa ugonjwa huu," alisema Josephat.

Alisema mkataba wa miaka mitano ambao serikali imesaini utakwenda kutatua changamoto katika mikoa ambayo imeathiriwa na sumu kuvu.

Alisema katika uboreshaji wamepanga kujenga maabara kubwa ya kimataifa yenye uwezo wa kupima mazao kabla ya kwenda nchi za nje.

Alisema mbali na ujenzi wa maabara, pia wanatarajia kujenga maghala makubwa bara na visiwani ambayo yatakuwa mfano wa kufundisha wakulima, wasindikaji namna ya kuhifadhi mazao yasiathiriwe na sumu kuvu.

Alisema wanatarajia pia kuhamasisha matumizi ya vihenge vya kisasa, na kwamba vihenge hivyo vitakuwa msaada mkubwa kwa wakulima.

# Kampeni ya usafi sasa yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya bidhaa mbalimbali ya Unilever Tanzania imezindua kampeni maalumu ya ya usafi wa miezi sita iitwayo 'Omo Ng'arisha Festival' itakayofanyika Tanzania nzima ikiwa na lengo la kuhamasisha faida, ubora na matumizi sahihi ya sabuni bora ya Omo..

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Mbagala jiji la Dar es Salaam jana, Meneja Masoko wa bidhaa ya Omo, Upendo Mkusa, alisema ni matumaini yao kwa kupitia kampeni hiyo jamii itatambua matumizi sahihi ili kupata matokeo yanayotarajiwa.

Akizungumza zaidi kuhusu kampeni hiyo, Upendo alisema baada ya uzinduzi huo, kampeni hiyo itaendelea kwa matamasha na matukio mengine katika mikoa ya Dodoma, Dar, Mwanza, Arusha, Moshi na Mbeya.

Alisema ili kuifanya kampeni hiyo kuwa yenye bashasha na mvuto, Unilever imemtangaza Msanii maarufu nchini, Isha Mashauzi, kuwa Balozi wa Kampeni ya Omo Ng'arisha, atakayeshiriki katika matukio mbalimbali katika kampeni hii ikiwamo michezo, michezo ya kufurahisha na burudani ya muziki kutoka kwa wasanii mbalimbali.

Kampeni itashirikisha timu ya promosheni ya Omo kwa kupita mlango kwa mlango majumbani, kwenye maeneo ya wazi na katika sehemu za biashara kuijulisha jamii juu ya ubora, faida na matumizi sahihi ya OMO, ambayo ni moja ya bidhaa kubwa zaidi ya Unilever.

Alisema kwa kutambua na kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano katika kuendeleza uchumi wa viwanda na katika kuwaletea watu wake maendeleo, wameandaa utaratibu maalumu la kuwatambua Wanawake wajasiriamali 10 Bora katika kila mkoa watakapofanya kampeni hiyo na kuwapa zawadi itakayowasaidia kuboresha biashara zao hivyo kuwafanya kung'aa.

"Ni imani yetu wanawake hawa miongoni mwao kuna wenye biashara ndogondogo, tutawatambua na kuwapa zawadi. Ni matarajio yetu utambuzi huu utaleta tija na kuwa kichocheo katika utendaji wao hivyo kukuza biashara zao.

"Unilever pia tupo mstari wa mbele katika kusaidia jamii, ni katika muskabali huo timu yetu ya kampeni katika mikoa hiyo..., tutatembelea katika mahospitali ambako tutaonyesha moyo wa kujali kwa kutoa msaada wa sabuni kwa wagonjwa waliolazwa katika hospitali hizo tukiongozwa

# Serikali yatoa msimamo hati ukaguzi wa hesabu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa serikali haina mpango wa kufuta Hati inayoridhisha yenye maoni ya kikaguzi wala kuingilia namna taaluma ya ukaguzi nchini inavyoendeshwa.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Bunda (CCM), Boniphace Getere.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema katika miaka ya hivi karibuni nchini kumekuwa na majina mengi katika Idara ya Ukaguzi toka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama vile Hati safi, Hati inayoridhisha na Hati chafu.

"Je, Shirika au Halmashauri kupata hati safi ni ishara kwamba Shirika au Halmashauri husika halina ubadhirifu wa mali ya umma kwa kuwa kuna kila dalili kuwa kutolewa kwa hati safi ni dalili ya wazi ya kuficha ubadhirifu katika baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma?" alihoji.

Pia alihoji lini Serikali itafuta utaratibu huo ambao umekuwa kinga ya ubadhirifu wa mali ya umma.

Akijibu swali hilo, Dk. Kijaji alifafanua kuwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kaguzi mbalimbali ambazo ni Ukaguzi wa Hesabu, Ukaguzi wa Kiuchunguzi, Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji.

"Lengo kuu la ukaguzi wa Hesabu ni kutoa maoni kama Hesabu zinazokaguliwa zinaonesha hali halisi ya mapato na matumizi ya serikali kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha," alisema.

Alieleza kuwa maoni hayo hutolewa kwa njia ya hati za ukaguzi ambazo zimegawanyika katika makundi manne ambayo ni Hati inayoridhisha, Hati yenye Shaka, Hati Isiyoridhisha na Hati Mbaya.

"Hati inayoridhisha hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa na kukaguliwa zinapokuwa zimezingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Sekta ya Umma, na Sheria na Kanuni za Fedha za Umma. Hati hii huonesha taarifa za fedha zinatoa taswira ya kweli na hali halisi ya mapato, matumizi, mali na madeni ya taasisi husika," alisema.

Hata hivyo alisema dhana ya kuwa 'hati Inayoridhisha' inatoa tafsiri ya kutokuwapo kwa kila aina ya ubadhirifu siyo sahihi kwa sababu mbalimbali.

"Sababu hizo ni pamoja na maoni ya ukaguzi yanatolewa kwa malengo maalum ya kuwafahamisha watumiaji wa taarifa za fedha kama taarifa hizo zinaonesha ukweli na hali halisi ya hesabu za mizania kwa tarehe husika, taarifa za mapato na matumizi pamoja na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa kipindi kilichokaguliwa," alisema.

Nyingine ni dhana ya ukaguzi wa hesabu inajikita katika masuala ambayo wakaguzi wanaamini kuwa ni mazito na yana athari kubwa kwenye taarifa za fedha za taasisi husika.

"Hii ina maana kuwa, mambo ambayo hayana athari kwenye taarifa za fedha yanashughulikwa na mifumo ya udhibiti wa ndani ya taasisi husika.Kwa majibu haya napenda kuliarifu Bunge lako kuwa utaratibu huu ndiyo unaotumika dunia nzima, hivyo Serikali haina mpango wa kufuta Hati inayoridhisha yenye maoni ya kikaguzi wala kuingilia namna taaluma ya ukaguzi nchini inavyoendeshwa," alisema.

Alisema kutoa utaratibu mwingine itakuwa ni kukiuka Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Tarifa za Fedha (IPSAS) katika Sekta ya Umma na pia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISSAI) ambavyo Serikali imeviridhia vitumike.

# Agizo barabara zilizoharibiwa na mvua kutengewa fedha

SERIKALI imeagiza Wakala wa Barabara nchini (Tanroads), kutenga bajeti kwa mwaka 2020/21 ya kukarabati miundombinu ya barabara kwenye mikoa ambayo imekuwa ikipata uharibifu mkubwa kutokana na mvua ukiwamo mkoa wa Tanga.

Kauli ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Korogwe Mjini (CCM), Mary Chatanda.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA



Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema mji wa Korogwe upo bondeni na mvua zinazoendelea kunyesha zimeendelea kuathiri miundombinu kwenye mji huo.

"Je, serikali itakuwa tayari kutenga fedha za kujenga mifereji wakati tukisubiri fedha kwa ajili ya kujenga barabara ya lami, na tupatiwe fedha kidogo kidogo kuliko kutenga kila mwaka fedha za ukarabati barabara za changarawe ambazo zinaharibiwa na mvua?"alihoji.

Kwandikwa alisema maji yasipodhibitiwa ni adui mkubwa wa barabara na kuna maelekezo yametolewa ili mamlaka zote muhimu kushirikiana kwa na mipango ya kudhibiti maji ya mvua.

"Kati ya mikoa ambayo imeshambuliwa sana na mvua ni Tanga na tumetoa maelekezo Tanroads kwa mikoa yenye uharibifu mkubwa kutengewa bajeti, tutaweka kipaumbele kwenye maeneo yaliyo na shida,"alisema

Katika swali la msingi, Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashidi Shangazi, alihoji ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Lushoto-Mlalo yenye urefu wa kilometa 45 kwa kiwango cha lami.

Kwandikwa, alisema serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo, ilianza kuijenga kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

"Hadi kufikia mwaka wa fedha 2018/19, jumla ya kilometa 8.6 zimekamilika kwa gharama ya Sh.Bilioni 5.2. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imeendelea kuitengea fedha barabara hii kwa ajili ya kuendelea na ujenzi," alisema

Alisema sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilometa 33 itaendelea kujengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

# Dampo la kisasa kujengwa Dar

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu (pichani), amesema hali ya uchafu mazingira katika jiji la Dar es Salaam ni kubwa kutokana na uwapo wa dampo moja.



Kufuatia hali hiyo, Zungu amesema kuna mpango mkubwa wa kujenga dampo la kisasa litakalokuwa na uwezo wa kubeba taka zote za jiji hilo.

Waziri Zungu alitoa kauli hiyo bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kawe (Chadema), Halima Mdee, ambaye alisema Dar es Salaam kuna wakazi milioni tano na kuna dampo moja katika eneo la Pugu Kinyamwezi na lipo kwenye hali mbaya.

Alihoji serikali ina mpango gani kujenga dampo la kisasa kwenye maeneo mengine kila wilaya ili kuzuia uchafu kutokana na lililopo kutokidhi kubeba uchafu katika jiji zima.

Zungu alisema kuwa kasi ya taka katika Jiji la Dar es Salaam ni kubwa licha ya kuwa linakua kwa kasi na kwamba miaka ijayo linakadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni nane hadi tisa na dampo ni moja.

Alikiri hali ni ya uchafu ni mbaya kwenye jiji hilo.

"Lakini nimwondoe hofu mbunge kuwa fedha zipo zimeshatolewa ili kujengwa la kisasa jipya ambalo litabeba taka zote katika jiji la Dar es Salaam," alisisitiza.

Awali, katika swali la msingi, Mdee alisema Jiji la Dar es Salaam limekabiliwa na tatizo sugu la uchimbaji mchanga na uchafuzi uliokithiri.

"Serikali ina mikakati gani ya muda mfupi na mrefu kukabiliana na kero hii sugu na hatarishi?"alihoji

Akijibu, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Mussa Sima, alisema ni kweli kuna tatizo kubwa ya uchimbaji wa mchanga Dar es Salaam.

"Yapo machimbo ya mchanga yaliyoruhusiwa kisheria na kupata vibali kutoka Mamlaka husika kama Serikali za Mitaa (Halmashauri za Jiji na Manispaa), Ofisi za Mamlaka za Mabonde na Wizara ya Madini," alisema.

Hata hivyo,alisema upo uchimbaji holela hususan katika maeneo ya mito na machimbo mengine ya mchanga ambayo sio rasmi yanayoanzishwa na wananchi katika maeneo mbalimbali.

Alieleza kuwa ili kukabiliana na hili hatua zinachukuliwa ni kuelimisha wananchi kuhusu athari za uchimbaji holela wa mchanga na kuzuia uchimbaji holela.

"Mamlaka mbalimbali zikiwamo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Mamlaka za Mabonde na Tume ya Madini kupitia Ofisi ya Madini Mkoa wa Dar es Salaam, zimekuwa zikifanya ukaguzi wa mara kwa mara na hatua stahiki kwa mujibu wa sheria huchukuliwa," alisema.

Aidha, alisema Serikali inaandaa mkakati wa muda mrefu utakaotokana na mapendekeo ya Kamati Maalum ya wadau iliyoundwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuwa na uchimbaji endelevu wa mchanga na usiokiuka Sheria za nchi na Kufanya tafiti na kuendeleza teknolojia za ujenzi zinazoweza kutumia mchanga kidogo.

# DC Muro atoa wiki mbili utatuzi wa mgogoro ardhi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, ametoa wiki mbili kwa Halmashauri ya Arusha DC, kutatua mgogoro wa ardhi kati ya Kijiji cha Engutukoit na Lesinoni, uliodumu kwa muda mrefu bila kutafutiwa ufumbuzi.

Akizungumza wakati wa ziara ya kikazi katika Kijiji cha Engutukoit Kata ya Oldonyowas, Muro ameagiza uongozi wa halmashauri hiyo, viongozi wa vijiji na wataalamu wa ardhi, kuitisha mkutano wa hadhara kutafuta suluhisho la mgogoro huo.

"Ninatoa wiki mbili mtatue mgogoro huu, kwa kuwa wataalamu wa ardhi watawashauri nini cha kufanya ili kufikia maridhiano kwa pande hizi mbili," Muro alisema.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC ambaye ni Ofisa Mifugo na Uvuvi, Charles Ngiloriti, alisema wamepokea maelekezo hayo na watakwenda kushirikiana na viongozi wa serikali ya kijiji, idara ya ardhi na mwanasheria ili kuutatua.

"Tunaomba mtupe ushirikiano kutafuta ufumbuzi wa mgogoro huu, kwa maslahi ya wilaya yetu ya Arumeru," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Engutukoit, Loserian Paangu, aliomba maeneo ya mipaka ya kijiji hicho, yapimwe na kuwekewa alama ili kuepuka mgogoro na vijiji vinavyowazunguka.

"Nashukuru Shirika la OIKOS, kwa kutusaidia kupima baadhi ya maeneo, lakini tunaomba suala la mipaka lizingatiwe kwa umakini ili kuepuka migogoro,"alisema Paangu. Alisema wananchi wa kijiji hicho wanakabiliwa na ukosefu wa zahanati na kusababisha kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 12 kwenda kutafuta huduma za afya katika vijiji vya jirani.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shanna, akionyesha moja ya silaha bastola aina ya Chinese kwa waandishi iliyokuwa ikitumiwa na watu wanaodaiwa kuwa majambazi sugu watano waliouawa na jeshi hilo. Kushoto ni Mkuu wa mkoa huo, Mrisho Gambo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Unywaji pombe kupindukia watajwa kuongeza kasi ubakaji

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

OFISA Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Hanan'g, Martha Sulle, ametaja moja ya sababu ya ongezeko la matukio ya ubakaji dhidi ya watoto ni ulevi kupindukia na kuwataka wazazi kubeba jukumu la malezi.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusu ukatili huo dhidi ya watoto, Sulle alisema matukio hayo yameshika kasi ndani ya halmashauri hiyo.

"Chanzo kikuu cha ubakaji siku hizi ni ulevi ambao unachangia kuwadanganya watoto kwa kuwapa pipi au zawadi zingine kama biskuti,"alieleza.

Sulle alisema alitaja sababu nyingine ni kuongezeka kwa familia zinazotelekezwa na wanaume, jambo linalosababisha watoto kukosa ulinzi wa uhakika dhidi ya watu wenye nia ovu.

Mkazi wa Babati, Isaya Nickson, aliwashauri wazazi kuhakikisha ulinzi wa watoto wao kuwa ni jukumu lao ili kuwaepusha na watu wanaowatapeli kwa kuwanunulia pipi. Nickson alisema ni vizuri wazazi ambao wanabanwa na majukumu wawe na wasaidizi wa nyumbani wa uhakika watakaobeba jukumu la ulinzi na usalama wa watoto pindi wazazi wakiwa kwenye majukumu yao ya kila siku.

Mkazi wa Matufa, Jackline Samwel alisema katika kipindi cha miaka minne vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka.

"Mtoto unakuta anakwenda kucheza kutwa nzima, mzazi au mlezi hamfuatilii kuona anacheza na nani na na yupo katika mazingira gani," alisema.

Samwel aliwataka wazazi kama wanavyofuatilia mifugo yao wasiibiwe wabebe jukumu la watoto kwa kuhakikisha wakati wote wanakuwa kwenye ulinzi na usalama.

Kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa na Kituo cha Haki za Binadamu Tanzania (LHRC) mwaka 2017, ukatili wa kingono hasa kwa watoto ulikuwa ni asilimia 85 na ukatili wa kimwili ulikuwa ni asilimia 15.

# Wanawake wafundwa mgawanyo mali kijinsia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAWAKE wa Mkoa wa Arusha, wametakiwa kusimamia haki sawa katika ugawaji mali kwa watoto wao bila kubagua jinsia ili kuondokana na migogoro ya kifamilia.

Mwanasheria na mwanachama wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Fransisca Gasper, aliyasema hayo jana jijini humo, wakati akitoa mada kwa vikundi mbalimbali vya wanawake kuhusu kupunguza migogoro ya ardhi na namna ya kuitatua.

Alisema ni vema kila mwanamke akaanza na familia yake kusimamia haki za mgawanyo wa mali kwa watoto wao.

"Ni vema wanawake hasa wa jamii za wafugaji wakaachana na kukumbatia mila na desturi za ubaguzi kwao na watoto wao wa kike kwa kuanza kusimama kidete kutetea haki sawa kwa watoto wa kike," alisema.

Pia aliwataka wakati wakidai haki katika mgawanyo wa miradhi ni vema wakaishi katika ndoa zinazotambulika kisheria.

"Wanawake wengi wanaishi kienyeji na mwisho wa siku mwenzio akiondoka inakuwa shida kutambulika, japo sheria inatambua mkiwa kwa miaka miwili mfululizo ni mke halali lakini hakuna nyaraka zinazokutambua mpaka watu adhibitishe,"alisema.

Mwanasheria wa TAWLA, Silveia Mwanga, aliwaomba wanawake hao kuhakikisha wanaandika wosia wa mgawanyo wa mali zao ili kuondoa migogoro pindi wanapofariki dunia.

"Wosia huu uwe siri, ukiwa wa wazi utaweza kusababisha vurugu kwa mtoto au watoto, hakikisheni mali zinagawanywa kwa kufuata haki sawa kwa watoto wa jinsia zote,"alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima (Mviwata), Wilaya ya Arumeru, Rehema Salmu, alishukuru TAWLA kwa kuwapatia elimu hiyo ambayo itawasaidia kuondoa manyanyaso kwa wananke na watoto wa kike vijijini.

"Tunachangamoto sana vijijini hasa kule kwetu Meru, tunanyanyasika hatupewi ardhi kabisa ni wanaume tu ambao ndiyo wanamiliki ardhi kwa sasa tumejua haki zetu tutazipigania,"alisema.

# 'Kilimo umwagiliaji chakosa usimamizi'

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKULIMA wa mazao ya mboga na matunda katika skimu ya Umwagiliaji ya Lower Moshi wameilalamikia serikali kuwa licha ya kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji kwa fedha nyingi, lakini bado sekta hiyo inakabiliwa na changamoto ya usimamizi.

Hayo yalisemwa jana na baadhi ya wakulima wa mazao ya mboga na matunda katika skimu ya Umwagiliaji ya Lower Moshi, baada ya timu ya wataalamu kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Kilimanjaro kufanya ziara ya ukaguzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

Severini Msofe, alisema ni vyema kwa tume kushirikiana na serikali kuanzisha utaratibu maalumu wa kusimamia miundombinu ili kuleta tija kwenye sekta ya kilimo na kulinda ili isiharibiwe na baadhi ya watu wasio waaminifu.

"Tunaomba Bunge litunge sheria ambayo itawabana wenyeviti wa vijiji, vitongoji na wasimamizi kulinda na kutunza miundombinu katika skimu hizi, wapo baadhi ya watu wasio waaminifu huharibu miundombinu hiyo bila kujali gharama zinazotumika na serikali kutengeneza," alisema Hawa Shabani.

Aidha, mtaalamu kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Said, alisema Sheria ya Umwagiliaji Namba 5 ya Mwaka 2013, inamtaka kila mkulima kulinda miundombinu na kwa atakayekiuka hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtuhumiwa.

Skimu ya Lower Moshi ambayo ipo umbali wa kilomita 5 kutoka Moshi Mjini, ilijengwa mwaka 1984 kwa Sh. bilioni tatu kwa ufadhili wa Serikali ya Tanzania na Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

# Watakiwa ubora uchakataji mazao misitu

**Na Mary Mosha**, MOSHI

SERIKALI imeutaka Umoja wa wenye Viwanda vya Mazao ya Misitu Kanda ya Kaskazini (NOFIA), kuzingatia ubora wa uchakataji wa mazao hayo ili kushindana katika masoko ya nje.

Kauli hiyo imetolewa na Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, alipokuwa akifungua Mkutano wa 10 wa Wanaviwanda Wadogo na wa Kati wanaochakata mazao yatokanayo na misitu katika kanda ya kaskazini inayojumuisha mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Manyara.

Prof. Silayo alisema ni vyema wanachama hao wakazalisha kwa ubora ili wapate masoko nje ya nchi, na kwamba tayari serikali imeshafanya mawasilianao na Kenya na Zambia ambao wamekubali kutuma wataalamu wao kuja kutembelea mashamba hayo kwa lengo la kuingia makubaliano katika uwekezaji na kuweka mkataba wa biashara hiyo.

"Masoko ya mazao ya misitu nje ya nchi yanahitaji bidhaa bora za hali ya juu, niwaombe wadau wanaohusika na uchakataji wa mazaoa haya kuzingatia hilo, kwa siku za hivi karibuni tumeshuhudia biashara ya mazao haya nje ya nchi imeshuka kidogo kutokana na kutokukidhi viwango vya ubora," alisema Prof. Silayo.

Prof. Silayo aliwataka wadau hao kuhakikisha kila mmoja anatoa bidhaa zenye ubora na kuwekeza kwenye teknolojia mpya kukabiliana na ushindani kwenye soko.

"Tumekuwa na mawasiliano na wenzetu wa Idara ya Misitu ya Zambia ambao wamekubali kutuma wataalamu wao kuja kutembelea mashamba yetu, kuona mazao ambayo tunayo kukutana na wadau ili k kuona namna wanaweza kuingia makubaliano katika uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuweka mkataba wa biashara hiyo," alisema.

Alisema wafanyabiashara wa mazao ya misitu hapa nchini wamekuwa wakilanguliwa mazao yao na madadali kutoka nchini Kenya kwa kushindwa kuzalisha kwa ubora licha ya kwamba mazao ya hapa nchini yana ubora zaidi hali ambayo imekuwa ikichangia kushinda kwenda kuuza mazao hayo nje ya nchi.

"Bidhaa nyingi zinazotoka nje ya nchi ni bora lakini sio imara kama zinazozalishwa hapa kwetu", alisema Prof. Silayo.

Aliongeza kusema: "Tayari nimefanya mawasiliano na nchi Kenya na Zambia pamoja na wazalishaji wanachotakiwa ili kuja kuweka teknolojia bora ili wazalishe kwa ubora na viwango vinavyotakiwa na waweze kufanya biashara nje ya nchi."

Prof. Silayo aliongeza kuwa serikali imeshazungumza na benki ya NMB ili kuangalia uwezekano wa kuwakopesha wenye viwanda vya mazao ya misitu kwa lengo la kuwa na mitambo ya kisasa ya uchakataji wa mazao hayo na hatimae kuuza nje ya nchi.

Naye Mwenyekiti wa NOFIA, Frank Karonge, alisema wawekezaji wamekuwa wakishindwa kuwekeza kutokana na kupata mikataba ya muda mfupi, hali ambayo inachangia kushindwa kukopesheka kwenye taasisi za kifedha.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo, Emanuel Khambay na Zaina Hashimu, wameiomba serikali kuwapatia mikopo ili kuingia kwenye uwekezaji wa teknolojia za kisasa.



Mkuu wa Wilaya ya Siha, , Onesmo Buswelu, akiteta jambo na wanafunzi wa Shule ya Msingi Sanya Juu, juzi, kuhusu hali ya ukatili dhidi ya watoto. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wanafunzi waiangukia serikali uhaba mabweni

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANAFUNZI katika Shule ya Sekondari ya Mangisina iliyopo Kata ya Kibosho wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro wanakabiliwa na changamoto ya mabweni na kusababisha kutembea umbali mrefu wa kilometa 10 kuelekea shuleni.

Hali inayohatarisha usalama wao hasa nyakati za jioni na kuiomba serikali na wadau mbalimbali kuwasaidia kujenga hosteli ili kuepukana na adha hiyo.

Hayo yameelezwa jana na mmoja wanafunzi wa eneo hilo Mariamu Mlay katika hafla fupi ya kupokea msaada wa kompyuta tatu pamoja vifaa vya michezo iliyotolewa na Diwani wa Kata ya Kibosho Magharibi, Deo Mushi.

Alisema kuwa, wasichana katika shule hiyo wanasoma kwenye mazingira magumu kutokana na shule hiyo kutokuwa na hosteli hivyo kuwalazimu kutembea umbali mrefu.

"Wengi wetu wanatoka vijiji vya mbali hivyo hukabiliwa na changamoto ya kutokuwa na mazingira rafiki hasa kwa mtoto wa kike kutokana na ongezeko walevi na asilimia kubwa huishi na bibi na hawana ulinzi,|" alisema.

Naye, Mratibu Elimu Kata ya Kibosho Kati, Hans Ngowi, alisema kuwa shule hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa hosteli za wasichana na kwamba wameanza vikao na wazazi ili kutoa michango kwa ajili ya hosteli pamoja na maabara.

Alisema kuwa, majengo ya maabara bado hayajakamilika licha ya serikali kupeleka vifaa vya maabara na hii bado ni changamoto inayowafanya wanafunzi kutofanya vizuri kwenye masomo yao.

Aidha, Diwani wa Kata ya Kibosho Magharibi, Deo Mushi, ameahidi kushirikiana na wazazi kuhakikisha kwamba wanasaidiana katika ujenzi wa hosteli hizo.

Alisema kuwa, licha ya kwamba shule hiyo haipo kwenye kata yake, lakini yupo tayari kusaidia ujenzi wa mabweni hayo.



Ukurasa 20

Ndoa ya kuungana na bilionea, tajiri 'akichacha ndio mwisho'



Ukurasa 18

Unataka kutajirika kupitia pilipili hoho? Ingia darasa kitaalamu



Ukurasa 15

## Shinikizo la mabinti 10, pedi yafutiwa kodi

# BUFE

Ijumaa Januari 31, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



### KILIMO PILIPILI KICHAA...

# Mradi utakaoajiri vijana mamia Unguja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MIAKA 20 iliyopita, Zanzibar ilikua mzalishaji mzuri wa zao la pilipili kichaa, ikisafirishwa nje ya nchi. Lakini leo hii, uzalishaji wake umepungua.

Zao la pilipili kichaa, ni miongoni mwa viungo vya mboga na limekuwa likitumika katika chakula. Wizara ya Biashara na Viwanda ya Zanzibar, hivi sasa imedhamiria kurejesha hadhi ya uzalishaji wa zao hilo, baada ya kuona inahitajika sana katika soko la ndani na nje ya nchi.

Hivi sasa wizara, kwa kushirikiana na Shirika la Biashara Zanzibar (ZSTC), imeshaandaa shamba darasa la pilipili kichaa lenye matarajio kuvunwa tani 200, mkakati unaoshirikisha mabaraza ya vijana ya mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja, ili vijana hao wajikite katika kilimo biashara cha zao hilo na kuondokana na ukosefu wa ajira.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

**Suala la pamba: Wadau walilia bei, serikali lao pembejeo na ubora wake** Ukurasa 14

BIASHARA

# Suala la pamba: Wadau walilia bei, serikali lao pembejeo na ubora wake



Pamba iliyokusanywa kwa ajili ya kuwekwa ghalani.



Upimaji pamba ukiendelea sokoni.

**Na Nimi Mweta**

WADAU katika sekta ndogo ya pamba ndani ya sekta ya kilimo kwa jumla na kama sehemu ya mkakati mpana wa mazao ya biashara nchini kupata fedha za kigeni za kutosha na kuweka msingi wa uchumi wa viwanda, wameanza mjadala mpya.

Ni kutokana na ripoti iliyowasilishwa wizarani na kikao kuitishwa cha wakuu wa mikoa inayolima pamba kwa wingi,ambayo maeneo muhimu ya mjadala yaliainishwa katika taarifa za vyombo vya habari.

Kimsingi, serikali inataka wizara iwasilishe pembejeo za zao hilo haraka kila msimu na kusimamia kuondolewa pembejeo feki sokoni, wakati wadau walieleza wasiwasi kuhusu bei wanayotaka.

Pamba ni moja ya mazao makubwa ya kibiashara nchini, yanayofanyiwa utafiti na kutolewa mapendekezo kuhusu sera za serikali kuhusiana na zao hio kila wakati.

Kuna, wakati pamba ilikuwa ndiyo zao tangulizi la kujenga Tanzania ya Viwanda baada ya Azimio la Arusha mwaka 1967. Serikali ya awamu ya kwanza nchini ilianzisha viwanda kadhaa vya nguo na hata kupata msaada kwa China kujenga kiwanda kikubwa cha nguo, jijini Dar es Salaam.

Vilianza kusuasua miaka 15 baadaye, hasa kutokana na kuathiriwa na bei mbaya katika soko la kimataifa, ubora hafifu na kutokuweza kutengeneza nguo za bei rahisi kwa soko la ndani, ilivyotazamiwa.

> “Pamba ni moja ya mazao makubwa ya kibiashara nchini, yanayofanyiwa utafiti na kutolewa mapendekezo kuhusu sera za serikali kuhusiana na zao hio kila wakati.



Dk. Charles Tizeba, aliposhiriki uvunaji pamba, katika zama zake alipokuwa Naibu Waziri wa Kilimo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Moja ya maeneo ya dhamira na utawala yanayojitokeza katika suala la pamba, tatizo liko katika hatma ya zao lenyewe, kama wakulima wanalitaka kwa faida yao binafsi au sehemu ya mkakati mpana zaidi wa kiuchumi nchini.

Hiyo ni kutokana na mkakati uliopo, ndiyo maana suala hilo linarudi mezani kujadiliwa kila wakati, kwani tatizo hapo siyo wakulima wanaopata tabu soko, kwa maana ya kupata pembejeo (mbegu na mbolea, vifaa tofauti) halafu watake msaada serikalini.

Tatizo lililoko ni wao kuhitajiwa kulima pamba, hivyo wanataka mazingira yaboreshwe, ili kuwapa motisha wa kutosha kutekeleza dhamira hiyo.

Wanatakiwa waelewe mjadala na mapendekezo katika sekta ndogo ya pamba na mwelekeo wake. Suala la msingi lililoko ni kuangalia aina ya uhusiano uliopo na picha inayotoa ufafanuzi wake ulivyokaa.

**AINA YA UHUSIANO**

Kuna uhusiano wa aina tatu, ambao unawezekana kuwapo kwenye suala la aina hilo;tatizo la kiraia, soko na uwakala.

Uraia ni aina ya matatizo katika sekta, ambayo serikali inahusika nayo tu katika utawala wa sheria, kwa mfano mtu anapoanzisha duka mahali fulani atakuwa ameridhika na miundombinu inayomuwezesha kufungua duka, ila kunawezekana kukawapo upungufu kadhaa, au kunazuka upungufu kama huo na yeye mdau kiuchumi yanamhusu.

Ni hapo kunapatikana lawama zinazowezekana serikali ya mtaa au mwelekeo wa kisheria kwa jumla, kwa mfano kutofunguliwa duka mapema siku ya kufanya usafi, mojawapo ya sheria ndogo za kiserikali wilayani.

Tatizo la aina ya pili linahusu soko; hapo ingekuwa ni mkulima kuwa na dhamira ya kuendelea kuhangaika na pamba kama bidhaa, kwa mahitaji yake mwenyewe.

Suala la msingi katika hali hiyo, ni uhusiano kati ya kutumia nguvu kiwango fulani na faida inayopatikana kwa nguvu hiyo na gharama, kwa mfano za pembejeo.

Kinachoamua hapo ni mtiririko au mwelekeo wa bei kila baada ya muda kupita, inaamua namna ya kumshikilia mkulima wa zao.

Aina ya tatu ya uhusiano, inaangukia katika uwakala, ambako wakulima inabidi walime pamba kwa sababu ni zao muhimu katika mipango ya uchumi, hasa kupata fedha za kigeni kwa kuuza zao hilo nje ya nchi.

> “Yako maeneo yenye matatizo katika sekta ndogo ya pamba kwa ujumla. Hilo linaendana na sekta ya madini, hasa uchimbaji wa kisanii au kiholela katika maeneo mengi.

**INAIBUKAJE?**

Katika miaka ya karibuni pamba imekuwa pia ni kianzio cha kutazamia kupata msukumo halisi katika kuinua uchumi wa viwanda, ila mazingira mapana ya utandawazi yamezuia kasi ya kung’ara kwa kilichokuwa kinalengwa kufuatiliwa kwa nguvu.

Dhamira ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuondoa uingizaji nguo zilitumika ili kujenga upya sekta ya nguo katika nchi hizo ilikwama, pale Marekani ilipotishia kuzifuta nchi hizo katika mpango wake wa biashara wa AGOA, unaounda urafiki wa kimasoko.

Kushamiri kwa uzalishaji wa bidhaa hiyo shambani, pia kufikia uchumi wa viwanda, ni sharti kuendane na mahitaji ya utandawazi ulioshika dunia hivi sasa.

Yako maeneo yenye matatizo katika sekta ndogo ya pamba kwa ujumla. Hilo linaendana na sekta ya madini, hasa uchimbaji wa kisanii au kiholela katika maeneo mengi.

Hiyo inatokana na ukweli wa kutoweza kufikia viwango vya mazingira ya kufanya kazi, inayomlinda mkulima au kwa maana hiyo, mchimba madini mdogo anayejaribu kupata riziki katika mazingira magumu.

Tofauti yao ni mkulima mara nyingi zaidi analima katika ardhi anayomiliki hana vifaa bora vya kazi na amekosa uwezo wa kupanga bei inayomridhisha, wakati wachimba madini wengi ni waliokimbia ‘hiyo pamba’ kutafuta eneo ambalo angalau mapato yanaweza kuendana na jitihada anayoweka.

Siyo rahisi kusema kama wachimba madini au vibarua wamefaulu zaidi, hali ambayo si bora zaidi kuliko pamba. Ndiyo maana, inakuwa mtihani kwa mamlaka kuweka mazingira toshelezi ya kulima pamba, wakati bei yake kimataifa inayumba kwa sababu mbalimbali.

Nchini, pamba inalimwa kwa asili, inahitaji pembejeo za aina tofauti, ambazo ni za gharama kubwa kwa mlimaji, wakati kuna nchi zilizofanikiwa zinalima pamba kijenetiki (pengine tungesema kidijitali ili mawazo yabaki kunakofahamika) halafu tunashindana nao. Hao gharama zao ni ndogo.

Isitoshe, nchi kama Marekani na nyinginezo ni takriban nusu karne zilishaachana hata na matrekta kutumia trekta-tela kuvuna, kuchambua, kujaza katika magunia na kushona, tayari kwenda viwandani.

Mashine hizo zinahitaji tu kujazwa mafuta na kumlipa dereva, siyo wakulima kwa maelfu. Ni katika mazingira hayo, ambako ushindani ni kati ya wenye hizo ‘combine harvesters’ na siyo kati yetu na wao, kwani tunajikongoja tu kujaribu kulima pia.

## Shinikizo la mabinti 10, pedi yafutiwa kodi

- Wavulana 2 waliwaunga
- Yageuka kampeni kitaifa




Mabinti wakishiriki kampeni, baada ya kupokea pedi zao. **PICHA: MTANDAO**

**Kigali,** RWANDA

NI mada kuu katika mtandao wa Twitter nchini Rwanda, likiwa na lengo la kusaidia wasichana wanaotoka katika familia maskini.

Hiyo ni kampeni iliyoanzishwa na wasichana 10 na wavulana wawili, katika vita ya kusaidia wasichana wanaokosa taulo za kike, hasa wale watokao katika nyumba maskini

Kimsingi ni msukumo uliozaa matunda, kwani mwezi uliopita, serikali ya Rwanda iliondoa kodi hiyo na Saidath Murorunkwere, mwanaharakati wa masuala ya kijinsia nchini Rwanda, anaitolea ufafanuzi:

“Tumeondoa Kodi ya Ingezeko la Thamani (VAT) kwa ‘sodo’ (taulo za kike) ili kurahisisha upatikanaji wake kwa wanawake na wasichana, pakiti moja inauzwa kwa karibia dola moja ya Marekani (Sh 2,200).

“Hatua hii ni nzuri, lakini gharama ya ‘visodo’ bado iko juu kwa familia nyingi maskini kote nchini Rwanda na kuhatarisha afya ya wasichana wengi, kutoka familia maskini”

Asilimia 35 ya wakazi wa Rwanda, kiuchumi wanatajwa na Benki ya Dunia kuwa wanaishi katika kipato nchini chini ya dola mbili kwa siku (Sh.4,400), hali inayowaopa mtihani mgumu kupata uwezo wa kumudu gharama ya kununua taulo za kike kuwakimu wakati wa hedhi zao.

Mnamo mwezi Septemba mwaka jana, msichana Jeannine Kizima na rafiki zake, walianzisha kampeni ya kutafuta ‘visodo’ kutoka kwa wafadhili na kila walipozipata, waligawanya bila ya malipo kwa wasichana kutoka familia maskini, zisizomudu kuwanunulia mabinti zao taulo hizo.

Hadi sasa imegeuka kuwa kampeni yenye mafanikio,kwa maana ya raia wa Rwanda wamekuwa wakiwahimiza rafiki zao kuunga mkono kampeni hiyo.

“Tulikuwa tumefikia shule mbili pekee eneo la Kaskazini, lakini kwa sababu watu wengi wanatoa ahadi zao, nimatumaini yetu kwamba tutafikia idadi kubwa ya wasichana kadiri ya uwezo wetu” anaeleza mwanaharakati huyo – Jeannine.

Kampeni yao, pia inatajwa kwamba haishii katika lengo la kugawanya taulo za kike tu, bali pia kumaliza imani potovu na ukimya katika masuala ya afya ya uzazi na hedhi miongoni mwa familia na wasichana nchini Rwanda.

“Katika masuala ya afya ya uzazi kama vile hedhi, familia ziko kimya, wasichana wako kimya huku wanaume wengine wakilichukulia kama mwiko kulizungumzia.

“Tunapofikia wasichana hawa, hatugawanyi tu ‘sodo’ tulivyokusanya, bali pia tunawafundisha na kuwafanya wazungumzie wazi masuala kama hayo ambayo bado ni mwiko,” anasema Jeannine.

Wakati anatoa ufafanuzi huo, anarejea wastani wa ndani ya saa 24 kupita, walishapokea ahadi zaidi za paketi 1000 ya taulo za kike na zinaendelea kumiminika.

“Tunafuraha kupita kiasi na matumaini makubwa ya kufikia wasichana wengi zaidi shuleni, ambao familia zao haziwezi kununua pedi,” anasimulia.


Suala la kampeni za kijamii kutaka upatikanaji wa pedi kuzifikia kata masikini hivi sasa lina sura ya kimataifa, hata nchini Tanzania wanaharakati wa kijamii wakiwa mstari wa mbele kuona haki inatendeka kwa mabinti hao.

*** Kwa mujibu wa vyombo vya kimataifa.**

# ...alilia bei, ...bora wake



...koni.



inayotoa ufafanuzi wake ulivyokaa.

**AINA YA UHUSIANO**

Kuna uhusiano wa aina tatu, ambao unawezekana kuwapo kwenye suala la aina hilo;tatizo la kiraia, soko na uwakala.

Uraia ni aina ya matatizo katika sekta, ambayo serikali inahusika nayo tu katika utawala wa sheria, kwa mfano mtu anapoanzisha duka mahali fulani atakuwa ameridhika na miundombinu inayomuwezesha kufungua duka, ila kunawezekana kukawapo upungufu kadhaa, au kunazuka upungufu kama huo na yeye mdau kiuchumi yanamhusu.

Ni hapo kunapatikana lawama zinazowezekana serikali ya mtaa au mwelekeo wa kisheria kwa jumla, kwa mfano kutofunguliwa duka mapema siku ya kufanya usafi, mojawapo ya sheria ndogo za kiserikali wilayani.

Tatizo la aina ya pili linahusu soko; hapo ingekuwa ni mkulima kuwa na dhamira ya kuendelea kuhangaika na pamba kama bidhaa, kwa mahitaji yake mwenyewe.

Suala la msingi katika hali hiyo, ni uhusiano kati ya kutumia nguvu kiwango fulani na faida inayopatikana kwa nguvu hiyo na gharama, kwa mfano za pembejeo.

Kinachoamua hapo ni mtiririko au mwelekeo wa bei kila baada ya muda kupita, inaamua namna ya kumshikilia mkulima wa zao.

Aina ya tatu ya uhusiano, inaangukia katika uwakala, ambako wakulima inabidi walime pamba kwa sababu ni zao muhimu katika mipango ya uchumi, hasa kupata fedha za kigeni kwa kuuza zao hilo nje ya nchi.

> **“Yako maeneo yenye matatizo katika sekta ndogo ya pamba kwa ujumla. Hilo linaendana na sekta ya madini, hasa uchimbaji wa kisanii au kiholela katika maeneo mengi.**

**INAIBUKAJE?**

Katika miaka ya karibuni pamba imekuwa pia ni kianzio cha kutazamia kupata msukumo halisi katika kuinua uchumi wa viwanda, ila mazingira mapana ya utandawazi yamezuia kasi ya kung'ara kwa kilichokuwa kinalengwa kufuatiliwa kwa nguvu.

Dhamira ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuondoa uingizaji nguo zilitumika ili kujenga upya sekta ya nguo katika nchi hizo ilikwama, pale Marekani ilipotishia kuzifuta nchi hizo katika mpango wake wa biashara wa AGOA, unaounda urafiki wa kimasoko.

Kushamiri kwa uzalishaji wa bidhaa hiyo shambani, pia kufikia uchumi wa viwanda, ni sharti kuendane na mahitaji ya utandawazi ulioshika dunia hivi sasa.

Yako maeneo yenye matatizo katika sekta ndogo ya pamba kwa ujumla. Hilo linaendana na sekta ya madini, hasa uchimbaji wa kisanii au kiholela katika maeneo mengi.

Hiyo inatokana na ukweli wa kutoweza kufikia viwango vya mazingira ya kufanya kazi, inayomlinda mkulima au kwa maana hiyo, mchimba madini mdogo anayejaribu kupata riziki katika mazingira magumu.

Tofauti yao ni mkulima mara nyingi zaidi analima katika ardhi anayomiliki hana vifaa bora vya kazi na amekosa uwezo wa kupanga bei inayomridhisha, wakati wachimba madini wengi ni waliokimbia 'hiyo pamba' kutafuta eneo ambalo angalau mapato yanaweza kuendana na jitihada anayoweka.

Siyo rahisi kusema kama wachimba madini au vibarua wamefaulu zaidi, hali ambayo si bora zaidi kuliko pamba. Ndiyo maana, inakuwa mtihani kwa mamlaka kuweka mazingira toshelezi ya kulima pamba, wakati bei yake kimataifa inayumba kwa sababu mbalimbali.

Nchini, pamba inalimwa kwa asili, inahitaji pembejeo za aina tofauti, ambazo ni za gharama kubwa kwa mlimaji, wakati kuna nchi zilizofanikiwa zinalima pamba kijenetiki (pengine tungesema kidijitali ili mawazo yabaki kunakofahamika) halafu tunashindana nao. Hao gharama zao ni ndogo.

Isitoshe, nchi kama Marekani na nyinginezo ni takriban nusu karne zilishaachana hata na matrekta kutumia trekta-tela kuvuna, kuchambua, kujaza katika magunia na kushona, tayari kwenda viwandani.

Mashine hizo zinahitaji tu kujazwa mafuta na kumlipa dereva, siyo wakulima kwa maelfu. Ni katika mazingira hayo, ambako ushindani ni kati ya wenye hizo 'combine harvesters' na siyo kati yetu na wao, kwani tunajikongoja tu kujaribu kulima pia.

# Shinikizo la mabinti 10, pedi yafutiwa kodi

## • Wavulana 2 waliwaunga
## • Yageuka kampeni kitaifa




Mabinti wakishiriki kampeni, baada ya kupokea pedi zao.
**PICHA: MTANDAO**

**Kigali,** RWANDA

NI mada kuu katika mtandao wa Twitter nchini Rwanda, likiwa na lengo la kusaidia wasichana wanaotoka katika familia maskini.

Hiyo ni kampeni iliyoanzishwa na wasichana 10 na wavulana wawili, katika vita ya kusaidia wasichana wanaokosa taulo za kike, hasa wale watokao katika nyumba maskini

Kimsingi ni msukumo uliozaa matunda, kwani mwezi uliopita, serikali ya Rwanda iliondoa kodi hiyo na Saidath Murorunkwere, mwanaharakati wa masuala ya kijinsia nchini Rwanda, anaitolea ufafanuzi:

"Tumeondoa Kodi ya Ingezeko la Thamani (VAT) kwa 'sodo' (taulo za kike) ili kurahisisha upatikanaji wake kwa wanawake na wasichana, pakiti moja inauzwa kwa karibia dola moja ya Marekani (Sh 2,200).

"Hatua hii ni nzuri, lakini gharama ya 'visodo' bado iko juu kwa familia nyingi maskini kote nchini Rwanda na kuhatarisha afya ya wasichana wengi, kutoka familia maskini"

Asilimia 35 ya wakazi wa Rwanda, kiuchumi wanatajwa na Benki ya Dunia kuwa wanaishi katika kipato nchini chini ya dola mbili kwa siku (Sh.4,400), hali inayowaopa mtihani mgumu kupata uwezo wa kumudu gharama ya kununua taulo za kike kuwakimu wakati wa hedhi zao.

Mnamo mwezi Septemba mwaka jana, msichana Jeannine Kizima na rafiki zake, walianzisha kampeni ya kutafuta 'visodo' kutoka kwa wafadhili na kila walipozipata, waligawanya bila ya malipo kwa wasichana kutoka familia maskini, zisizomudu kuwanunulia mabinti zao taulo hizo.

Hadi sasa imegeuka kuwa kampeni yenye mafanikio,kwa maana ya raia wa Rwanda wamekuwa wakiwahimiza rafiki zao kuunga mkono kampeni hiyo.

"Tulikuwa tumefikia shule mbili pekee eneo la Kaskazini, lakini kwa sababu watu wengi wanatoa ahadi zao, nimatumaini yetu kwamba tutafikia idadi kubwa ya wasichana kadiri ya uwezo wetu" anaeleza mwanaharakati huyo – Jeannine.

Kampeni yao, pia inatajwa kwamba haishii katika lengo la kugawanya taulo za kike tu, bali pia kumaliza imani potovu na ukimya katika masuala ya afya ya uzazi na hedhi miongoni mwa familia na wasichana nchini Rwanda.

"Katika masuala ya afya ya uzazi kama vile hedhi, familia ziko kimya, wasichana wako kimya huku wanaume wengine wakilichukulia kama mwiko kulizungumzia.

"Tunapofikia wasichana hawa, hatugawanyi tu 'sodo' tulivyokusanya, bali pia tunawafundisha na kuwafanya wazungumzie wazi masuala kama hayo ambayo bado ni mwiko," anasema Jeannine.

Wakati anatoa ufafanuzi huo, anarejea wastani wa ndani ya saa 24 kupita, walishapokea ahadi zaidi za paketi 1000 ya taulo za kike na zinaendelea kuminika.

"Tunafuraha kupita kiasi na matumaini makubwa ya kufikia wasichana wengi zaidi shuleni, ambao familia zao haziwezi kununua pedi," anasimulia.

Suala la kampeni za kijamii kutaka upatikanaji wa pedi kuzifikia kata masikini hivi sasa lina sura ya kimataifa, hata nchini Tanzania wanaharakati wa kijamii wakiwa mstari wa mbele kuona haki inatendeka kwa mabinti hao.

*** Kwa mujibu wa vyombo vya kimataifa.**

BIASHARA

KILIMO PILIPILI KICHAA...

# Mradi utakaoajiri vijana mamia Unguja

• Waziri awahakikishia kipato njia nyeupe • Darasa la Bagamoyo lawapa jibu uhakika • Shirika Biashara: Iko wazi soko linawangoja • Kila mwezi 'mshahara'... staili ya kazini



Soko Kuu la Mwanakerekwe, ambako kunatarajiwa bidhaa mpya ya pilipili kichaa kuuzwa. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**INATOKA UK.13**

Waziri wa Bishara na Viwanda Balozi, Amina Salum Ali, anasema umefika wakati kwa vijana kubadili fikra, kuondokana na mtazamo na mawazo ambao wengi wao wanatamani mtazamo wa taaluma kama mabaharia, wanajeshi, pia ajira za uaskari serikalini.

Kwa mujibu wa Amina, mtazamo mkuu unaopaswa ufutatwa ni kujikita katika kilimo biashara na vijana kujitegemea na kubadili mawazo yao ya kutegemea fursa chache za ajira za serikalini pekee, wakati ziko chache na kundi la vijana ni kubwa.

"Umefika wakati sasa kwa vijana kubadili fikra na mawazo ambao wengi wenu mnatamani kuwa mabaharia, wanajeshi au askari polisi," anasema.

Anaishauri Wizara ya Vijana Zanzibar, kuendeleza elimu kwa vijana wabadili mawazo yao, kutoka utegemezi na wajiekeze katika kilimo cha biashara.

Kwa kurejea dhana ya nafasi ya kilimo cha pilipili kichaa, Balozi Amina anasistiza kilimo ni kizuri, kwani hakina gharama kubwa, ikilinganishwa na kinginecho na wakati huohuo, kina mahitaji makubwa zaidi sokoni.

> **"Umefika wakati sasa kwa vijana kubadili fikra na mawazo ambao wengi wenu mnatamani kuwa mabaharia, wanajeshi au askari polisi.**

"Soko la pilipili kichaa lipo la uhakika, hivyo vijana niwaombe kuchangamkia fursa hiyo, ili kuweza kupata maendeleo," anasisitiza Balozi Amina.

Waziri anawakumbusha namna katika kipindi kilichopita Zanzibar ilikuwa mzalishaji mzuri wa pilipili kichaa, hata kuwaza kusafirisha kwa wingi nje ya nchi bidhaa hiyo, lakini ghafla soko lilianguka na wananchi wakaacha kulima kilimo hicho.

Anasema, wizara yake imejipanga kuchangia uanzishwaji tena wa kasi wa kilimo hicho, baada ya kutembelea shamba la pilipili kichaa Bagamoyo, Tazania Bara na kushuhudia faida inayopapatikana toka kwa wakulima wa eneo hilo, mkoani Pwani



Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali.

### DARASA BARA

Pia, anataja mradi huo unaenda sambamba na sera ya Zanzibar ya Viwanda na Kilimo ambapo Zanzibar bado ipo nyuma katika suala hilo na nchi, akikiri Zanzibar iko nyuma katika uzalishaji huo, ikilinganishwa na Tanzania Bara iliyofika mbali katika uzalishaji wake.

Anasema, baada ya kutembelea na kukishuhudia kilimo hicho nchini Tanzania bara na kuona matokeo ya mradi huo, anaamini utawasaidia vijana Wazanzibar kupitia kilimo anachokitafsiri kuwa ni rahisi.

"Hatutaki kuwafanya vijana wetu wa Zanzibar kama mayai na ndio maana tukawashirikisha vijana katika mradi huu, ili kupata ajira na kujikomboa kiuchumi," anasema.

Anasema Sera ya Biashara Zanzibar, ni kutoanzishwa biashara ambayo haina uhakika wa kuuzwa au kukosa soko na ndio maana wakaazisha kilimo hicho kwa sababu ya kuwapo soko la uhakika.

Aliongeza kwa kauli: "Mwelekeo wetu, kila mmoja awe na pesa katika nyumba, hivyo lazima vijana wafanye kazi na kazi zenyewe ni kama hizi".

### SHIRIKA BIASHARA

Said Seif Mzee, ni Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC). Anasema, malengo ya mradi huo wa kilimo cha pilipili kichaa ni kujiweka katika kilimo cha kibiashara, kwani ni muda mrefu Wazanzibari wako katika kilimo kisicho cha kibiashara.

Aidha, anawataka vijana wajitahidi katika kilimo cha biashara, hasa uzalishaji viungo, ambacho kina soko zuri na kina uwezo wa kuwasaidia kiuchumi. Anaendelea:

"Lengo la serikali kuanzisha mradi huu, ni kuwasaidia vijana kupata ajira, kwani vijana wanapokua na ajira vitendo vingi vya uhalifu hupungua."

Mzee anaeleza kwamba, kuna mtazamo mwingine wa kutanua fursa za kilimo cha biashara, kwa kujaza nafasi ya karafuu iliyobaki kuwa zao pekee.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, anaeleza kuwa ZSTC kwa muda mrefu imesimamia soko la pilipili kwa muda mrefu, hivyo anawataka wakulima kuzalisha zao hilo kwa wingi na kujitanua katika mazao ya biashara hasa ya viungo, ambayo yana bei nzuri sana hivi sasa.

### MTALAMU PILIPILI

Mtaalamu wa kilimo cha pilipili kichaa Josephat Kigondo, alisema zao hilo sio geni na lilikuwapo miaka mingi, kisha lilipotea, kwa sababu ya kukosa soko na uzalishaji ukadorora.

Anasema, hivi sasa soko la zao hilo limerudi kwa kasi na anawataka vijana hao wanaohimizwa na wakulima wengine kufanya bidii katika kilimo, ili kuendana na kasi ya soko la zao hilo.

Kigondo anataja njia mojawapo ya kulifanyia bidii zao hilo ili uzalishaji wake kuwa bora, ni kutumia mbinu za kisasa katika kilimo, ikiwamo umwagiliaji maji na mimea ya zao hilo kutunzwa.

"Zao hili lina faida sana. Kwanza, mmea wake unahimili magonjwa, unakupa miaka mitatu ya mavuno bila ya wasiwasi wowote na unakupa muda mwingi wa kupata kipato," anasema mtaalamu huyo.

Alisema kilimo hicho kinakupa uwezo wa kuvuna miaka mitatu mfululizo bila ya kupanda mimea mingine na hauwezi kufa hivyo mkulima hupata mavuno bila ya kuwa na wasiwasi na humpa muda mrefu wa kupata kipato .

Kigindo anaeleza kwamba, katika shamba la kijiji cha Pangatupu wamelima ekari 15 zilizopandwa zao na kila ekari ina wastani wa miche 10,000 na iwapo itakuwa vizuri, vijana wa eneo hilo watakua na uhakika wa kuvuna kilo 600 kwa mwezi, wakijipatia wastani wa shilingi milioni mbili.

### VIJANA WAONGEA

Kwa upande wao vijana kutoka mabaraza ya vijana wa mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja, ambao ndio walengwa wa mradi, wanaipongeza Serikali ya

Zanzibar kwa kuwapatia mradi wanaoutafiri kuwa ni neema kubwa kwao.

"Tuna imani kuwa kile kilio cha vijana wengi cha kutokuwa na ajira sasa kitapungua, kwa sababu mradi huu wa kilimo biashara, ni mkombozi kwetu sisi vijana," anatamka Shein Khamis Mohamed, Mwenyekiti wa Mabaraza ya Vijana Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja kwa niaba ya vijana wenzake.

Shein anauelezea mradi ni neema kubwa kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja na utaongeza idadi ya vijana waliojiajiri kupitia sekta ya kilimo, hivyo watahakikisha kilimo hicho wanakiendeleza na kutoa elimu kwa vijana wengine kujiajiri.

"Tunatarajia Desemba mwaka huu, tunaanza mavuno ambayo makisio katika ekari hizi 15 ambazo zimewahusisha vijana 60, kila mmoja atakuwa na uhakika wa kupata (Sh.) 400,00 kwa mwezi ambao ni mshahara kamili ...wengine hawakipati kiwango hicho cha fedha," anasema.

### WAFANYABIASHARA

Mosi Juma ni mjasiriamali anaetengeneza chipsi za Muhogo, anasema kuna wakati anapata usumbufu anapotengeneza bidhaa zake kwa kukosa pilipili kichaa, hivyo kuanzishwa kilimo hicho kutamrahisishia upatikaji wa bidhaa hiyo pasipo usumbufu.

"Wakati mwingine unahangaika sokoni kutafuta unga wa pilipili kichaa, ambazo nimekuwa natumia kuweka katika bidhaa zangu, ili ziweze kuwa na ladha nzuri," anasema.

Anaeleza, pindi pilipili hiyo inapoadimika sokoni, hulazimika kununua nyingine za kuwasha, ambazo sio nzuri kwa katika bidhaa zao.

Mfanyabiashara mwingine, Ali Juma, ana maelezo kwamba, amekuwa akitumia pilipili kichaa katika bidhaa yake ya mahindi ya kuchoma akiichanganya na chumvi, inayopendwa sana na wateja wake.

Ni mradi unaotarajiwa kuwafikia vijana 100 kutoka mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja, wakinufaika.

# Biashara katika picha



Meneja Mkuu wa Pizza Hut Afrika, Ewan Davenport akikata utepe kuzindua mgahawa mpya katika eneo la Mikocheni, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa Dough Works Ltd ambayo inamiliki migahawa hiyo, Vikram Pesai (kushoto) na Meneja wa mgahawa huo, Emmanuel Shizya. **NA MPIGAPICHA WETU**




Wateja wa Diamond Trust Tanzania, wakiwa katika kifungua kinywa kilichoandaliwa na benki hiyo, kama ishara ya kumaliza ukarabati wa tawi la Masaki, lililopo Barabara ya Chole, jijini Dar es Salaam. DTB Tanzania ina matawi 28, 13 jijini Dar es Salaam na mengine 15 katika miji mingine nchini. **PICHA: DTB**



Wachuuzi wa mananasi, wakisubiri wateja katika soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam, mapema wiki hii. Nanasi linauzwa kwa bei ya Sh. 500 hadi Sh.1000, kulingana na ukubwa wake. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UCHUMI

# Unataka kutajirika kupitia pilipili hoho? Ingia darasa la kitaalamu

• Utunzaji& mavuno; wadudu, magonjwa

**Na Mwandishi Wetu**

PILIPILI hoho ni zao la viungo linalolimwa zaidi katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Mbeya na Iringa. Inatumika kwenye vyakula mbalimbali kama nyama, viazi na ndizi.

Vilevile inatumika kutengeneza kachumbari, baada ya kukaushwa na kusagwa ili kupata unga wenye faida ya vitamini A, B,C; madini chokaa na chuma.



Mkulima wa pilipili hoho akiandaa shamba. Picha ndogo, mazao shambani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



**MAZINGIRA YAKE**

Ni zao linakua vizuri kwenye nyuzi joto 18 hadi 20 sentigredi, likiwa na tabia joto linapozidi, maua na matunda yake huanguka. Linahitaji mvua za wastani milimita 600 hadi 1500, katika udongo wenye mboji nyingi, usiotuamisha maji.

**MAANDALIZI**

Kuna aina zaidi ya 10 ya zao hilo na mfumo wa upandaji wake ni kwamba, kunatengezwa tuta lenye upana wa mita moja, linalowekewa mbolea za asili zilizooza vizuri kiasi cha ndoo mbili au zaidi katika kila eneo la mita mraba moja.

Mbolea hiyo inapochanganywa vizuri na udongo, kisha mlimaji anatengeneza mifereji vyenye nafasi ya sentimeta 10 hadi 15, yenye kina cha sentimeta moja hadi tatu katika eneo hilo.

Hapo ndipo kunakopandizwa miche katika eneo na kisha kunamwagiliwa maji, hatua inayoendelea kila siku asubuhi na jioni hadi mbegu zitakapoota na baada ya hapo, umwagiliaji uendelee kati ya siku sita hadi 10.

**UTAYARISHAJI SHAMBA**

Shamba linaandaliwa kwa mwezi mmoja, kabla ya kupandikiza miche ardhini kina cha sentimeta 30. Hapo inawekwa mbolea za asili kiasi cha tani 10 hadi 15 kwa hekta, ambayo ni debe moja inayotakiwa kuchanganywa vizuri; mbolea na udongo

Ikiwa kuna upungufu wa madini aina ya fosiforasi kwa uthibitisho wa wataalam hapo, weka mbolea chokaa kiasi kinachotakiwa ni kilo 200 kwa hekta, kisha lainisha udongo kati ya siku tatu hadi tano, kabla ya kupandikiza miche.

**UPANDIKIZAJI MICHE**

Miche huwa tayari kupandikizwa shambani baada ya wiki nne hadi 10, kwa kuitenganisha umbali wa sentimeta 40 hadi 50 kutoka shimo hadi jingine na mistari inapishana kwa upana sentimeta 60 hadi 75.

Ikiwa mbolea za asili hazikuwekwa wakati wa kutayarisha shamba, inawekwa kiasi cha nusu kilo hadi moja katika kila shimo la kupandia.

Siku moja kabla ya kuung'oa miche, mwagilia tuta ili kulainisha udongo na kuing'oa na udongo wake, kisha inapandikiza katika kina cha sentimita mbili zaidi kuliko ilivyokuwa kwenye kitalu na baada ya kupandikiza, inamwagiliwa maji ya kutosha. Ni kazi inayofanywa asubuhi na jioni.

> **"Utiriri Mwekundu (Red Spidermites): Ni wadogo wenye rangi nyekundu au machungwa yaliyoiva. Huonekana upande wa chini wa majani na hushambulia mmea kwa kufyonza utomvu wake.**

**UTUNZAJI SHAMBA**

Inapaswa kutandaza nyasi kavu ili kuhifadhi unyevu ardhini, kuongeza rutuba ya udongo, kuzuia magugu kuota na mmmomonyoko wa ardhi.

Kisha ifanyike palizi kwa magugu yanapoota, kwa staili ya kupandishia udongo kuzunguka shina, ili kuifunika mizizi na kuzuia mmea usiangushwe na upepo mkali.

Pilipili hoho hustawi vizuri zinapopata maji ya kutosha, hasa wakati wa kiangazi.

Zao hilo linahitaji mbolea za kukuzia zinazowekwa wakati maua yanapoanza kutoka, kiasi cha gramu tisa hadi 10 (kijiko kimoja kikubwa) kwa kila mmea.

Baada ya kupita majuma manne, inawekwa tena kwa vipimo vilivyoshauriwa

**WADUDU WAHARIBIFU**

Kuna wadudu waharibifu na magonjwa yao wapo;

*Vidukari au wadudu Mafuta (Aphids): Ni wadogo na wana rangi nyeusi, kijani au kahawia. Wanashambulia majani kwa kufyonza utomvu na kusababisha mmea kudumaa.

*Mbawakau: Wana rangi nyeusi na kahawia na mabawa yao nje ni magumu. Tabia yao ni kushambulia shina na kulifanya liwe na nundu.

Fukusi wa Pilipili (Pepper Weevil): Anatajwa kuwa hatari zaidi kwa zao hilo na hushambulia kupitia funza wake weupe wanaokula sehemu ya ndani ya matunda machanga na kusababisha yaanguke.

*Vithiripi (Thrips): Ni wadogo wenye rangi ya njano. Hushambulia majani na husababisha mmea unaong'aa, kunyauka, kuanzia ncha ya jani. Pia, wanaeneza magonjwa yatokanayo na virusi- kuna dawa za kuwadhibiti.

*Sota (Cutworms): Wana Tabia ya kukata miche michanga karibu usawa wa ardhi.

*Nzi Weupe (White flies): Ni wadogo wenye rangi nyeupe, na huonekana kama vumbi la unga kwenye majani. Mmea, unapotikiswa wanaruka. Kawaida yao, hushambulia mmea kwa kufyonza utomvu na hueneza ugonjwa wa virusi unaosababisha kujikunja kwa majani.

*Utiriri Mwekundu (Red Spidermites): Ni wadogo wenye rangi nyekundu au machungwa yaliyoiva. Huonekana upande wa chini wa majani na hushambulia mmea kwa kufyonza utomvu wake.

Makundi yote ya wadudu hao wanaosabisha madhara, kuna dawa maalam za kuwadhibiti kwa kila aina yao.

**MAGONJWA**

Magonjwa ya virusi hivyo ni mengi, ikiwamo majani kudumaa, kukunjana na kuwa na rangi ya njano. Hiyo inazuiwa kwa njia kadhaa, mojawapo ni kupanda aina ya pilipili zinazostahimili ya magonjwa hayo.

Njia nyingine ni kung'oa miche yenye dalili za magonjwa; kuzuia wadudu waenezao magonjwa ya virusi kwa kutumia dawa; kubadilisha mazao na baada ya kuvuna pilipili tamu, zao linalofuata lisiwe la jamii la zao hili kwa mfano nyanya na bilinganya.

Kuna ugonjwa unaosababishwa na ukungu na unashambulia matunda na kuwa na makovu ya mviringo mweusi, iliyochanganyika na kahawia.

Ugonjwa mwingine ni Madoa Bakteria, unaosababishwa na Bacteria na kushambulia majani machanga, baadaye matunda. Dalili zake ni madoa ya njano kwenye majani na matunda.

Kuna kuoza mizizi; huo ni ukungu unashambulia mizizi kuoza, mmea unanyauka na kufa na unapatikana zaidi kwenye unyevunyevu na joto jingi, hivyo inazuiwa kwa kuepuka kupanda pilipili kwenye sehemu inayotuamisha maji.

Mnyauko; Unaletwa na ukungu unaopatikana kwenye udongo na kushambulia shina libadilike rangi kuwa kahawia. Baadaye mmea hunyauka na kufa. Unazuiwa kwa kubadilisha mazao.

**UVUNAJI ULIVYO**

Pilipili hoho huwa tayari kwa kuvunwa baada ya wiki 10 hadi 14 tangu kupandikiza miche. Uvunaji huendelea kwa muda wa wiki nane hadi 10. Muda wa kuvuna hutegemea aina na matumizi yanayohitajika.

Pilipili kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, huvunwa zingali na rangi yake kijani kibichi inayong'aa na za kusindima kiwandani, huvunwa zikiwa zimekomaa zenye rangi nyekundu.

Matunda yakivunwa yangali machanga hunyauka kirahisi, Wastani wa mavuno ni tani 30 hadi 45 kwa kila hekta .

***Makala hii imenukuliwa kutoka tovuti ya Dira ya Mafanikio, ikimrejea mwandishi Saidi Malogo, aliyejitambulisha, mtaalamu wa kilimo.***

BIASHARA

ZAO LA SIDO

# Kiwanda mvinyo kilichomaliza shida ya soko zabibu Hombolo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA



Wakulima wa zabibu Kata ya Hombolo, wakikagua shamba lao. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

DODOMA na zao la zabibu, hazitengani. Uzalishaji wa zao hilo nalo limekuwa likiibua wasindikaji wa matunda hayo, kuandaa vinywaji vitokanavyo na bidhaa hiyo na kuunda mnyororo wa thamani mrefu.'

Kutokana na hilo, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) mkoani hapa, nalo haliko nyuma kuendelea kuibua viwanda vidogo kutengeneza vinywaji mahsusi aina ya wine, kwa jumla inaleta jibu la maendeleo ya kiuchumi.

Awali kulikuwapo changamoto ya wakulima kulalamika zabibu imekuwa ikiharibikia shambani na wanakosa pa kuzipeleka. Sido imeamua kubeba sehemu ya jukumu, kwa kutoa mafunzo ya utengenezaji na kuendeleza mnyororo wa thamani wa zabibu.

### MZALISHAJI

Kupita mtaa wa Sido, mjasiriamali Evarist Maganga, mkazi wa Mtaa wa Hombolo, mwenye kiwanda kidogo kwa jina la Wendeche, akisema bidhaa zake katika maeneo ya jiji Dodoma na nchi kwa jumla.

Ni hatua ambayo imekuwa nuru pia kwa wazalishaji zabibu wa Hombolo, ambao hivi sasa wamepata soko la karibu.

Mkurugenzi wa kiwanda, Maganga, anaiambia Nipashe kuwa jitihada zake hadi kufikia hatua hiyo ni zao la huduma za Sido, waliokuwa mstari wa mbele kutoa elimu ya utengenezaji wine.

Pia, usimamizi wa utengenezaji mlolongo mzima wa kinywaji mvinyo, ni suala lenye sura ya ukombozi mkubwa kwa mkulima wa zao hilo, kwa sababu wamepata soko la hakika la zabibu na sehemu ya kujifunza kuhifadhi lisiharibike, baada ya mavuno.

"Nitakuwa mchoyo wa fadhila katika mafanikio haya kama, sitamtaja Meneja wa Sido kwa jitihada za kufundisha na kuwainua wajasiriamali wa zao hilo," anatamka na kuendelea:

"Sido imetufanya tupige hatua sana wasindikaji na wakulima wa zabibu tunaishkuru sana na kuwataka kuendelea kuwashika mkono wakulima wa zao hili."

Maganga anasema, uwepo wa Wendeche katika Kata ya Hombolo, ni mafaniko makubwa kwa sababu kila mkulima sasa analima kwa jitihada kuhakikisha anapeleka sokoni, pia kuna somo la kutunzaji na kutengeneza mchuzi wa zabibu.

Kuhusu malengo yake, anataja anahitaji kufika mbali katika utengenezaji kinywaji - mvinyo pamoja na kuwainua wakulima wadogo, ili nao wafikie hatua ali-

> **Sido imetufanya tupige hatua sana wasindikaji na wakulima wa zabibu tunaishkuru sana na kuwataka kuendelea kuwashika mkono wakulima wa zao hili.**

yoifikia yeye katika kutengeneza Wine.

Maganga anasema anahitaji kuona kiwanda hicho kinakuwa na uwezo wa kutengeneza mvinyo zitazopelekwa nje ya nchi, kama zilivyo nyingine zinazoingizwa.

Anasema, hilo linawezekana kupitia Sido Dodoma kutokana na jitihada inazofanya kuhakikisha wajasiriamali wanaochukua mikopo yao, wanafika mbali katika malengo yao katika kutengeneza bidhaa zinazowakuza kiuchumi na kuendesha maisha yao na familia.

### AJIRA VIJANA

Maganga anataja lingine, ni kutoa ajira nyingi kwa vijana, ikiwa namna moja ya kujiendeleza na familia zao katika maeneo tofauti.

Kwa mujibu wa mmiliki huyo wa kiwanda, hivi sasa ana vijana wengi wanaojifunza na wakitoka hapo, wanakuwa katika nafasi ya kwenda kunazisha viwanda vyao kwa ajili ya kuwavuta wengine, katika mfumo waliopitia.

### MAFANIKIO?

Mkurugenzi Maganga anataja moja ya mafanikio anayojivunia, ni kusaidia kuinua vijana wengi kwa kuwapa ajira zinazowasaidia kimaisha, tofauti na kukaa vijiweni.

"Hii ni mafanikio makubwa sana kwangu, ukiacha mengine ambayo ninapata kupitia kiwanda cha Wendecher," anasema Maganga.

Anaiomba serikali kupitia wizara inayohusika na viwanda, kuendelea kuunga mkono kupitia Sido kuibua viwanda vidogo vya usindikaji na utengenezaji vinywaji vitokanavyo na zabibu.

Maganga anaitaka jamii hususani wakazi wa Dodoma, kutumia zao la zabibu kama mkombozi wao kiuchumi, kama ilivyo mikoa mingine nchini, inavyotumia mazao yanayolimwa na kustawi kwa wingi kujiinua kiuchumi.

### WANUFAIKA WAKE

Mbukwenyi, ni moja ya vikundi vinavyotaja mafanikio waliopata kupitia Wendeche katika soko la zabibu, pia kupata mikopo kutoka benki ya NMB, inayowafanya wapige hatua kubwa katika uzalishaji na ulimaji wa zao zabibu.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Samwel Abdallah, anasema moja ya changamoto kubwa waliokuwa nayo ni ukosefu wa soko la zabibu, lakini hivi sasa tatizo hilo limekwisha kwa sababu ya uwepo wa kiwanda cha Wendeche kilichopo jirani, Hombolo.

Anasema wanajivunia kufanya kazi nayo, kwa sababu amekuwa akiwashika mkono kila pale wanapoanguka hadi kufikia hapo walikofikia sasa.

"Awali zabibu zilikuwa zikiharibikia shambani, kwa sababu tulikuwa hatuna pa kuzipeleka, lakini hivi sasa Wendeche yupo," anasema Abdalah.

### SERIKALI

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, anasema jitihada za wajasiriamali wadogo zinapaswa kuangaliwa na kufanyiwa kazi na Sido, kwa sababu wao ndio wanaofanya kazi na wajasiriamali, hata kuwatambua kwa karibu.

Mhandisi Stella, anasema Sido inapaswa kuendelea kuwashika mkono, ikiwamo katika suala la kuwapa elimu ya kutosha ya usimamizi wa viwanda vidogo, pia utengenezaji mvinyo na kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao zabibu.

Anaiambia Sido kwamba wakifanya hivyo kadri siku zinavyoenda, viwanda vidogo vitaendelea kuwapo na hatimaye wataviendeleza kuwa vikubwa.

"Huu ni mwanzo tu naimani baadae tutazungumza mengine," anasema Mhandisi Manyanya.

### MENEJA WA SIDO

Sempeho Manongi, anamhakikishia Naibu Waziri kuwa Sido itaendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali, ili kuhakikisha wanafika mbali katika utengenezaji mvinyo.

Manongi anasema, wameanza na viwanda vidogo, lakini lengo ni kuwafikisha kumiliki vikubwa na anafafanua: "Tunaanza nao katika viwanda vidogo, lakini tunahitaji wawe na viwanda vikubwa na ndio lengo tulilojiwekea."

Manongi anataja mkakati mmowapo ni Sido Dodoma kutoa mafunzo kwa jamii, ili ipate uwezo wa kumiliki viwanda kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

UCHUMI

BIASHARA KILA KONA?

# Ndoa ya kuungana na bilionea, tajiri 'akichacha ndio mwisho'

**Na Gaudensia Mngumi**

BINADAMU wanaishi kwa matarajio ya kusubiri kutimia ndoto zao. Ndio uchumi wa kihistoria kwa mwanadamu.

Wengi wanapenda kuona maisha yao yanabeba sehemu kubwa ya furaha kuliko mahangaiko, dhiki, njaa na kero kutoka kwa mwenza wake.

Anatamani kuwa na mwenza mwenye kipato kikubwa na pengine anayempenda, ili kuondokana na shida zinazowakabili wengi leo hii.

Hata hivyo, maisha ya furaha hayaji yenyewe, bali ni jukumu la kila mmoja kuyatafuta. Ndivyo ilivyo hata kwenye uhusiano wa kimapenzi. Ubora wa ndoa hauishii katika ukaguzi wa fedha pekee.

Mtu anaiyeishi bila malengo, hawezi kufanikiwa katika maisha, kwa sababu mafanikio yoyote huja kutokana na hamu ya mtu kufikia anapoona panafaa kwa kufanya kazi.

Kutokana na kukua kwa maisha na mabadiliko yanayoikumba jamii hivi sasa, watu wana ndoto na matarajio tofauti, inapofananishwa na zamani.

Zamani, suala la kuoa lilionekana kuwa wajibu usiokwepeka, lakini hivi sasa ni tofauti. Uamuzi ya kuishi maisha ya ndoa, yanahitaji umakini na pengine tafakari ya kina.

Katika maisha ya ndoa ya sasa, anayevumilia anakuwa tayari kupenda, kujali, kuheshimu na hata kusaidia kwa namna yoyote. Kuna msamiati wake'uvumilivu' ndio nguzo ya kusogeza maisha ya wanandoa.

**KWA NINI?**

Mtu anaweza kujiuliza, chanzo cha hali kama hiyo ni nini hasa? Sababu ziko nyingi, lakini pengine muhimu kugusa zinazowafanya watu kufika uamuzi wa ama kuoa au kuolewa.

Vipo vigezo vingi vinavyowashawishi kufikia uamuzi wa ama kuoa au kuolewa. Wapo ambao ndoto zao ni kuolewa na wanaume wenye uwezo kipesa, au kinyume chake, mume kumtarajia mke mwenye 'pochi lililonona.'

Mtazamo wa kiuchumi sasa unaenda mbali katika mikusanyiko ya kijamii, mbali na ndoa, hata makazi, vikundi vya kijamii an hata aina ya shule wanazosoma watoto, dhana 'uchumi' ina nafasi yake kunda sura ya muungano ambayo katika sura ya pili, asiye na uwezo (maskini) anasogezwa kando.

Ni aina ya ndoto na falsafa za wengi, kutokana na hali halisi ya maisha iliyoko katika jamii, bila ya kusahau uchumi wa soko unaojipenyeza katika maisha.



Moja ya harusi ya kifahari iliyofanyika ughaibuni. Uimara wake, Pia unategemea sana ubora wa maadili toka kwa wawili. **PICHA: MTANDAO**

> **"Utajiri na uwezo kifedha, hauna nguvu wala dhamana ya kutetea na kulinda ndoa isivunjike.**

Imefika hatua, kila mtu angependa kuona maisha yake yanaenda vizuri na njia ya mkato iliyo, ni kutafuta mwenye uwezo wa kumsaidia kumudu maisha ya kila siku.

Ni msukumo wa mawazo unaowalazimisha watu kwenda katika fikra ya kunuia makubwa kuliko uwezo wao. Wanafikiria ama kuoa au kuolewa na wenye uwezo kifedha, bado wanasahau maisha bora ya ndoa hayaishii kwenye ama kuolewa au kuoana na watu wenye uwezo kifedha tu.

Utajiri na uwezo kifedha, hauna nguvu wala dhamana ya kutetea na kulinda ndoa isivunjike. Siku zote haijengwi kwa utajiri pekee.

Wapo wachache wenye mtazamo tofauti na hali ya maisha na wanafikiri, njia ya kufanikisha ndoa ni kigezo cha kifedhaa.

Maisha ya ndoa hayahitaji njia za mkato, haipo sababu ya kuoa au kuolewa na usiyempenda, mwisho wake unajivuna kwa utetezi wa sheria na kanuni ya kijamii "nimelazimika kufanya hivyo kwa sababu ya utajiri aua pesa alizo nazo."

**SWALI LAJITOKEZA**

Pesa hazina nafasi ya kulinda penzi la dhati. Sasa inakuwaje pale unayempenda kwa ajili ya pesa anapoishiwa? Jibu fupi ni kwamba, uhusiano unakuwa umefika mwisho.

Ni makosa, iwe kijamii, kisaikolojia na hata kisheria, kwa wanaofikiria kuwa kigezo cha ama utajiri au kuwapo mali nyingi, ni sehemu muhimu inayopa nafasi ya kupata rafiki, mchumba ama mke wa kuishi pamoja.

Katika suala la mapenzi, kila mmoja ana kigezo chake cha kumchagua anayemfaa kuwa rafiki, mchumba, ili amuandae kufikia hatua ya ndoa.

Sifa za anayeweza kuwa rafiki ziko nyingi. Hapo, inaweza kujumuishwa kwa kiasi fulani, mtazamo wa msukumo wa maisha kiuchumi.

Mara nyingi tunda la historia ya malezi binafsi, yana nafasi muhimu katika kutengeneza kigezo cha mtu kumsaka anayemfaa katika uhusiano ya kimapenzi, mpaka hatua ya ndoa.

**KUHUSU MWENZA**

Kijana wa kiume, aliyelelewa katika familia ya mabilionea, utamaduni na uzoefu unaonyesha atakuwa na mawazo ya kuoa mwanamke ama mwenye uwezo au walau wazazi wake.

Ni aina ya uzoefu kwamba uhusiano wa kimapenzi kwa waliotoka katika familia zenye uwezo, unaambatana na matatizo mengi na unaweza kuvunjika kwa sababu ya kukosekana uaminifu na mapenzi yanapungua, kwa sababu mbalimbali.

Maisha ya ndoa ni safari ndefu. Yanahitaji mapenzi ya dhati na hayana njia za mkato, kwani ndio kianzilishi sumu kuu, tamaa za mwili.

Ni kasoro ambayo, inapopewa nafasi hata kwenye maisha ya ndoa, inachangia kukosekana uvumilivu, upendo na uaminifu.

Safari ya mapenzi kufanikiwa, kunaambatana na shida na taabu nyingi, kabla ya kufanikisha malengo ya msingi. Fedha na utajiri, ina mnafasi ndogo katika kutatua hilo la kijamii na kisaikolojia na hakuna maisha ya ndoa ambayo hayajawahi kupitia katika kipindi cha matatizo.

Mmoja anaweza kuwa kwenye nafasi ya kutoelewa kasoro zake, lakini mwenzake akatambua na akashindwa kuyaanika kwa hofu ya kukaribisha matatizo. Ni hatua ya kukaribisha karaha na kupisha upendo na furaha.

Kuoa na kuolewa, si dhana ya kuwekewa matarajio ya muda mfupi na kusahau mengi ya baadaye inapotokea tatizo la uhusiano, fikra hazitakimbilia fedha, mali na utajiri.

***Imeandaliwa kwa msaada wa ufafanuzi wa kutaaluma kutoka mtandaoni.***





Ujenzi wa tanki la maji ukiwa unaendelea katika kijiji cha Izumbwe, kwajili ya kutekeleza mradi wa maji wa Shongo, ambao unatokana na agizo la Rais Dk. John Magufuli, wakati wa ziara yake mkoani Mbeya. **PICHA: INNOCENT NG'OKO**

# Wakulima watakiwa kukata bima

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WAKULIMA katika mikoa ya Nyanda za juu Kusini wametakiwa kukata bima za kilimo kutoka kwenye kampuni ya Bima za kilimo ili kukabiliana na majanga mbalimbali yatokanayo na shughuli za Kilimo kwa lengo la kujihakikishia usalama wa mazao ya kilimo.

Wito huo umetolewa jana na Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) Kanda ya Nyanda za juu Kusini, Consolata Gabone wakati akizungumzia umuhimu wa wakulima kuwa na bima za kilimo.

Alisema kwa sasa kuna mashirika mengi yanayotoa huduma za bima za kilimo katika mikoa ya nyanda za juu kusini na kuwa ni wakati mwafaka kwa wakulima hao kujiunga na Bima za Kilimo kwajili ya manufaa yao.

Consolata alisema sekta ya kilimo imekuwa na mchango mkubwa sana kwajili ya maendeleo ya kilimo nchini na imekuwa ikichangia pato la taifa na hivyo ni muhimu kwa wakulima kujihakikishia usalama wa mazao yao kwa kukata bima za kilimo.

"Kuna kampuni za bima ambazo zinatoa huduma za bima za kilimo, ni muda mwafaka kwa wakulima kuchangamkia fursa hizo ili kupata fidia ya mazao yao pindi majanga yakiwamo ya mafuriko yanapowakumba wakulima," alisema Consolata.

Alisema kilimo kina mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya viwanda nchini na kuwa wakulima ni lazima waendeshe shughuli za kilimo kwa manufaa kutokana na kuwa na bima za kilimo kwa ajili ya mazao yao.

Aliyataja baadhi ya majanga ambayo wakulima wamekuwa wakikabiliana nayo mara kwa mara kuwa ni wadudu waharibifu kwa mazao,hali ya hewa, wizi wa mazao yao pamoja na majanga mengine yanayohusiana na kilimo.

Consolata alisema umefika wakati kwa wakulima kuhakikisha wanachangamkia mpango huo ili kuondokana na changamoto za mara kwa mara za majanga yatokanayo na Kilimo.

"Unajua mkulima akijiunga na bima za Kilimo kutoka kwenye kampuni zinazojihusisha na bima za kilimo itamuwezesha kujihakikishia usalama wake wa kiuchumi kutokana na kiasi alichowekeza kifidiwa," alisema.

Consolata alisema kampuni za bima zimekuwa na mchango mkubwa katika kuunga jitihada za serikali katika sekta ya kilimo kutokana na kuzingatia kipaumbele cha serikali katika uchumi wa viwanda.

Baadhi ya kampuni zinayotoa bima za kilimo kwa mikoa ya nyanda za juu kusini ni shirika la bila la Taifa(NIC), Jubilee Insurance na MGEN ambayo zimejipanga kuwakomboa wakulima dhidi ya majanga yatokanayo na kilimo chenye tija.

# Rukwa kukabili uharibifu vyanzo maji

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

OFISI ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa imeanza mkakati ya kuweka alama za mipaka (vigingi) kwenye vyanzo vya maji, pamoja na kutoa elimu kwa wananchi wa mikoa mitatu ya mbeya, Rukwa na Katavi ili kukabiliana na tatizo kubwa la uvamizi wa vyanzo hivyo.

Kauli hiyo imetolewa na Ofisa wa Maji Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa, Mkanjilwa Watson, wakati akizungumza na Nipashe jana na kubainisha kuwa mkakati huo ni moja ya mikakati ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaofanywa na baadhi ya wananchi katika maeneo ya vyanzo vya maji.

Alisema licha ya kuwapo kwa sheria za kulinda vyanzo vya maji na kusimamiwa kikamilifu, lakini ofisi ya Bonde la Ziwa Rukwa imeamua kuja na mbinu ya kuweka alama ambazo zitazungushiwa katika vyanzo vyote vya maji kwa mikoa hiyo mitatu ya Mbeya, Rukwa na Katavi.

Aidha alisema kwa muda mrefu kumekuwa na jitihada za kutoa elimu juu ya uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji, hata hivyo hali ya mwitikio imekuwa ni ndogo kutokana na baadhi ya wananchi hususani wakulima na wafugaji wamekuwa wakipuuzia elimu inayotolewa kuhusiana na uhifadhi wa vyanzo hivyo vya maji.

"Mpaka sasa tumefanikiwa kuweka alama za mipaka kwa kuweka vigingi (bicon) kwenye vyanzo katika Wilaya ya Chunya mkoani mbeya na baadhi ya wilaya katika mikoa ya Katavi na Rukwa na kuwa mpango huo kwa sasa unakusudiwa kutekelezwa katika vyanzo vyote vya maji vilivyopo katika Jiji la Mbeya.

Alisema ofisi hiyo ya bonde la Ziwa Rukwa imefanikiwa kuunda jumuiya za watumiaji maji katika maeneo wanayosimamia ili kurahisisha uhifadhi wa vyanzo vya maji katika maeneo hayo yaliyopo katika mikoa hiyo na sehemu ndogo ya mikoa ya Tabora na Singida.

"Mpaka sasa Jumuiya za maji zilizoundwa zinafanya kazi vizuri na zinashirikiana kwa ukaribu na ofisi za wilaya na mikoa katika mikoa tunayoisimamia katika suala zima la uhifadhi wa vyanzo vya maji," alisema.

Mbali na kuwapo kwa mikakati ya kuweka alama katika vyanzo vya maji, ofisi ya bonde la Ziwa Rukwa imekuwa ikishirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) katika kuzalisha miche ambayo inafaa kwa ajili ya kupanda katika vyanzo vya maji vilivyopo katika mikoa hiyo

# NSSF yasisitiza vitambulisho vya Taifa

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) mkoani Mbeya umewataka wanachama wake wote kuwa na vitambulisho vya taifa kwa lengo la kuhakiki taarifa zao na kulipwa stahiki katika mfuko huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa mfuko huo mkoani Mbeya, Nurdin Mruma, alisema kuwa uamuzi huo utasaidia kuwatambua wanachama kwa urahisi zaidi na kuwa vitambulisho vilivyokuwa vikitumiwa awali havitatumika tena na mfuko huo.

Alisema vitambulisho vya taifa ni muhimu katika mambo mbalimbali na kuwa kwa umuhimu huo, NSSF imewataka wanachama wote kuzingatia utaratibu wa kuwa na kitambulisho cha utaifa pindi wanapohitaji huduma ndani ya shirika hilo.

"Unajua vitambulisho hivi vya utaifa ni muhimu katika nyanja mbalimbali na sisi kama NSSF tumewataka wanachama wetu wote kuwa na vitambulisho vya Taifa kwajili ya shughuli mbalimbali zinazohusiana na shirika la NSSF," alisema.

Mruma alisema kuwa kuanzia sasa wanaendelea kuwasiliana na waajiri na wanachama wanaochangia kwa hiyari kuhakikisha wanaharakisha zoezi hilo haraka iwezekanavyo na kuwa iwapo mwanachama hatakuwa na kitambulisho cha Taifa atatakiwa kwenda kujiandikisha na kupata kitambulisho hicho ili kupata huduma.

Alisema kuna mtazamo hafifu kuwa kitambulisho hicho cha Taifa ni kwa ajili ya kusajili simu tu, lakini ukweli ni kuwa vitambulisho, hivyo vitatumika katika nyanja mbalimbali hapa nchini kama ilivyo kwa NSSF ambao wameona umuhimu wa vitambulisho hivyo kwa wanachama.

Mruma alisema NSSF ni moja ya mashirika ya jamii ambayo yana wanachama wengi ambao wamekuwa wakichangia katika shirika hilo kwajili ya kujipatia mafao ya uzeeni na huduma mbalimbali zitokanazo na mfuko huo

Maneja huyo amewataka wanachama kujenga utamaduni wa kuhakiki taarifa kila wakati ili kuboresha taarifa zao kwa lengo la kuepukana na usumbufu wakati wa kujipatia mafao mbalimbali ndani ya shirika hilo kwa sasa kuna zoezi la wastaafu na wategemezi kujihakiki katika mfuko huo.

Alisema kuna wakati maofisa wa shirika hilo wamekuwa wakitumia muda mwingi kufuatilia taarifa za wateja wao wakati wakistaafu ili kulipwa pensheni zao kutokana na wanachama wengi kutojenga utamaduni wa kufuatilia taarifa kila wakati, hivyo kufanya malipo kuchelewa.



# Kesi za kikodi 652 zimesikilizwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, amesema mwaka jana kesi za kodi 652 zenye thamani ya Sh.Trilioni 2.03 na dola za Marekani 81,613 zimesikilizwa Baraza la Rufaa za Kodi(TRAT) na Bodi ya Rufaa za kodi(TRAB).

Kauli hiyo aliitoa juzi bungeni alipokuwa akijibu hoja mbalimbali za wabunge walipokuwa wakichangia taarifa za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali(PAC) na ya Serikali za Mitaa(LAAC). Alieleza kuwa kesi za kodi za mwaka 2017 zote zimeshashughulikiwa na zimebaki kesi 13 za mwaka 2018 ambazo sasa zinashughulikiwa.

Alisema Alhamis (jana) kesi zaidi ya 10 zitatolewa hukumu, kwa sasa Mwenyekiti wa bodi yupo Dar es Salaam, Makamu mwenyekiti yupo Mwanza na baadhi ya wajumbe wapo Arusha, wote wanafanya kazi kwa haraka.

"Kwa sasa mabaraza ya kodi na bodi za rufaa za kodi zinashughulikia kesi za mwaka 2019 na tumepanga ifikapo Juni mwaka huu wawe wamemaliza kesi zote na kuanza kushughulikia kesi zilizofunguliwa mwaka 2020,"alisema

Aliongeza kuwa kasi imekuwa kubwa kushughulikia kesi hizo baada ya Rais John Magufuli kuteua Mwenyekiti na makamu na wajumbe wake.

Awali, katika taarifa ya PAC iliyosomwa na Mwenyekiti wa kamati, Naghenjwa Kaboyoka, alisema kuna ucheleweshaji usiokuwa na tija wa maamuzi ya rufaa za kikodi ambapo jumla ya mashauri 817 ya kikodi yalikuwa hayajashughulikiwa hadi kufikia Juni 30, 2018.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT), Gulamuhafeez Mukadamu, akizungumza wakati wa kuzindua ofisi za makao makuu ya jumuiya hiyo, jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tamisemi yaagiza Halmashauri uchambuzi wa mpango Equip-T

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA za Serikali za Mitaa zimeagizwa kuchambua mafanikio yote yaliyopatikana katika Mpango wa Kuinua Elimu nchini (EQUIP-T) katika shule za msingi ikiwamo utengenezaji wa zana za ufundishaji ili kuwapo na uendelevu wa utekelezaji wa mpango huo.

Mpango huo umetekelezwa kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) kwenye mikoa ya Kigoma, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Dodoma, Singida, Katavi, Mara na Lindi na Halmashauri 63 ambao ulilenga stadi za kujua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gerald Mweli, katika kikao cha wadau na wafadhili wa mradi huo walipokuwa wakifanya tathmini ya mpango huo uliotekelezwa kwa miaka sita. Mweli alisema katika mradi huo walimu wamefundishwa kutengeneza zana za kufundishia zinazopatikana kwenye maeneo yao na kuwataka walimu kuondokana na dhana kwamba zana za kufundishia ni lazima zinunuliwe.

"Unaweza kutumia zana zinazozunguka kwa mfano vifuniko vya soda kwa ajili ya kuhesabu, lakini wamefundishwa namna ya kuandaa program mbalimbali kwa ajili ya elimu ya kujitegemea na serikali itaendelea kutekeleza,"alisema

Aidha, alizitaka mamlaka hizo kutenga fedha za matengenezo ya pikipiki ambazo zilitolewa kwa waratibu kata kupitia mradi huo.

"Tumetoa elimu kwa walimu kwenye mikoa tisa ambao wamepata mafunzo ya kuimarisha ufundishaji wa kusoma, kuandika na kuhesabu," alisema.

Alieleza kuwa mafanikio ya mpango huo yameanza kuonekana mwaka huu ambapo matokeo ya darasa la nne kwenye mikoa hiyo asilimia 91 wanafunzi wamefaulu kuingia darasa la tano wakiwa na stadi tatu za kusoma, kuandika na kuhesabu.

"Ni wajibu wa serikali kuhakikisha mafanikio yote yaliyopatikana katika mradi wa Equip-T yanaendelezwa na matatizo yaliyopatikana kwenye mradi yanatatuliwa," alisema.

Naye, Ofisa Elimu Mkoa wa Tabora, Suzana Mwalubamba, alisema mkoa huo wamepata mafanikio katika uboreshaji wa miundombinu ya shule ambapo kuanzia mwaka 2014 kulikuwa na shule 700 na hadi sasa kuna shule 805 za msingi.

"Kumekuwepo na hamasa kwa jamii kupitia ushirikiano wa walimu na wazazi, walimu wetu pamoja wazazi kwenye shule zote za msingi wamekuwa na vikao vyao ambavyo wanakaa kujadili maendeleo ya shule, mwenendo wa huduma mbalimbali zinazopatikana shuleni na masuala ya nidhamu,"alisema

Kwa upande wake, Mratibu Msaidizi wa mradi huo, Mwalimu Joseph Katabalo, alisema programu hiyo ilianzishwa katika mikoa ambayo ufaulu wake ulikuwa chini kwa miaka mitatatu mfululizo kabla ya program kuanza.

"Hali hiyo ilitokana na kudorora kwa ufaulu wa wanafunzi kwa kushindwa kusoma, kuandika na kuhesabu na imesaidia katika mambo tofauti tofauti ikiwamo kusaidia walimu kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika kuboresha elimu, lakini kutoa mafunzo katika ngazi ya wilaya kuhusiana na namna ya kupanga na kusimamia katika mipango ya elimu na pia namna ya kusimamia shule ili iweze kufanya vizuri katika mambo ya mipango na utawala," alisema mratibu huyo.

# Tasnia ya maziwa yakosa ushindani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa pamoja na serikali kupunguza utitiri wa tozo mbalimbali, lakini bado tasnia ya maziwa haionyeshi ushindani mkubwa kama tasnia zingine nchini.

Hayo yalielezwa jana na Meneja mradi wa Agricultural transforming market (TAM) kutoka Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), Tom Ole Sikar, katika semina iliojumuisha wadau wa tasnia ya maziwa na wawakilishi kutoka ofisi za Serikali na taasisi mbalimbali.

Alisema sekta hiyo haina ushindani kama zilivyo nchi nyingine.

"Tumekutana hapa kwa lengo la kuangalia tatizo gani linayofanya ushindani usiwepo ili hali maziwa yapo mengi na wasindikaji wapo wengi," alisema Ole Sikar.

Alisema mradi huo unafanya kazi na tasnia ya maziwa pamoja na wadau wa alizeti, lengo ni kuhakikisha wanasaidia watu hao kupiga hatua kwa kutatua tatizo lililopo ndani ya sekta hizo ndogo.

Meneja huyo alisema mkutano huo ambao kila mmoja atatoa maoni yake nini kifanyike ili kuingia katika ushindani wa maziwa kama zilivyo nchi nyingine.

"Moja ya kitu ambacho tunahitaji kufanya bodi ya maziwa ni kuhakikisha wanakuwa na mpango wa kufuatilia mabadiliko ya kisera ili yaweze kuleta ushindani soko la ushindani la maziwa," alisema.

Naye,Mdau Wa sekta hiyo, Prof. Lusato Kurwijila, alisema soko la maziwa linahitaji kukua na kuleta ushindani ili wasindikaji na taifa kwa ujumla wanufaike.

Alisema wao kama wadau wa tasnia hiyo, wanapaswa kuleta mabadiliko ya pamoja ambayo yatatoa mwongozo wa kuhakikisha wanakuza tasnia hiyo hapa nchini.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Maziwa nchini (TAMPA), Fabian Mwakatuma, alisema semina iwe chachu ya mabadiliko katika kujenga tasnia ya maziwa nchini.



# Maalim Seif sasa kugombea uenyekiti wa ACT-Wazalendo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MSHAURI wa Chama Cha ACT Wazalendo Maalim Seif Shrif Hamad, jana amechukua fomu ya kugombea nafasi ya uwenyekiti wa chama hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho Vuga Mjini Zanzibar baada ya kuchukua fomu hiyo alisema kuwa ameamua kugombea nafasi hiyo kwa sababu anauwezo na uzoefu wa kutoka katika kukiendesha chama.

Alisema kuwa bado wafuasi wake wanapenda awe kiongozi katika safu ya juu ndani ya chama hicho hakutaka kuwaangusha wafuasi wake na kuamua kugombea nafasi hiyo.

"Wanachama wangu wanapenda niwe katika safu ya uongozi kitaifa hivyo kama sitotumia nafasi hiyo kuwaridhisha hawatonielewa kwa sababu bado wananiamini", alisema Maalim Seif.

Alisema kuwa ameamua kutumia haki yake ya kikatiba kugombea nafasi hiyo kwa sababu anaelewa wazi kuwa nafasi hiyo haihusiani na utendaji katika chama badi nafasi hiyo ni ya uongoozi.

Alieleza kuwa iwapo atachaguliwa nafasi hiyo atahakikisha anashirikiana na viongozi wa chama hicho katika kuleta maendeleo.

Alisema kama wanachama watamridhia kumpa nafasi hiyo atatoa mchango wake katika kukiimarisha na kukiendeleza chama hicho.

"Mwenyekiti wa chama ni kiongozi ambae anatarajiwa atoe uongozi katika na kusimamia chama chenyewe kupitia sera zake.

Aliongeza kwa kusema kuwa "naamini kabisa kwamba ninao uwezo huo, nina uzoefu wa kutosha na wanachama walio wengi katika chama chetu wanapenda niwemo katika safu ya uongozi".

Aidha alisema kuwa kwa kushirikiana na wezake ataweza kuendeleza utamaduni wa kuajibika kwa kila mtu nafasi aliyoiyomba na kuendeleza nidhamu za kufanya kazi kwa ushirikiano.

Alisema uongozi wake kwa kushirikiana na viongozi wezake katika chama hicho wataijenga taasisi hiyo ili miaka mitano ijayo iwe inaungwa mkono na watanzania walio wengi na kuwa mfano wa ndani na nje ya nchi.

"Pia tunataka taasisi yetu iwe inashiriki na kusimamia chaguzi zote za serikali ili ifikapo mwaka 2025 chama hiki kiweze kuongoza halmashauri nyingi za wilaya na miji na kuendelea kuongoza serikali ya Zanzibar na kuwa sehemu ya uongozi wa kitaifa wa serikali ya Jamuhri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema kuwa matumaini yake kuwa wanachama wa chama hicho watamuunga mkono katika safari hiyo ya kugombea uwenyekiti.

Hata hivyo kuhusu kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar kupitia chama hicho alisema kuwa bado ni mapema na wakati utakapofika ataeleza nia yake.

Naye Kaimu Katibu Mkuu wa chama hicho Dorothy Temu aliwataka akina mama na vijana kujitokeza kuchukua fomu kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ili waweze kushiriki katika kujenga chama chao.

Zoezi la uchukuaji fomu kugombea nafasi za ndani za uongozi katika chama hicho lilianza Januari 27 mwaka huu na linatarajiwa kumalizika Febuari mwakani ambapo mpaka sasa mgombea pekee aliyechukua fomu ya kugombea nafasi ya uwenyekiti ni Maalim Seif Sharib Hamad.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kulia), akizungumza na Mkurugenzi wa Sheria na Mahusiano wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC), Godson Kiliza (wa pili kushoto), na ujumbe wake mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Walimu waelezwa kusimamia miongozo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Halmashuri ya Wilaya ya Kusini Unguja, Kassim Abuu Mtoro, amewataka Walimu wakuu wa Shule za msingi na Sekondari katika Halmashauri hiyo kusimamia miongozo na taratibu zilizowekwa na Wizara ya elimu ili kuondosha matokeo mabaya katika Wilaya hiyo.

Aliyasema hayo huko Shule ya Kitogani wakati alipokuwa katika kikao cha kujadili maendeleo ya elimu katika Halmashauri hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema Halmashauri haitosita kuwachukulia hatua walimu watakaoshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Hata hivyo aliwataka Walimu kusomesha kwa kutumia mbinu bora na za kisasa na badala yake waache kusomesha kwa mazoea.

Aidha alimuagiza Naibu Mkurugenzi elimu Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kuweka utaratibu wa kupita kila shehia kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa elimu kwa Watoto wao.

Kwa upande wake Ofisa elimu Wilaya ya Kusini Unguja Hamid Abdulhamid Khamis ,alisema ufaulu wa wanafunzi katika wilaya hiyo hauridhishi kutokana na ushirikiano mdogo kwa baadhi ya Wazazi na walimu, uwajibikaji mdogo wa Walimu wakuu na juhudi ndogo ya Wanafunzi katika kudurusu masomo.

Kwa upande wao baadhi ya Walimu wa wilaya hiyo walisema suala la kuwafanya wanafunzi kufaulu vizuri linahitaji ushirikiano lakini jambo la kusikitisha hutupiwa lawama walimu pekee.

# DC ahimiza upandaji miti kukabili tabianchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, Rajab Ali Rajab, ameitaka jamii kupanda miti ya kudumu katika maeneo yenye mmong'onyoko wa ardhi katika kipindi cha mvua ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Alisema njia pekee ya kukabiliana na mabadiliko ya tabiayanchi ni kupanda miti pamoja na kujiepusha kukata miti ovyo hususan kwa kutumia misumeno ya moto ambayo imeonekana kuwa ndio chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira.

Akizungumza baada ya kushiriki zoezi la upandaji miti katika kijiji cha Mwanakombo Wilayani humo,Mkuu huyo wa Wilaya alisema jamii itumie fursa ya mvua inaoendelea kwa kupanda miti ya kudumu.

Aidha aliwataka masheha kusimamia miti iliyopandwa katika maeneo yao ili iweze kukua vizuri na lengo la serikali la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi liweze kufikiwa.

Hata hivyo Mkuu huyo aliitaka jumuiya isiyo ya kiserikali ya VSO kuendelea kushirikiana na uongozi wa wilaya katika kutoa huduma mbalimbali za kijamii hasa kwa vijana ili kuwakwamua kiuchumi na kuachana na utegemezi.

Naye Ofisa mazingira Wilaya ya Kaskazini B, Mashavu Khamisi Khatibu, alisema lengo la kupanda miti katika eneo hilo ni kuhifadhi kianzio cha maji cha mto mwanakombo ambao umeathirika kutokana na mmong'onyoko wa ardhi.

Kwa upande wake mshauri wa baraza la vijana Zanzibar, Abdon Fidelis, alisema upandaji wa miti katika wilaya hiyo Unalengo la kuwajenga vijana kuwa na sauti ya pamoja katika utunzaji wa mazingira katika maeneo yaliyowazunguka.

# Madiwani Chadema waliohamia CCM kusaidia kampeni uchaguzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Arusha Mjini, Joseph Massawe, amewakaribisha waliokuwa madiwani watatu na Katibu wa Wilaya wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kwenye chama hicho, na kuwataka kuunganisha nguvu ya kupata ushindi mnono uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Aliyasema hayo jijini hapa,wakati akiwapokea wanachama hao wapya kwenye ofisi za chama hicho.

Alisema hawajachelewa wamerudi wakati mwafaka wa uchaguzi mkuu ambao wanahitaji ongezeko la wanachama.

"Kikubwa naomba fuateni taratibu za chama na tunawakaribisha sana kujenga chama," alisema. Katibu wa Chama cha CCM Wilaya ya Arusha, Denis Zakaria, alisema chama chao hakijafunga milango wanahitaji wanachama wengi zaidi.

Alisema ujio wa viongozi wa Chadema unaashiria wengi wao kukubali kazi zinazofanywa na Rais John Magufuli za maendeleo.

Aliyekuwa Katibu wa Chadema Wilaya ya Arusha, Innocent Kisanyage, alidai ametoka Chadema sababu ya kupinga kila kitu wakati yeye anaona kazi zinazofanyika.

Zakaria Mollel wa Olorieni, alidai amejiunga CCM ili ashirikiane na Rais Magufuli kufanya kazi za maendeleo katika kata yake.

"Lakini wale wanaofikiri nimekuja CCM nimehongwa waongo, maana mimi mfanyabiashara hakuna wa kunihonga na Chadema nilitumia fedha zangu nyingi kujenga chama," alidai. Diwani Kata ya Themi, Melace Kinabo alisema ametoka Chadema kwa sababu ya kupata vikwazo vya kimaendeleo.

Diwani wa Unga Limited, James Lyatuu, alishukuru kupokelewa CCM, na kudai kuwa ataungana nao kuiepeleka nchi kwenye uchumi wa kati.




Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti (kushoto), na Mkuu wa Chuo cha Kilimo cha Wazazi Kaole, Sinani Simba, wakifurahia jambo baada ya kusaini makubaliano, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani juzi, yatakayoiwezesha kampuni hiyo kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kilimo wa chuo hicho kila mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu mkwamo wanawake kufanya biashara nje bayana

**Na Happy Severine,** SIMIYU

CHAMA cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC) kimesema kuwa wafanyabiashara wengi wanawake nchini wanashindwa kufanya biashara nje ya nchi kutokana na kutokuwa na elimu ya sheria pamoja na taratibu zinazotumika kwa biashara hizo.

Aidha, kimesema kuwa wanawake wengi wamekuwa wakilalamikia uwapo wa kodi nyingi maeneo ya mipakani wanaingiza bidhaa au malighafi kutoka nje ya nchi, jambo ambalo alisema siyo kweli bali wengi wao hawajui sheria na taratibu za ufanyaji wa biashara hiyo.

Hayo yamesemwa jana na Mwenyekiti wa Chama hicho, Jackline Maleko, wakati wa ufunguzi wa semina ya siku nne kwa wajasiriamali wanawake Mkoa wa Simiyu, inalenga kuwapatia elimu na mbinu za kufanya biashara nje na ndani ya nchi.

Maleko alisema kuwa hatua hiyo imekuwa ikiwazuia wanawake wengi kufanya biashara hizo, ukizingatia Tanzania imepata fursa ya uwapo wa soko la pamoja la Afrika Mashariki, lakini bado wanawake wengi hawajalitumia.

Alisema baadhi ambao wamekuwa wakifanya biashara hizo, wamekuwa wakitumia njia za panya kwa kutumia rushwa na kukwepa kodi, jambo ambalo alisema siyo sahihi.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa kutokana na hali hiyo, chama hicho kiliandaa mkakati wa kuhakikisha kinazunguka nchi nzima na kukutana na wanawake wajasiriamali ili kuwapatia elimu ya ufanyaji biashara hiyo ambapo wamepanga hadi kufikia mwaka 2023 kuwafikia wanawake 10,000.

"Kupitia mpango mkakati wetu kama TWCC wanawake wengi sasa wameanza kufanya biashara za kuvuka mipaka baada ya kupatiwa elimu hii, ndiyo sababu leo tunakutana na wanawake 100 wa Mkoa wa Simiyu kutoka kwenye wilaya zake zote," alisema Maleko.

Alisema mbali na kuwapatia elimu na mbinu za kufanya biashara hizo, chama hicho kimekuwa kikitumia fursa hiyo kuwapatia mikopo yenye riba nafuu kama mitaji pamoja na kuwaelimisha juu ya kutunza kumbukumbu za kifedha.

Awali akifungua semina hiyo Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, aliwataka wanawake kutumia fursa ya mikopo inayotolewa na serikali kupitia asilimia 10 ya halmashauri ili kujiendeleza.

"Hiyo mikopo inayotolewa na hamashuari ni haki yenu, ipo kisheria wala siyo utashi wa mkurugenzi au kiongozi yeyote. Tumieni fursa hiyo kudai hiyo haki na kufuatilia kwenye halmashauri zenu kama wanatoa," alisema Kiswaga.

Mmoja wa wajasiriamali, Wilimina Kundi, alishukuru TWCC kwa kuwaletea mafunzo hayo ambayo yatawasaidia kukuza biashara zao, kwani wengi wao wamekuwa wakiogopa kufanya biashara nje ya nchi kutokana na kodi nyingi.

# Wazee walilia sheria matibabu

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

BARAZA la wazee wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, wameitaka Serikali ipeleke muswada bungeni ili itungwe sheria ya wazee, ambayo itawasaidia kutatuliwa changamoto zao za matibabu bure.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wilayani Kishapu, Suzana Masebu, kwenye kikao cha Baraza hilo na Shirika lisilo la kiserikali la Tawlae linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga.

Masebu alisema kutokana na kukosekana kwa sheria, mambo mengi hayatekelezewi ikiwamo upatikanaji wa vitambulisho vya matibabu bure na dawa kwa wazee.

"Miaka mingi sasa tunalilia kutungiwa sheria ya wazee... hii sera ambayo ipo sasa haina faida kwetu kwa sababu mambo mengi hatutekelezewi kwa vitendo, lakini kama kungekuwa na sheria ya wazee, tungeishi maisha mazuri sana," alisema Masebu.

"Mfano kwenye halmashauri hii ya Kishapu wazee wengi hawana vitambulisho vya matibabu bure, hakuna dawa kwa wazee pamoja na madaktari bingwa wa magonjwa yetu, hivyo tunaomba Serikali itunge sheria ya wazee," aliongeza.

Naye Ofisa ustawi wa jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Rehema Kasita, alikiri baadhi ya wazee wilayani humo hawana vitambulisho vya mat-

# Mil. 700/- kujenga jengo halmashauri

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, imeanza kutekeleza ujenzi wa mradi wa jengo la ofisi unaoghalimu Sh. milioni 700 kwa lengo la kuwasogezea huduma wananchi.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, alisema Halmashauri inatekeleza mradi wa jengo la ofisi lenye ghorofa mbili, na kwamba wataanza na ghorofa moja, huku ghorofa la pili litajengwa baada ya kukamilika baada ya maombi ya mpango huo yatakubaliwa na madiwani.

Alisema mpango huo ulipangwa kuanzia kipindi cha mwaka 2019/2020 baada ya Halmashauri hiyo kupitisha bajeti ya kuimarisha jengo lake kwa kutumia fedha ya Force Account kwa kuwa lina zaidi ya miaka 40.

HABARI KIMATAIFA

## Ufaransa na Uturuki zalaumiana mzozo wa Libya

**PARIS,** Ufaransa

WAKATI Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, akiilaumu Uturuki kukiuka makubaliano ya kusimamisha uingiliaji wa nje kwenye mzozo wa Libya, Uturuki imeilaumu Ufaransa kwa kusababisha kukosekana kwa utulivu nchini humo.

"Hapa nataka pia kuzungumzia wasiwasi wangu kuhusu hatua za karibuni za Uturuki zinazotofautiana na dhamira ya Rais Erdogan kwenye mkutano wa Berlin.

"Siku chache zilizopita tumeziona meli za Uturuki zikiongozana na wanajeshi wa kukodi wa Syria wakiingia kwenye ardhi ya Libya. Huu ni ukiukwaji mkubwa sana wa kile tulichokubaliana Berlin," alisema Rais Macron.

Alisema hayo baada ya mkutano na Waziri Mkuu wa Ugiriki, Kyriakos Mitsotakis uliofanyika mjini Paris.

Hatua hiyo inatokana na makubaliano ya shughuli za majini kati ya Uturuki na Libya yaliyofikiwa mwaka jana, ambayo yangeyawezesha mataifa hayo mawili kuufikia ukanda wa kiuchumi licha ya vikwazo kutoka Ugiriki, Misri na Cyprus, mataifa ambayo kijiografia yanakutana katikati ya Libya na Uturuki.

Rais Macron aliyaelezea makubaliano hayo kama nyaraka zisizo halali na zisizokuwa na msingi wa kisheria na hata kisiasa.

Wakati Rais Macron akitoa kauli hiyo, Uturuki imejibu kwa kuilaumu Ufaransa kuwa ndio chanzo cha kukosekana kwa hali ya utulivu nchini Libya.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Uturuki, Hami Aksoy alisema kwenye taarifa yake kwamba mhusika mkuu wa matatizo ya Libya tangu kuanza kwa mzozo mwaka 2011 ni Ufaransa.

Amenukuliwa akisema "Sio siri tena kwamba Ufaransa imekuwa ikimpatia misaada isiyo na masharti mbabe wa kivita nchini Libya, Khalifa Haftar, ili awe na uamuzi kuhusu masuala ya maliasili za taifa hilo, akisema Macron mara nyingine hujaribu kutengeneza ajenda kwa madai yanayovutia." **DW**

# Bunge lapiga kura ya kumwondoa Gavana

**NAIROBI,** Kenya

BUNGE la Seneti la Kenya limepiga kura ya kumuondoa madarakani Gavana wa Jimbo la Kiambu, Ferdinand Waititu, maarufu 'Babayao' kwa madai ya ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka.

Maseneta 27 kati ya 38 waliopiga kura usiku wa kuamkia Alhamisi, waliidhinisha hoja ya kumwondoa madarakani Waititu iliyopitishwa na Bunge la Kaunti ya Kiambu mwezi Desemba, mwaka 2019.

Safari ya kumfurumusha madarakani, Waititu ilianza mwaka jana katika kaunti yake ya Kiambu wakati madiwani walipopiga kura ya kutokuwa na imani naye.

Madiwani wa Jimbo la Kiambu walidai kuwa, Waititu alijihusisha na ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka, ukiukaji wa katiba na sheria nyinginezo, mashtaka ambayo yaliidhinishwa na Seneti.

Inadaiwa kwamba, Waititu alitumia ushawishi wake kujinufaisha kifedha, kutoa zabuni za mamilioni ya pesa kwa kampuni za jamaa wake kutoa huduma katika kaunti ya Kiambu. Mwaka jana, Waititu, mke wake, Susan Ndung'u na binti yao, Monica Njeri walishtakiwa mahakamani kwa kuchukua zabuni ya fedha za Kenya Sh. milioni 588 (sawa na Dola za Marekani 6,000,000) bila ya kufuata sheria.

**Magavana wengine wanne wanakabiliwa na mashtaka ya kuhusu madai ya ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka miongoni mwao Gavana wa Nairobi, Mike Sonko kwa jina maarufu Sonko.**

Hatua ya serikali ya Kiambu kuzipa zabuni kampuni zinazomilikiwa na watu wa familia ya Waititu ni kwenda kinyume na sehemu ya 66 (8A) ya Sheria ya Ununuzi na Uuzaji wa Bidhaa za Umma 2015.

Sehemu hiyo inasema: "Mtu au jamaa za mtu wanapopewa zabuni katika asasi anayosimamia atakuwa, ametenda kosa kwa mujibu wa sheria ya ununuzi na uuzaji bidhaa."

Waititu ni Gavana wa kwanza kupigiwa kura na Bunge la Seneti nchini humo kwa madai ya ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka.

Kufukuzwa kwa Waititu kumefanyika wakati ambapo Kenya inaonekana kuimarisha vita dhidi ya ufisadi ambao umekithiri hasa miongoni mwa maofisa wa serikali wa kitaifa na majimbo.

Mwanasheria ambaye pia ni mchambuzi wa masuala ya kijamii na kisiasa, Daktari Alutalala Mukhwana alisema kutimuliwa kwa Waititu ni ishara kwamba vita dhidi ya matumizi mabaya ya fedha za umma vimeanza kuzaa matunda.

"Sasa maofisa wa serikali, wabunge na hata magavana itabidi wawe waangalifu katika matumizi ya fedha za umma."

Magavana wengine wanne wanakabiliwa na mashtaka ya kuhusu madai ya ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka miongoni mwao Gavana wa Nairobi, Mike Sonko kwa jina maarufu Sonko.

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta kila mara ameshtumu idara ya mahakama nchini humo kwa madai kwamba haisaidii utawala wake kupambana na ufisadi uliokolea serikalini.

Kwa upande mwingine, Jaji Mkuu wa nchi hiyo, amelalamikia vikali kuhusu hatua ya serikali ya kupunguza bajeti dhidi ya idara ya mahakama, jambo ambalo alisema, linavuruga shughuli na usimamizi na utekelezwaji wa haki. **BBC**




Wasichana waliopokea taulo za kike katika kampeni ya kusaidia wale wasiojiweza Rwanda. Kampeni hiyo imeanzishwa na wasichana 10 na wavulana wawili ya kumaliza ukosefu wa taulo hizo. **PICHA: MTANDAO**

# Mlipuko wa Corona wasababisha familia kutengana

**BEIJING,** China

WAKATI mlipuko wa virusi vya Corona ambavyo vimesababisha maambukizi zaidi ya watu 7,711 na wengine 170 kupoteza maisha nchini China, familia sasa zinalazimishwa kutengana kutokana tatizo hilo.

Mtaalamu wa Teknolojia ya Komputa ambaye ni raia wa Uingereza, Jeff Siddle amejikuta akifanya maamuzi maagumu ya kumuacha mke wake ili asafiri na binti yao, Jasmine mwenye umri wa miaka tisa, kurejea nyumbani kwao.

Siddle na mke wake Sindy, ambaye ni raia wa China walikuwa wamesafiri na binti yao katika jimbo la Hubei ili kusheherekea mwaka mpya wa China pamoja na ndugu zake.

Hubei ni eneo ambalo watu zaidi ya 3,500 wamethibitishwa kuwa na ugonjwa huo, haswa katika mji wa Wuhan, eneo ambalo mlipuko wa ugonjwa huo ulianzia.

Jimbo hilo lina makazi ya raia wa kigeni 10,000 ambao ni wafanyakazi na wanafunzi.

Mataifa mengi yametangaza mipango ya kuwaondoa raia wake katika eneo hilo.

Marekani na Japani tayari wamewaondoa mamia ya raia wake. Siddle anatarajiwa kusafiri Februari Mosi, lakini ndege zote za Wuhan zimefungiwa kutoka na serikali kuufunga uwanja wa ndege na usafiri wote wa umma pamoja na barabara zikiwa ni jitihada za kukabiliana na maambukizi ya virusi vya Corona.

Waliambiwa na mamlaka ya Uingereza kuwa Sindy hawezi kuondoka licha ya kuwa na Hati ya Kusafiria ya kudumu ya Uingereza tangu mwaka 2008, kwa sababu ndege hiyo ni maalum kwa ajili ya kuwaokoa raia wa Uingereza katika mji huo.

"Ofisi ya mambo ya nje imetuambia kuwa ndege hiyo ni kwa ajili ya raia wa Uingereza peke yake kwa sababu mamlaka ya China inakataza raia wake kuondoka nchini humo,"Siddle aliiambia BBC.

"Ilinibidi nifanye maamuzi ya kuondoka na binti yangu ambaye ana hati ya kusafiria ya Uingereza au tubaki wote watatu."

China ni miongoni mwa nchi ambazo haitambui uraia wa nchi mbili.

Familia ya Siddle iliamua kuchagua kutengana, uamuzi ambao unasababisha masikitiko makubwa sana.

"Yalikuwa ni maamuzi magumu sana na yanayoumiza," Siddle alisema. "Kumtenganisha binti wa miaka tisa na mama yake, na hakuna anayejua itachukua muda gani, binti yangu amelia sana, yaani anashindwa kuelewa na amekuwa na majonzi makubwa." **BBC**

# Serikali yajivunia kasi ukusanyaji wa mapato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema wastani wa ukusanyaji mapato ya kodi kwa kati ya Julai-Desemba 2019, nchini umepanda hadi kufikia Sh. trilioni 1.5.

Aidha, imesema hali hiyo inaonyesha dhahiri, uwezo wa nchi wa kuhudumia sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi umezidi kuimarika.

Msemaji mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, aliyasema hayo jana jijini Dodoma, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji serikari ya awamu ya tano katika mambo mbalimbali.

"Kwa miaka mitatu sasa, mafanikio ya serikali ya awamu ya tano katika ukusanyaji wa mapato kwa mwezi ilikuwa ni kutoka Sh. bilioni 850 kwa mwaka 2015 hadi Sh. trilioni 1.3, na sasa wastani wa mwezi ni Sh. trioni 1.5," alisema.

Aidha, alifafanua kuwa kuhusu makusanyo yatokanayo na utalii kwa mujibu wa Ripoti ya Taasisi maarufu za Utalii ya mwishoni mwa mwaka jana, imeonyesha kwa mwaka 2018 Tanzania imekuwa ya nne Afrika kwa kuingiza mapato ya utalii ya Dola za Marekani bilioni 2.43 kutoka Dola bilioni 2.19 mwaka 2017.

"Nchi yetu ni ya kipekee na dunia inajua... katika taarifa ya Novemba, 2019 iliyotolewa na Kituo cha Utangazaji cha CNN, Africas Most Amazing Places To Visit in 2020 Tanzania imekuwa namba moja kupitia Hifadhi ya Serengeti," alisema.

Dk. Abass alitoa wito kwa Watanzania kujenga utaratibu wa kutembelea vivutio vyao katika kukuza uchumi kupitia sekta ya utalii.

Kwa upande wa sekta ya madini alisema kwa mujibu wa taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya Novemba, 2019 Takwimu zinaonyesha kuwa mauzo ya bidhaa zisizo uwa za kawaida mapato yameongezeka kwa asilimia 31.0 kwa sababu kubwa ya kuongezeka mauzo ya dhahabu pamoja na matokeo yaliyoletwa na ujenzi wa viwanda.

"Hadi Novemba, 2019, mauzo ya dhahabu nje ambayo ni asilimia 51.4 ya mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi (bidhaa zisizo za kawaida), yaliongezeka kwa asilimia 41.9 kufikia kiasi cha Dola Bilioni 2.1," alisema.

Alisema mauzo ya bidhaa za viwandani nje yameongezeka kwa asilimia 28.4 kufikia Dola milioni 996 ikichangiwa zaidi na bidhaa kama bidhaa za chuma na mabati, vioo, tumbaku, katani na mbolea

Dk . Abbas akielezea suala la hali ya uchumi alisema kuwa wakati taarifa ya Shirika la Fedha duniani (IMF) ya Januari 20, 2020 ikionyesha kuwa uchumi wa dunia utakua kidogo kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2019/20, mpaka Septemba, 2019 uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara kwa kukua kwa asilimia 6.9.

Alisema ukuaji huo ni ukuaji mkubwa katika nchi za Afrika Mashariki nyuma ya Rwanda pekee na bado nchi iko miongoni mwa nchi za juu kwenye ukanda wa SADC na Afrika kwa ujumla.

Alisema Sekta zilizochangia ukuaji huo ni pamoja na Ujenzi kwa asilimi (16), uchimbaji madini na mawe (13.7), habari na mawasiliano (10.7), maji (9.1) na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (9.0).

Kuhusiana na rushwa katika Ripoti ya Transparency ya 2019 ya Januari 23, 2020, Tanzania imekuwa ya 96 kutoka ya 117 mwaka 2015 na 103 mwaka 2017.

Kwa matokeo hayo Tanzania ni ya pili kwa Afrika Mashariki kwa kutokuwa na rushwa nyuma ya Rwanda.

Hata hivyo, alisema kuwa mafanikio yote hayo yanatokana na msimamo wa Rais Magufuli, mageuzi ya kimfumo na kitaasisi aliyoyafanya ikiwamo kuanzisha Mahakama ya Mafisadi na kuchukua hatua haraka hasa yanapotendeka makosa ya uhujumu uchumi.



Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Japhet Justine (kulia), akizungumza na Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Uwekezaji wa Norway kwa nchi ninazoendelea (Norfund), Tellef Thorleifsson, jijini Dar es Salaam juzi. Thorleifsson na ujumbe wake walikuwa nchini kwa ziara ya kukagua miradi inayofadhiliwa na mfuko huo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya MNB yapata faida asilimia 52

**Na Mwandishi Wetu**

Benki ya NMB imepongeza faida kwa asilimia 52 baada ya kulipa kodi kwa mwaka unaoishia Desemba 31, mwaka jana.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa benki hiyo, Ruth Zaipuna, faida ya benki baada ya kilipa kodi iliongezeka kutoka Sh. bilioni 97.7 mwaka 2018 hadi Sh.bilioni 148.6 mwaka 2019.

Alisema hali hiyo pamoja na mambo mengine imechangiwa na hatua za kubana matumizi. Hivyo gharama za uendeshaji kulingana mwaka hadi mwaka.

Zaipuna alisema kuwa pato kutokana na riba limeongezeka kwa asilimia nne kutoka Sh. bilioni 601.6 mwaka 2018 hadi Sh. bilioni 626.3 mwaka 2019, mapato yasiyofadhiliwa yaliongezeka kwa asilimia 14 kutoka Sh. bilioni 195.9 mwaka 2018 hadi Sh. bilioni 224 mwaka 2019.

Kaimu Mkurugenzi huyo alifafanua zaidi kwamba gharama kwa ajili ya uharibifu zilishuka kwa asilimia 27 kutoka Sh.bilioni 137.3 kwama 2018 hadi Sh. bilioni 100.4 mwaka jana.

Alieleza kwamba hali hiyo ilitokana na kuboreka kwa kiasi kikubwa vitabu vya mikopo pampja na kiwango cha urejeshaji wa mikopo mwa mwaka huo.

Zaipuna pia alieleza kuwa jumla ya mali za benki hiyo zilikua kwa asilimia 15 kutoka Sh. bilioni 5,680 mwaka 2018 hadi Sh. bilioni 6,548 mwaka 2019.

Benki hiyo imesema kuwa mikopo na wateja iliongezeka hadi Sh. bilioni 3,619 likiwa ongezeko la asilimia 12 kutoka Sh. bilioni 3,272 mwaka jana.

Zaipina alisema benki yake inawashukuru wateja, wanahisa, wawekezaji, serikali na wafanyakazi kwa kuendelea kuipa sapoti, kuiamini na kujiamini.

# Standard Chartered yapata ongezeko faida asilimia 29

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Standard Chartered Tanzania imetangaza kufanya vizuri katika mwaka uliopita baada ya kupata faida kabla ya kodi ya Sh. Bilioni 47.14 kutoka Sh. Bilioni 36.44 kwa mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 29.

Taarifa iliyotolewa juzi na benki hiyo ilisema, sambamba na ongezeko la faida, Standard Chartered iliongeza utoaji wa mikopo kwa asilimia 11 kutoka Sh. Milioni 640.12 hadi Sh. 712.52 robo moja kwenda nyingine.

Kutokana na mafanikio hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Standard Chartered, Sanjay Rughani, alisema: "Tuna furaha kutokana na mafanikio haya. Matokeo haya ni kielelezo cha uwezo na nguvu katika mkakati wetu kibiashara, kupitia wafanyakazi wetu wenye ari pamoja na utekelezaji wa malengo yetu na kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Ongezeko la mikopo ya muda mrefu na mfupi limetokana na juhudi zetu na ushirikiano zaidi na wateja wetu waaminifu katika nyanja zote. Pia tulipanua wigo katika utoaji wa huduma za kibenki kwa wateja wetu. Kwa hiyo tunajivunia kubaki washirika waaminifu, kusaidia wadau wetu kwa manufaa zaidi."

Taarifa hiyo pia ilisema benki hiyo pia ilipata matokeo mazuri katika urejeshaji wa mikopo ikiwamo ile ya muda mrefu.

Ofisa Fedha Mkuu wa benki hiyo, Rayson Foya, alisema vitendo vya wateja binafsi na kampuni vilikuwa na mikakati mizuri iliyosababisha matokeo chanya katika urejeshaji.

"Wateja wetu wanaendelea kuwa sababu kuu ya sisi kuwa katika biashara, ndiyo maana tupo hapa kwa mambo mazuri kama jina letu linavyosema. Mwaka 2019 vitengo vyetu vya biashara vilifanya kazi karibu na wateja wetu na kukubaliana katika mipango ya urejeshaji mikopo wenye manufaa kwa pande zote.

Akizungumzia matokeo ya benki kuingia kidigitali kwa njia ya simu, ambao ulizinduliwa na kuingizwa katika soko Februari, mwaka jana, Rughani alisema mwaka 2019 benki ilikua kwa kiwango kikubwa hasa katika kuongeza wateja.

Hatua hiyo, alisema imethibitisha kuwa Watanzania wamekua kidigitali zaidi kwa kutumia simu za mkononi katika kufanya miamala ya kibenki. Hatua hiyo pia imewezesha shughuli zote za kibenki, kuanzia kufungua akaunti na miamala ya kibenki kufanyika kwa njia ya mtandao.

Kutokana na mafanikio hayo, Rughani alisema benki itaendelea kutekeleza mkakati wake ambao unalenga kutoa huduma kwa gharama zenye ufanisi pamoja na kufanya kazi kwa karibu na serikali kwa kusaidia kutekeleza ajenda yake ya kitaifa ya maendeleo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL.**

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


### KUPOTEA KWA CHETI



MESHACK JACOB MALICK anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha sita chenye index namba S.0629-0684 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **EDMUND RICE SINON SEKONDARI** mwaka 2016.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. 991081150233.**

115606702

### KUPOTEA KWA CHETI



**Tekla Dongo Bahame** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1227-0041 kilichoctolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya Sekondari Misasi.

Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
MWA/NY/RB/66730/2020

115606302

### PRO SHARE CAPITAL LIMITED

Magari yanayouzwa

1. **JOHN N. RUSIBAMAYILA** (S/LEGACY T413 CXX)
2. **JOHN N. RUSIBAMAYILA** (S/IMPREZA T150 DBT)
3. **GRENTINA B. KIDULILE** (T/IST T993 DMT)
4. **FIELD LOGISTICS LTD** (BEDFORD T680 BGP)

### TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Mariam Silim Hemed** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Suzuki Swift yenye namba za usajili T 138 CBZ.

Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Taarifa ya polisi
**KAH/ /RB/ 650/2020.**

215610002

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu, **JOHN IGENGE ZAKAYO** wa S.L.P 1370 Mwanza,anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba **T.504 DKT Engine No AGN 220975 Rangi Silver CHASIS No WAU2228LZYA116229.**

Kwa atakayeiona atoetaarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa
**KUMB: MWA/NY/RB/24215/2020.**

115608902

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**DEEP CONSTRUCTION LIMITED** Anatangaza kupotelewa na kadi za gari Zenye namba za usajili T 134 AQQ (TRAILER), T 882 AWL (SCANIA) na T 882 AVC (TRAILER).

Yeyote atakaziona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi,

**Taarifa ya Polisi: MOR/MOR/RB/6153/2020.**

215609802

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GSM MOTORBIKE LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 289 BNB.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/MAG/RB/93868/2020.

115609002

### KUPOTEA KWA KADI

Happiness Lotti Msonga anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina TOYOTA HARRIER yenye namba ya usjili T739 DGW iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: MBE/MBE/RB/93938/2020**

115611102

### KUPOTEA KWA KADI

**Jackline Christopher** Kiwango anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaj yenye namba MC589 BYP iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DAR/GOG/94647/2020

215610102

### KUPOTEA KWA KADI

**Jackline Christopher Kiwango** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaj yenye namba MC331 CAM iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.
Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/GOG/94647/2020**

215610102

### KUFUNGA KAMPUNI

Tunapenda kutoa taarifa kuwa Kampuni ya **EDUMART LOGISTICS COMPANY LIMITED** inafungwa rasmi kuanzia tarehe **27/01/2020.** Kwa taarifa hii Kampuni ya **EDUMART** haitahusika na madai au biashara yoyote itakayofanyika kwa jina hili.

Imetolewa na

**MASOUD MAJID M ASOUD KWA NIABA YA BODI YA WAKURUGENZI EDUMART LOGISTICS COMPANY LIMITED.**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

SLIVESTER YAKOBO HANDI amepotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 406 CJU.Aina yake SANLG.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi :
**Ref.No/RB/177/2019.**

215609702

### HATI YA KIAPO

**KUKIRI KUPOTELEWA NA OFFER YENYE USAJILI WA PLOT NO. 644 KITALU "B" NEW NGUVUMALI YENYE JINA LA bibi HILDA MSONDE:**

Mimi LIGHTNESS FANUEL KIAZE wa S.L.P TANGA, Mkristo mtu mzima na mwenye akili zangu timamu ninathibitisha kama ifuatayo.

1. Kwamba mimi ndiye muapaji nilietajwa hapo juu. Mmiliki halali kwa sasa wa kiwanja Na. 644 Kitalu"B" Kilichopo katika eneo la New Nguvumali, kata ya nguvumali, Tanga Mjini.
2. Kwamba **OFFER, HIYO NINATHIBITISHA KUWA IMEPOTEA MIKONONI MWANGU MIMI LIGHTNESS FANUEL KIAZE.**
3. Kwamba nimejaribu kuitafuta kwa juhudi zangu sijafanikiwa nimetoa taarifa Polisi na kupatiwa **LOSS REPORT TAN/RB/85039/2020.**
4. Kwamba naiomba Ofisi ya Mipango Miji, pamoja na polisi Mkoa wa Tanga itambue upotevu huu na ninathibitisha imepotea mikononi mwangu mimi muapaji, nipo tayari kulipa kodi zote husika za serikali.

**UTHIBITISHO;** Nakiri na kuapa, kiapo hichi na kuyatamka haya yote nikiwa na akili zangu timamu na bila ya kushawishiwa na mtu yeyote na kukiri kwa kuweka saini yangu hapa chini kama ifuatavyo.

LIGHTNESS FANUEL KIAZE

115611202


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose*

*Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku Tupigie*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SETIEN ARIDHISHWA NA KIKOSI CHA BARCA



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Quique Setien angependa kuwakaribisha nyota wapya Barcelona Januari hii, lakini ana furaha kufanya kazi na kikosi alichokikuta na kumaliza nacho msimu.

Dili la kumsajili mshambuliaji, Rodrigo Moreno, lilionekana kama linalowezekana baada ya kocha wa Valencia, Albert Celades, kuthibitisha Jumanne kuwa klabu hizo mbili zilikuwa kwenye mazungumzo kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania.

Hata hivyo, taarifa kutoka kwa vyombo vya habari vya Katalunya zimedai kwamba, uhamisho huo hautawezekana, na kuwaacha Barca wakiwa na pengo la fowadi baada ya kuumia goti kwa Luis Suarez, ambaye atakikosa kipindi chote cha msimu kilichobakia.

Setien alithibitisha kwamba mabingwa hao wa LaLaiga walikuwa na mpango wa kuongeza mshambuliaji kabla ya dirisha la usajili kufungwa, lakini sasa mpango huo umeshindikana.

"Kitu cha kwanza, nina furana na kile nilichokikuta kwenye kikosi," alisema Setien akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana Alhamisi wa Kombe la Copa del Rey dhidi ya Leganes.

"Hatuwezi kukataa kuwa tungependa kuongeza mchezaji wakati huu wa usajili, lakini naendelea na kile nilicho nacho.

# Zidane: Vazquez ana mapenzi yangu yote

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amemwelezea Lucas Vazquez kuwa ana "mapenzi yangu yote" baada ya winga huyo kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati Real Madrid wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Real Zaragoza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania aliifungia Madrid bao la pili baada ya lile la ufunguzi la Raphael Varane.

Mabao mengine ya kipindi cha pili kutoka kwa Vinicius Junior na Karim Benzema yaliwapeleka Los Blancos kwenye robo fainali ya Kombe la Copa del Rey, juzi Jumatano.

Vazquez mara zote amekuwa akizua maswali kwa kutokuwa na kiwango bora hapo Madrid, lakini Zidane amebakia kuwa shabiki mkubwa kwa ubora wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.

"Jambo la muhimu ni kile ninachofikiria kuhusu yeye. Ana mapenzi yangu yote, namwamini Lucas kwa sababu ni kijana anayejitoa kwa kila kitu akiwa uwanjani," alisema Zidane.

"Watu wanaweza kutoa maoni yao na unatakiwa kuyakubali. Ni mchezaji aliyetokea timu ya vijana na watu wanachotaka kukiona kutoka kwa mchezaji ni kujitoa kwa kila kitu uwanjani na Lucas anafanya hivyo."





# United wamalizana na Bruno Fernandes

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imefikia makubaliano ya kumsajili Bruno Fernandes kutoka Sporting CP, imetangazwa Jumatano.

Usajili wa Fernandes kwenda pale Old Trafford ulikuwa unasubiriwa vipimo vya afya pamoja na makubaliano ya maslahi binafsi.

Sporting iliweka video kwenye ukurasa wake wa Twitter ikimuaga mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 25, ambaye ameigharimu United ada ya awali ya euro milioni 55 na inatarajia kuongeza nyingine euro milioni 25.

Mashetani hao wekundu watamlipa bonasi Fernandes ya euro milioni 5 kama itafuzu kushiriki Ligi ya mabingwa Ulaya na euro milioni 15 kama bonasi binafsi.

Sporting watakuwa wakipata faida ya asilimia 10 kwa mauzo yoyote ya Fernandez kwa siku za usoni.

Video hiyo ya Sporting ya kumuaga mchezaji huyo pia ilikuwa na maneno yasemayo: "Wengine wamezaliwa kuwa wakubwa, kufikia mafanikio fulani. Asante nahodha wetu."

Uvumi wa kumsajili Fernandes kwenda pale Old Trafford ulivuma kwa miezi kadhaa ya hivi karibuni, lakini dili hilo lilionekana kama lisingefanikiwa baada ya United kuripotiwa awali kwamba imekataa kufikia ada inayotakiwa na Sporting.

## Joao Felix kuikosa Madrid

**MADRID,** Hispania

JOAO Felix anatarajiwa kutoichezea Atletico Madrid kwenye mchezo wa 'dabi' ya jiji moja dhidi ya Real Madrid baada ya kuumia misuli ya mguu wake wa kulia.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno aliumia wakati wa mchezo wa Jumapili wa sare ya bila kufungana dhidi ya Leganes na alishindwa kufanya mazoezi Jumanne na Jumatano.

"Joao Felix ameumia misuli ya kwenye mguu wake wa kulia wakati wa mchezo wa Jumapili dhidi ya Deportivo Leganes," ilisomeka taarifa ya klabu hiyo.

"Amepewa siku za kupumzika, huku timu ya madaktari ikiendelea na matibabu kuona ni lini anaweza kurudi uwanjani."

Huku kukiwa hakuna muda uliotajwa kwamba atarejea uwanjani, ripoti za vyombo vya habari vya Hispania vimesema kwamba, ataukosa mchezo wa Jumamosi pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Joao Felix alitua hapo kwenye dimba la Wanda Metropolitano kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 126 akitokea Benfica Julai mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 amekuwa hana bahati tangu atue hapo Hispania, akifunga mabao mawili tu na kutoa 'asisti' moja kwenye mechi 17 za LaLiga.

Atletico wapo nafasi ya tano kwenye msimamo, wakipitwa pointi 10 na vinara Madrid.







# EVERTON YAWABANIA BARCA KWA RICHARLISON

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inaonekana haitaweza kumsajili mshambuliaji Richarlison wa Everton licha ya kuhusishwa na raia huyo wa Brazil ambaye thamani yake ni pauni milioni 85.

Kwa mujibu wa Sky Sports, miamba hao wa soka la Hispania walikuwa wanamwania Richarlison kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ushambuliaji, baada ya kuumia kwa Luis Suarez ambaye atakikosa kipindi chote cha msimu kilichobakia.

Sky Sports imedai kwamba Everton imekataa ofa kutoka kwa Barcelona, ambayo Mkurugenzi wake wa michezo, Eric Abidal akitajwa kuvutiwa zaidi na mchezaji huyo wa zamani wa Watford.

Hata hivyo, Omnisport inaeleza kuwa dili hilo halitaweza kufanyika kwa sababu Everton hawako tayari kumwachia.

Richarlison alisaini mkataba wa miaka mitano na timu hiyo ya Ligi Kuu England Desemba mwaka jana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 anatarajiwa kuwa nguzo kubwa ya kikosi hicho kwa siku za usoni.

Huku Carlo Ancelotti akiwa amechukua mikoba ya kuinoa timu hiyo kabla ya Krismasi mwaka jana, Everton wana matumaini makubwa ya kuendelea kubakia na Richarlison.

Nyota huyo amefunga mabao nane na kutoa 'asisiti' tatu kwenye mechi 22 za Ligi Kuu msimu huu, baada ya kufunga mabao 13 wakati akianza kuichezea timu hiyo msimu wa 2018-19.

# *Conte: Sikutaka kumtumia Eriksen*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte hakuwa tayari kumwanzisha haraka Christian Eriksen kwenye mchezo wake wa kwanza Inter Milan, lakini alifanya hivyo kwa sababu ya kutokuwa na chaguo la kiungo mwingine wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Fiorentina.

Eriksen alikamilisha usajili kutoka Tottenham na kutua Inter Jumanne, akiwa mchezaji wa tatu kwa miamba hao wa Serie A kusajiliwa Januari hii baada ya Ashley Young na Victor Moses.

Conte alimwingiza Eriksen zikiwa zimesalia dakika 24 katika mchezo huo wa robo fainali ya Kombe la Coppa Italia Jumatano, huku Nicolo Barella akifunga bao la ushindi sekunde 42 baadaye.

Kiungo mchezeshaji huyo, ambaye alichukua nafasi ya Alexis Sanchez kutoka benchi, alionekana kama ametoa 'asisti' yake ya kwanza ya bao wakati alipomlisha mpira Lautaro Martinez na kufunga bao la tatu, lakini lilikataliwa kwa madai ya kuotea.

Hata hivyo, Conte alibainisha kwamba hakuwa na mpango wa kumchezesha Eriksen haraka baada ya kutua San Siro.

"Hatukutarajia kumtumia Eriksen haraka hivyo, kwa sababu alianza mazoezi na sisi jana tu (juzi), lakini viungo Matias Vecino na Barella walikuwapo," alisema Conte akiiambia Rai Sport.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ADEBAYOR MBIONI KUREJEA ENGLAND

Klabu tatu zinawania saini ya mshambuliaji huyo ambaye ana rekodi ya kufunga mabao 97...

**LONDON,** England

KLABU tatu zinazoshiriki Ligi Kuu England zimeonyesha nia ya kumrejesha nchini humo straika wa zamani wa Arsenal, Emmanuel Adebayor, imefahamika.

**Aston Villa, Newcastle na Brighton zinatajwa kufanya mchakato wa kumpa ofa ya mkataba mfupi wa kurejea England, Adebayor (35), ambaye anatarajiwa kujiongezea heshima kwa kupachika mabao.**

Adebayor ambaye ni mchezaji huru tangu Desemba mwaka jana alipoondoka katika klabu ya Kayserispor ya Uturuki, anaweza kusaini mkataba na moja ya klabu hiyo kabla ya dirisha dogo la usajili halijafungwa leo Ijumaa.

Nyota huyo ambaye ni raia wa Togo anatarajia kukamilisha ndoto yake ya kucheza England kwa mara ya mwisho na huenda akafikia rekodi ya kupachika wavuni mabao 100 kwenye ligi hiyo.

Adebayor, ambaye aliwahi kuichezea Arsenal, Manchester City, Tottenham na Crystal Palace zote za England, anashikilia rekodi ya kufunga mabao 97 kwenye Ligi Kuu England.

Mshambuliaji huyo mwenye urefu wa futi 6 na inchi 3 alikuwa akicheza soka nchini Uturuki tangu Januari 2017 alipojiunga na Istanbul Basaksehir.

Mechi yake ya mwisho kucheza katika Ligi Kuu England akiwa na Crystal Palace ilikuwa ni Februari 13, mwaka 2016 alifunga bao wakati timu yake maarufu Eagles ikiwa nyumbani ilichapwa magoli 2-1 na Watford.

Kwa mara ya kwanza mshambuliaji huyo alitua London Kaskazini miaka 14 iliyopita baada ya Arsene Wenger kumsajili kwa dau la pauni milioni tatu akitokea Monaco.

Tukio lake la kukumbukwa alilolifanya kwenye Ligi Kuu England ilikuwa ni kuseleleka kuanzia mwanzo wa uwanja hadi mwisho akishangilia bao alilofunga Septemba 2009 dhidi ya Arsenal akiwa na kikosi cha Manchester City.

## ZISIKUPITE

### EVERTON YAIBANIA BARCA

MABOSI wa Everton wamekataa kupokea ofa ya pauni milioni 85 kutoka Barcelona kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Richarlison,. ***(Sky Sports)***

### BARCA YASAKA STRAIKA

MABINGWA wa Ligi Kuu Hispania, Barcelona wanafanya jitihada za kila namna kuhakikisha wanakamilisha usajili wa mshambuliaji mpya kabla ya dirisha la usajili halijafungwa leo ili kuziba pengo la straika wa Uruguay, Luis Suarez (33), ambaye ni majeruhi. ***(Sport)***

### BALE AKARIBIA SPURS

TOTTENHAM inaendelea na mazungumzo ya kukamilisha usajili wa kushtukiza wa mshambuliaji wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale ambaye ana umri wa miaka 30. ***(Mail)***

### THAMANI YA HAALAND HII

BORUSSIA Dortmund imeweka wazi kuwa thamani ya straika wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland, ambaye ana umri wa miaka 19 ni pauni milioni 63 na litaboreshwa ifikapo majira ya joto mwakani. ***(Bild - in German)***

### CHELSEA, NAPOLI WATETA

CHELSEA imeanza mazungumzo na Napoli kwa ajili ya kufanya mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Dries Mertens (32), kabla ya dirisha la usajili halijafungwa leo. Thamani ya mchezaji huyo ni pauni milioni sita. ***(Mail)***

### ATLETICO YAIGOMEA PSG

ATLETICO Madrid imekataa kuongeza dau la pauni milioni 12.6 kuwapa PSG ili kufanikisha usajili wa mshambuliaji Edison Cavani. ***(Le Parisien - in French)***

### JOSE ANUKIA SPURS

TOTTENHAM iko katika mazungumzo na Real Sociedad kwa ajili ya kunasa saini ya straika wa Timu ya Taifa ya Brazil, Willian Jose (28), ambaye thamani yake imetajwa katika mkataba ni pauni milioni 59. ***(ESPN)***

### PIATEK KUTUA UJERUMANI

HERTHA Berlin inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Poland na AC Milan, Krzysztof Piatek (24), ambaye pia anawindwa na Tottenham. ***(Sky Sports)***

### KALOU ATAJWA WEST HAM

WEST Ham imepeleka maombi ya kumsajili kiungo wa Hertha Berlin na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Salomon Kalou, ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 34. ***(Express)***

### UNITED YAMFUATA RAKITIC

MANCHESTER United imewasiliana na Barcelona kwa ajili ya kuwania saini ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Rakitic (31). ***(ESPN)***

### KOULIBALY HAKIJAELEWEKA

BEKI wa Napoli na Timu ya Taifa ya Senegal, Kalidou Koulibaly (28), hatajiunga na Ligi Kuu England mwezi huu licha ya Manchester United kuonyesha nia ya kumsajili katika dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufungwa leo usiku. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

# LALA SALAMA LIGI KUU Z'BAR KUANZA JUMATATU

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Malindi itawakaribisha KMKM katika mechi ya kwanza ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar msimu wa 2019/20 itakayochezwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Amaan.

**Ligi hiyo ilisimama kupisha zoezi la usajili la dirisha dogo pamoja na mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yalimalizika kwa Mtibwa Sugar kuibuka mabingwa wapya wa michuano hiyo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Hussein Ahmada, alisema maandalizi ya hatua hiyo ya lala salama yamekamilika na wanatarajia timu zote kuonyesha ushindani katika kila mechi.

Ahmada alisema ligi hiyo inaytoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itamalizika ifikapo Aprili 19, mwaka huu.

"Maandalizi ya ligi hiyo yamekamilika katika hatua ya awali na timu zinazopaswa kuanza kucheza Kisiwani Pemba kutoka hapa Unguja zinatarajiwa kusafiri Jumapili kuelekea katika mechi zake," alisema Ahmada.

Hata hivyo alisema baadhi ya mechi za ligi hiyo huenda zikafanyiwa mabadiliko na hiyo itatokana na ratiba za usafiri wa meli kutoka Unguja kwenda Pemba na kurejea Unguja.

Aliongeza uamuzi wa baadhi ya mechi kuchezwa kuanzia saa 8:00 mchana unatokana na kuhitaji kumaliza msimu kabla ya kuanza kwa mwezi Ramadhani.

Alisema pia mechi za viporo vya mzunguko wa kwanza zimepangwa muda huo wa mchana ili kuvimaliza kwa wakati.

Mechi nyingine zitakazochezwa Jumatatu ni kati ya Mwenge dhidi ya Jang'ombe Boys kwenye Uwanja wa Gombani wakati Chipukizi itawakaribisha Polisi kwenye Uwanja wa Mau na Chuoni itawakaribisha Selem View.



Mshambuliaji wa Simba B, Omary Kazi (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Temeke Squad, Magai John, katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Sauti za Busara kupinga unyanyasaji

**Na Elizabeth Zaya**

TAMASHA la Sauti za Busara limepangwa kufanyika kuanzia Februari 13 hadi 16, mwaka huu, huku likijikita katika kupinga vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia wanavyokutana navyo baadhi ya wasanii.

Mkurugenzi wa tamasha hilo ambalo mwaka huu linafanyika katika msimu wa 17, Yusuf Mahmoud, alisema litafanyika katika eneo la Mji Mkongwe Visiwani Zanzibar.

Mahmoud alisema katika tamasha hilo wanatarajia kuwaalika wasanii kutoka hapa nchini na mataifa mbalimbali barani Afrika.

"Katika tamasha la mwaka huu, tuna kampeni inayosema 'Paza sauti, kataa unyanyasaji wa kijinsia'. Na tumeona kwamba tuliwekee mkazo hii ili kuwasaidia vijana wengi hasa wa kike wanaochipukia katika tasnia hiyo ambao wamekuwa wakinyanyaswa kijinsia,"alisema Mahmoud.

"Kila mtu anajua Tamasha la Sauti za Busara lina umuhimu wake katika nchi ya Tanzania, tumekuwa tukitangaza nchi katika sekta ya uwekezaji, kupitia wageni wengi wanaokuja, utamaduni, tunachangia pato la taifa, na pia tunachangia kutoa ajira kwa vijana wengi,"alisema.

Alisema tamasha hilo limekuwa likiwasaidia wasanii wengi na kwamba baadhi yao wameunganishwa na wasanii wakubwa duniani.

"Tunaona manufaa makubwa yanayotokana na tamasha hili, wapo ambao wamefika mbali kwa kujulikana na kufanya kazi na wasanii wakubwa duniani na ni matumaini yetu tuendelee kuwasaidia, licha ya kuwa tunachangia katika pato la nchi kupitia wageni wanaokuja kila mwaka na hata kuleta wawekezaji,"Mahmoud alisema.

Naye Meneja wa tamasha hilo, Journey Ramadhani, alisema wameamua kuweka nguvu zaidi katika kukemea unyanyasaji huo na wameunda timu ya wasanii kutoka ndani na nje ya nchi ambayo watatumia jukwaa hilo kuimba nyimbo za kukemea vitendo hivyo.

Ramadhani alisema pia wamealika wadau wa tasnia nyingine ili kuongeza nguvu katika kutumia jukwaa hilo kukemea vitendo hivyo vya unyanyasaji.

## JKU, KVZ, Chuoni zasonga mbele

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU za JKU, KVZ, Chuoni, Dula Boys na Gulioni FC zimefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la FA (Zanzibar) baada ya kufanya vizuri katika mechi zao zilizopita kutoka Kanda ya Unguja.

Bado timu tatu zinasubiriwa kuungana katika hatua hiyo ambayo bingwa wake hupata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizunguma na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Mohammed, alisema wanafurahi kuona ratiba ya michuano hiyo imekwenda kama ilivyopangwa.

Hata hivyo Mohammed alisema wamepokea malalamiko kutoka katika timu ya Uhamiaji ikiilalamikia Malindi imechezesha wachezaji ambao hawapo katika leseni katika mchezo uliomalizika kwa Uhamiaji kufungwa bao 1-0.

"Kesi hiyo ipo katika kamati ya rufaa na itatolewa uamuzi ili waweze kupanga ratiba ya hatua ya robo fainali ya michuano hiyo," alisema kiongozi huyo.

Michuano hiyo ilianza kwa kushirikisha timu 68 na kati ya hizo, Pemba ilitoa timu 36 kwa upande wa Unguja iliwakilishwa na klabu 32.

## Gofu ya Lugalo kufanyika Jumapili

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Jeshi ya gofu yamepangwa kufanyika Jumapili kwenye klabu ya Lugalo jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa Jeshi Lugalo, Selemani Semunyu alisema mashindano hayo ni ya kwanza kufanyika kwa mwaka huu.

Semunyu alisema kuwa mashindano ya mwaka huu yameboreshwa na wanawaalika wachezaji kutoka sehemu mbalimbali kushiriki michuano hiyo.

"Mashindano hayo hufanyika kila mwezi, tunaomba wadau wajitokeze kwa wingi siku ya mashindano," alisema Semunyu.

Alisema kuwa mabadiliko yaliyofanywa katika mashindano hayo yanalenga kuongeza idadi ya washiriki tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita.

"Mwaka huu tumeboresha zawadi tofauti na mwaka jana, tunaomba wadau waje kwa wingi, na tunawakumbusha pia mchezo wa gofu ni wa wote," Semunyu alisema.



Michezo
Ijumaa Januari 31, 2020
Nipashe



Adebayor mbioni kurejea England

UKURASA 30



Wachezaji wa Manchester United, Fred (kushoto) na Aaron Wan-Bissaka (kulia), wakipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Manchester City, Joao Cancelo katika mechi ya marudiano ya nusu fainali ya Kombe la Ligi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad juzi usiku. United ilishinda bao 1-0, lakini ilitolewa katika mashindano hayo kwa matokeo ya jumla. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, YANGA VITANI MACHI 8

## ●●● Ni katika mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye...

**Na Somoe Ng'itu**

MECHI ya marudiano ya watani wa jadi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20, Yanga dhidi ya Simba imepangwa kufanyika Machi 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Kwa mujibu wa ratiba hiyo iliyotolewa na Bodi ya Ligi kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), jana mwenyeji wa mchezo huo ambao wa raundi ya 28 ni Yanga inayofundishwa na Kocha Mkuu Mbelgiji Luc Eymael.**

Katika mechi hiyo, timu hizo zitashuka dimbani zikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya mabao 2-2, ambayo walipata katika mchezo wa mzunguko wa kwanza iliyochezwa Januari 4, mwaka huu jijini.

Matokeo hayo bado yamekuwa yakiwaumiza mashabiki wa Simba baada ya kuamini timu yao ingeondoka na pointi tatu na yakionekana kufurahiwa na Yanga ambayo ilidhani 'jahazi' lao limezama baada ya kuwa nyuma kwa magoli 2-0.

Magoli ya Simba inayonolewa na Sven Vandenbroeck, raia wa Ubelgiji katika mchezo huo uliochezeshwa na refa Jonesia Rukyaa kutoka Bukoba yalifungwa na Meddie Kagera na Deo Kanda huku ya Yanga yakipachikwa kimiani na Mapinduzi Balama na Mohammed Issa 'Banka'.

Ratiba hiyo inaonyesha kuwa Simba itashuka dimbani kesho kuwakaribisha Coastal Union kutoka jijini Tanga na Februari 4, mwaka huu itawavaa Polisi Tanzania, mechi zote zikichezwa jijini wakati Mtibwa Sugar itawafuata Yanga Jumapili na Februari 5, mwaka huu itacheza dhidi ya Lipuli FC ya mkoani Iringa.

Yanga ambayo ina mechi pungufu, itashuka tena uwanjani Februari 8, mwaka huu ikiwa mgeni wa Ruvu Shooting na siku tatu baadaye itawakaribisha Mbeya City wakati Simba itakuwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro kuwavaa wenyeji Mtibwa Sugar na baada ya hapo itaelekea Iringa kucheza dhidi ya Lipuli FC hapo Februari 15, mwaka huu.

Ratiba hiyo inaonyesha raundi ya tano ya mechi za mashindano ya Kombe la FA zitachezwa kati ya Februari 25 na 26 mwaka huu huku msimu ukipangwa kumalizika katikati ya Mei.

Hata hivyo, mapema jana Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Stephen Mguto, alisema ofisi yake 'ilijisahau' kuwapangia Yanga mechi katikati ya wiki hii kwa ajili ya kumaliza 'viporo' walivyonavyo.

"Vijana wangu walijisahau kuwapangia Yanga mechi katikati ya wiki hii baada ya kumaliza mchezo wao wa Kombe la FA, walipaswa kucheza katikati ya wiki kama zilivyocheza timu nyingine," Mguto alisema.

Simba itafunga pazia la msimu huu kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi dhidi ya wenyeji Polisi Tanzania wakati Lipuli FC itawakaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Samora mkoani Iringa.

## Sven afunguka kinachowatesa

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema wachezaji wake hawachezi kandanda la kuvutia kutokana na uchovu.

Sven alisema hali ya uchovu inayowakabili nyota wake inasababisha kushindwa kuendana na kasi ya ushindani kutoka kwa wapinzani wao, lakini anajipanga kumaliza tatizo hilo.

Kocha huyo alisema kuwa changamoto hiyo inafanya timu yake kupata ushindi kwa 'tabu' tofauti na ilivyokuwa wakati anajiunga na kikosi hicho.

"Sijaridhishwa na kiwango tulichokionyesha, tunapiga pasi nyuma badala ya kwenda mbele, hilo ni jambo ambalo tutalifanyia kazi katika mchezo ujao," alisema kocha huyo ambaye amerithi mikoba ya Mbelgiji mwenzake, Patrick Aussems.

## Azam, Mtibwa hakuna mbabe

**Na Adam Fungamwango**

AZAM FC imeshindwa kupata pointi tatu na kuongeza pengo la pointi nane badala ya sita baina yake ya vinara Simba, baada ya kulazimishwa sare ya nyumbani ya bao 1-1 dhidi ya Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana.

Mtibwa Sugar ndio ilianza kupata bao dakika ya 66 kupitia kwa Riffat Hamisi, baada ya kupata pasi fupi ya kona na kuipiga moja kwa moja na kujaa wavuni huku ukisindikizwa na kipa wa Azam FC, Razack Abarola wakati akijaribu kuokoa na dakika 10 baadaye Azam ilisawazisha bao kwa mkwaju wa penalti, iliyopachikwa wavuni na Richard Djoji, baada ya Idd Selemani 'Nado' kuchezewa madhambi ndani ya eneo la hatari.

Kwa matokeo hayo, Azam inaendelea kushika nafasi ya pili ikiwa na pointi 36, huku vinara Simba wakiendelea kupeta kileleni na pointi zao 44 huku Mtibwa Sugar ikikamata nafasi ya 10, ikiwa imejikusanyia pointi 23 kwa michezo 17 ambayo tayari imeshacheza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >